RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam. Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527,
Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. FA.27/249/01/2011/201242/01

Tarehe 28 Machi, 2013

Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Sanduku la Posta 9120,
Ikulu,
DAR ES SALAAM.

Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (ilivyorekebishwa 2005), nawasilisha kwako ripoti yangu ya sita ya mwaka ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama ilivyoelezewa katika Sehemu ya 3 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Ripoti hii inajumuisha taarifa za ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma 126 kwa vipindi vilivyoishia tarehe 30 Septemba, 2011, 31 Disemba, 2011 na tarehe 30 Juni, 2012.

Nawasilisha kwako ripoti hii kwa ajili ya kuiwasilisha Bungeni kulingana na matakwa ya sheria.

Ludovick S.L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(Imeanzishwa kwa Mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

Kazi na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali vimeainishwa katika Ibara 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (ilivyorekebishwa 2005) na kufafanuliwa na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008 (ilivyorekebishwa) na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

Dira ya Ofisi
Kuwa kituo bora kwenye ukaguzi wa hesabu katika sekta ya ukaguzi wa umma.

Lengo la Ofisi
Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji unaozingatia thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora unaostahili, Ofisi inaongozwa na vigezo vya misingi vifuatavyo:

Kutopendelea	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.
Ubora	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalam inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma vya Kimataifa.
Uadilifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha kwa maadili ya kazi kiwango cha juu na kuheshimu sheria.

Kujali Watu	Tunajali mahitaji ya wadau kwa kujenga utamaduni mzuri wa kujali wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na tija.
Ubunifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya Taasisi.
Matumizi bora ya Rasilimali za Umma	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake.

YALIYOMO

Ukurasa

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali v

Dira na Lengo la Ofisi v

Majedwali ix

Vielelezo xi

SHUKRANI xiii

MUHTASARI xvii

SURA YA KWANZA.. 1

Utangulizi na Taarifa za Jumla 1

SURA YA PILI... 9

Aina za Hati za Ukaguzi Zilizotolewa 9

SURA YA TATU 17

Muhtasari wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Miaka Iliyopita 17

SURA YA NNE 29

Masuala Muhimu Ambayo Hayakutolewa Taarifa Katika Ripoti ya Mwaka Uliotangulia 29

SURA YA TANO 37

Usimamizi wa Sheria ya Manunuzi na Mikataba 37

SURA YA SITA..57

Usimamizi wa Mali za Umma..57

SURA YA SABA 77

Usimamizi wa Rasilimali Watu 77

SURA YA NANE 87
Utawala Bora...87

SURA YA TISA... 103
Vitega Uchumi vya Serikali, Umiliki/Uwekezaji wa Serikali na Mchakato wa Ubinafsishaji 103

SURA YA KUMI 113
Matokeo ya Kaguzi Maalum 113

SURA YA KUMI NA MOJA... 125
Matokeo Yatokanayo na Kaguzi za Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali .... .125

SURA YA KUMI NA MBILI 135
Hitimisho na Mapendekezo.. 135

VIAMBATANISHO 150

MAJEDWALI

Ukurasa

Jedwali Na 1: Mgawanyo wa Kazi za Ukaguzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa Mwaka 2011/2012 7

Jedwali Na 2: Kuwasilisha Hesabu 12

Jedwali Na 3: Mchanganuo wa Hati Zilizotelewa kwa Mashirika ya Umma kwa Miaka Mitatu Mfululizo 13

Jedwali Na 4: Orodha ya Mashirika Yasio na Hati Miliki 59

Jedwali Na 5: Hali Mbaya ya Ufanisi Kifedha kwa BAKITA 60

Jedwali Na 6: Mikopo Ambayo Hailipiki 62

Jedwali Na 7: Wateja Wapya Ambao Hawapo Kwenye Kumbukumbu za Mikopo 66

Jedwali Na 8: Madeni ya Biashara ya Muda Mrefu 69

Jedwali Na 9: Matukio ya Ujangili TANAPA 73

Jedwali Na 10: Doria Zilizofanyika Katika Baadhi ya Hifadhi 74

Jedwali Na 11: Manahodha Waliopo na Muda wao wa Kustaafu.. 83

Jedwali Na 12: Mwenendo wa Gawio, Ulipaji wa Mikopo na Mapato Mengine 107

VIELELEZO

Ukurasa

Kielelezo Na 1: Mgawanyo wa Kazi za Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa Mwaka 2011/2012 7

Kielelezo Na 2: Mchanganuo wa Hati Zilizotolewa Kwa Kipindi cha Miaka Mitatu Mfululizo Kutoka 2009/2010 Hadi 2011/2012. . 14

Kielelezo Na 3: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi kwa Kila Mwaka (Miaka 3 Kuanzia 2009/10 hadi 2011/12) 15

Kielelezo Na 4: Ongezeko la Deni la Wizara ya Afya Wanalodaiwa na MSD.. 32

Kielelezo Na 5: Mwenendo wa Gawio, Ulipaji wa Mikopo na Mapato Mengineyo Kuanzia Mwaka wa Hesabu 2008/2009 hadi 2011/2012..108

Kielelezo Na 6: Ongezeko la Mashirika Yanayokaguliwa 130

SHUKRANI

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za mara kwa mara za kutilia msisitizo kwenye ripoti zangu za jumla za mwaka za ukaguzi.

Shukrani zangu za dhati pia ziende kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wenyeviti na waheshimiwa wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge na Wabunge wote kujitoa kwa dhati kujadili mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti yangu.

Napenda, kutoa shukrani zangu za dhati kwa Bodi za Wakurugenzi, Watendaji Wakuu na wafanyakazi wote wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma za Umma zilizokaguliwa kwa ushirikiano walioutoa kwa wakaguzi wakati wa zoezi zima la ukaguzi.

Vilevile, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kukamilisha uchapaji wa ripoti hii na hivyo kuifanya itoke na kuweza kupelekwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge kwa muda uliowekwa kisheria.

Zaidi, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wabia wa maendeleo ambao wamekuwa wakitoa msaada kwa Ofisi yangu hususani Mpango wa Maboresho wa Menejimenti ya Fedha za Umma (PFMRP) chini ya usimamizi wa Benki ya Dunia, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO), Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Watu wa Sweden (SIDA), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID) ya Uingereza, Benki ya Maendeleo ya Africa (ADB), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya India (SAI India) kupitia Serikali ya India, Serikali ya watu wa Marekani kupitia Shirika lao la Maendeleo (USAID), Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la Maendeleo (GIZ) na wadau wote wanaoitakia mema Ofisi yangu na waliochangia kwa sehemu kubwa kuifanya kuwa ya kisasa kwa kufadhili mafunzo ya

wafanyakazi na kutupatia vifaa mbalimbali zikiwemo kompyuta na Magari.

Zaidi ya hayo, napenda kuzishukuru Kampuni Binafsi za Ukaguzi ambazo zimekuwa zikifanya kazi za ukaguzi kwa niaba ya Ofisi yangu katika ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru sana wafanyakazi wangu wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kujitolea kwao na uvumilivu waliouonyesha katika kukamilisha ripoti hii, umekuwa wa manufaa na faraja sana kwangu.

Kwa ujumla wigo wa ukaguzi umepanuka baada ya ofisi yangu kuungana na Ofisi ya Ukaguzi wa Hesabu ya Uingereza pamoja na Ofisi ya Ukaguzi wa Hesabu ya China kuunda Bodi ya Ukaguzi wa Umoja wa Mataifa kwa miaka sita ijayo kuanzia tarehe 1 Julai, 2012. Nawasihi wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi waendelee kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa bidii na umoja kwa siku zijazo ili kuendelea kudumisha heshima ya Ofisi yetu katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora, kuhimiza uwajibikaji na kuzingatia thamani ya fedha katika makusanyo na matumizi ya rasilimali za Umma.

DIBAJI

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya sita ya mwaka ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012. Ripoti hii ni mkusanyiko wa ripoti za kaguzi mbalimbali za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine zilizofanyika kwa kipindi husika. Ripoti hii inaainisha masuala yanayozorotesha ufanisi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma katika kutekeleza na kufikia malengo waliyojiwekea.

Lengo la ripoti hii, ni kuwataarifu wadau kama vile Serikali, Bunge, Mahakama, Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kijamii na Umma wa Watanzania kwa ujumla, kuhusu muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo za Umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012, pamoja na kutoa mapendekezo kwa lengo la kuboresha ufanisi wa Mashirika na Taasisi hizo. Ripoti hii imechambua mambo mbalimbali ambayo yameonekana kwa njia moja au nyingine kuathiri ufanisi na uwajibikaji wa Mashirika hayo katika kufikia malengo yake. Katika kipindi hiki ambacho kimekuwa na ongezeko kubwa la uwajibikaji kwa umma, uwazi na utawala bora ni jambo la muhimu kwa watendaji kutoa taarifa zao za utendaji ikiwa ni pamoja na taarifa za fedha na usimamiaji wa mali za umma ndani ya Mashirika na Taasisi za Umma. Napenda kueleza kuwa ripoti hii imetayarishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka, 2008.

Ili kuhakikisha kuwa kazi yangu inachangia katika maendeleo ya Taifa, ofisi yangu imekuwa ikipitia na kuboresha mbinu za ukaguzi mara kwa mara ili kuona kuwa matokeo ya kaguzi yanakidhi haja za wadau wangu. Kujenga uwezo wa wakaguzi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni jambo linalopewa kipaumbele kikubwa ili kuhakikisha wanapata uelewa wa sheria, miongozo, kanuni na matoleo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na mabadiliko yanayofanywa na Taasisi za taaluma ya uhasibu na ukaguzi za kimataifa kama vile “IFAC”, “INTOSAI” na nyinginezo ambazo ofisi yangu ni mwanachama.

Kutokana na jitihada hizo, Wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wamekuwa wakipewa mafunzo, ili kuongeza ubora na ufanisi katika kufanya kazi. Kwa mtazamo huo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina mpango wa kujenga Kituo cha mafunzo ya ukaguzi katika eneo la Gezaulole Kigamboni-Dar es Salaam. Ninayo imani kubwa kuwa Serikali kwa kutambua umuhimu wa mafunzo kwa wakaguzi, itaisadia ofisi yangu katika maeneo yote ya msingi ili kufanikisha mradi huu.

Ni vyema ikafahamika kwamba, wakati vyombo vyenye dhamana ya uangalizi (Oversight Organs) vina jukumu la kuhakikisha kuwa Sheria na taratibu zinafuatwa ndani ya Taasisi za umma, Bodi za Wakurugenzi na Maafisa Watendaji Wakuu wa Taasisi hizo kwa upande wao wana jukumu la kuweka mifumo imara ya udhibiti wa ndani na miongozo ili kuhakikisha kwamba sheria na taratibu hizo zinafuatwa.

Juu ya yote, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake kwa ujumla, Kamati za Bunge za usimamizi wa utendaji, Bunge kwa ujumla, Wadau wa Maendeleo hasa Benki ya Dunia, Taasisi zisizo za Kiserikali vyombo vya Habari kwa michango yao katika kufanikisha uwajibikaji katika nchi yetu.

Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

MUHTASARI

i. Utangulizi

Muhtasari huu unaainisha kwa kifupi hoja mahususi zilizojadiliwa kwa kina katika sura husika za ripoti hii na zinazohitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti husika ili kuhakikisha kunakuwepo utendaji wa Mashirika ya Umma wenye ufanisi.

Mambo yanayozungumzwa kwenye ripoti hii yanajumuisha: aina ya maoni ya ukaguzi yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa mujibu wa kifungu cha 33(3) cha Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka, 2008; muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita; masuala muhimu ambayo hayakutolewa taarifa katika ripoti za miaka iliyopita; Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba, Usimamizi wa Mali za kudumu; Usimamizi wa Rasilimali Watu; Utawala Bora; Utendaji wa uwekezaji wa Serikali na mwenendo wa mchakato wa ubinafsishaji na ukaguzi Maalum kama ifuatavyo:

ii. Hali za Ukaguzi na Ripoti Zilizokaguliwa

Kufikia tarehe 28 Feburuari, 2013 nimefanikiwa kuhitimisha kaguzi 126 (71.6%) kati ya kaguzi 176 zilizotakiwa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika kaguzi zilizokamilika mashirika 95 ripoti zake zilikamilika na kuridhiwa na Bodi za wakurugenzi na maoni ya ukaguzi kutolewa, wakati mashirika 31 yanasubiri hesabu kuthibitishwa na kusainiwa na Bodi za Wakurugenzi. Sababu kuu ya kuchelewa kusainiwa kwa ripoti hizi ni pamoja na kutokuwepo kwa Bodi za Wakurugenzi katika baadhi ya mashirika pamoja na kuchelewa; kuitisha vikao vya Bodi za Wakurugenzi vya kuridhia hesabu kwa wakati kama sheria inavyoelekeza. Hali kadhalika, pamekuwepo na ucheleweshwaji wa majibu juu ya hoja za ukaguzi uliopelekea kuchelewesha zoezi la ukaguzi kumalizika kwa wakati. Ninashauri mamlaka husika, kuhakikisha kwamba

Bodi za Wakurugenzi zinateuliwa kwa wakati pindi muda wake unapokwisha.

iii Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka Iliyopita

Katika ripoti za miaka iliyopita, kuna jumla ya mapendekezo 25 ambayo bado hayajatekelezwa na yameandikwa kwa muhtasari katika sura ya tatu ya ripoti hii. Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa hayajatekelezwa kwa zaidi ya miaka minne kitendo ambacho kinaonyesha kuwa watendaji wakuu na Bodi za Mashirika husika hawatekelezi majukumu yao vizuri. Mapendekezo yanayokaa muda mrefu bila kutekelezwa yanaweza kusababisha kurudiwa kwa mapungufu hayo katika miaka inayofuata hayo na kwa hali hiyo inarudisha nyuma ufanisi wa udhibiti wa rasilimali za umma katika taasisi husika.

Ningependa kueleza kwamba majibu yaliyotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali hayakutosheleza kujibu hoja zilizotolewa kwa sababu mapendekezo mengi bado hayajatekelezwa. Natoa ushauri kwa serikali kwamba hatua madhubuti zichukuliwe katika kutekeleza mapendekezo yote ya miaka iliyopita ili kuongeza uwajibikaji na upatikananji wa thamani ya fedha matumizi ya rasilimali za Taifa.

iv Masuala Muhimu Ambayo Hayakutolewa Taarifa Katika Ripoti ya Mwaka Uliotangulia

Mahitaji ya nyumba Tanzania yanakadiriwa kuongezeka kwa kiasi kikubwa, kiasi kwamba kuna haja ya kuweka mkakati mkubwa wa uwekezaji kwenye nyumba kwa kadri ya ongezeko la idadi ya watu inavyoongezeka. Kwa sasa upungufu huu wa makazi Tanzania unakadiriwa kuwa nyumba milioni 3, na mahitaji yanategemewa kuongezeka kwa kiwango cha nyumba 200,000 kwa kila mwaka. Upungufu huu unatokana na ukuaji wa kasi wa mahitaji ya nyumba kwa kila mwaka kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu mijini. Ukuaji huu hutoa fursa kubwa kwa uchumi wa nchi pia. Ingawa serikali imechukua hatua mbalimbali kwa lengo la kupunguza uhaba wa nyumba kwa kutunga na kurekebisha

sheria mbalimbali ili kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi kushiriki, bado sekta hii haifanyi vizuri na inahitaji msukumo zaidi. Ningependa kulipongeza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuonyesha njia katika kutafuta uvumbuzi wa tatizo hili hapa nchini.

Bohari ya Madawa ambayo ndiyo inayowajibika na ununuzi na usambazaji wa madawa na vifaa vingine vya hospitali kwa niaba ya Serikali, haifanyi vizuri kutokana na sababu zifuatazo; mtiririko usioridhisha wa fedha toka Wizara ya Fedha kwenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, na kisha Bohari ya Madawa kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa madawa haya kumekuwepo pia ugumu katika usuluhishi wa taarifa za hesabu kati ya Bohari ya Madawa, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii nawadau wengine kama Taasisi ya Mifupa Muhimbili. Hii inaleta mashaka ya taarifa za hesabu za pande zinazohusika. Kwa hiyo inashauriwa kuwa Wizara ya Fedha na Wizara ya Afya zinapaswa kila mara kutoa taarifa za fedha zinazopelekwa Bohari ya Madawa kwa ajili ya manunuzi ya madawa na kufanya usuluhishi wa taarifa za pande zote zinazohusika ili kuhakikisha kuwa taarifa zinazotolewa ni sahihi. Vile vile Bohari ya Madawa inapaswa kuzijulisha halmashauri zote nchini kuhugu mgao wa fedha zilizopelekwa kwa ajili ya ununuzi wa Madawa na vifaa vya hospitali.

Kwa miaka mingi, VETA imekuwa ikikua kwa kasi bila ya kupitia na kufanya tathimini ya muundo uliopo ili kuona kama unakidhi mahitaji ya Mamlaka. Aidha, mfumo wa uhasibu wa VETA, hautoi habari na takwimu za kuaminika ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya kufanya maamuzi kwa kuwa mfumo hauwezi kuunganisha ofisi za kanda na makao makuu. Ukosefu huu wa mfumo ambao unaweza kuziunganisha ofisi za kanda na makao makuu, unazuia upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wakati muafaka kwa ajili ya maamuzi ya namna ya kusimamia na kudhibiti rasilimali za taasisi hii.

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iliripoti kiasi cha Shilingi bilioni 793.5 ikiwa ni kiasi cha mkopo ambacho Bodi inadai kutoka kwa watu mbali mbali waliokopeshwa kwa ajili ya kusoma elimu ya juu. Kiasi hiki kinajumuisha kiasi chote kilichokopeshwa tangu mwaka 1994 wakati mpango wa kuchangia gharama za masomo ulipoanzishwa.

Kwa mujibu wa kiwango cha Kimataifa cha hesabu Na.36, Bodi ilipaswa kufanya tathimini ya kupungua kwa thamani ya fedha inazodai. Kutokana na ukweli kwamba kuna dalili zote za kutorejeshwa kwa fedha zote zilizokopeshwa kwa wanafunzi, hivyo tathmini ya hasara ya upungufu wa thamani ya mkopo ifanyike na kuingizwa kwenye vitabu vya hesabu kwa kuwa si sahihi kuripoti kwenye vitabu vya Bodi deni la Shilingi 793.5 bilioni ambalo ni dhahiri kuwa halitakusanywa lote.

Kiasi cha Shilingi milioni 317.8 zilizotolewa kama mikopo kwa walengwa mbalimbali bila kuzingatia mifumo na kanuni za udhibiti wa fedha. Baadhi ya nyaraka zilizotumika kwenye malipo hazikupitiwa na kuidhinishwa na maafisa waandamizi. Kulikuwa na wizi wa kughushi nyaraka na kuiba fedha za Bodi zipatazo Shilingi milioni 90.8 uliofanyika makao makuu ya Bodi ya Mikopo. Pia kulikuwa na malipo ya kughushi kupitia fedha zilizopelekwa Chuo Kikuu cha Mkwawa ambako jumla ya Shilingi milioni 66.1 ziliibiwa.

Aidha, Bodi imekuwa ikitoa mikopo kwa walengwa bila kupitia nyaraka vizuri. Kwa mfano, Bodi ilitoa mikopo kwa ajili ya utafiti kwa wanafunzi wa mwaka wa tatu (3) wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa zipatazo Shilingi milioni 15.5 pasipo kuwa na nyaraka muhimu zinazotakiwa.

V Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba

Usimamizi wa ununuzi na mikataba ni eneo muhimu sana linalohitaji kutazamwa na kusimamiwa vizuri na taasisi zote zinazohusika kwenye manunuzi. Karibu asilimia sabini na

tano (75%) ya bajeti ya mwaka ya nchi inatumika kwenye manunuzi ya bidhaa na huduma. Hii ndio sababu iliyopelekea serikali na vyombo vyake kuona umuhimu wa kutunga sheria ya manunuzi ya umma namba 21 ya mwaka 2004. Napenda kutambua mchango mkubwa na juhudi zinazofanywa na Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Manunuzi ya Umma katika kuhuisha mifumo ya manunuzi iliyo wazi, makini na yenye manufaa kiuchumi na inayoleta thamani ya fedha. Mamlaka hii imekuwa ikifanya jitihada za kujenga uwezo katika nchi kwa kuweka viwango stahiki katika mifumo ya manunuzi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kinyume na matarajio haya na jitihada zinazofanywa na mamlaka husika bado kuna baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo bado hazizingatii matakwa ya Sheria ya Manunuzi namba 21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005. Ukaguzi huu umebaini mapungufu ambayo ni muhimu kutolewa taarifa kwa ajili ya Serikali kufanyia maamuzi. Mambo muhimu ambayo yaliripotiwa katika Mashirika yaliyokaguliwa ni kama: manunuzi ya dharura yaliyofanyika bila idhini mrejesho ya Mlipaji Mkuu wa Serikali, manunuzi yaliyofanyika bila kuwa na mikataba, manunuzi yaliyofanyika nje ya mpango wa manunuzi ulioidhinishwa, muingiliano katika mihimili mikuu ya manunuzi, matumizi yasiyo sahihi ya njia za manunuzi, matumizi katika manunuzi yasiyofuata bajeti, na udhaifu katika kusimamia mikataba. Napenda kuweka wazi juu ya matumizi yasiyokuwa na faida ya kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 2.2 zilizolipwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa mkandarasi Oceana Advanced Industries Ltd ikiwa ni tozo lililosababishwa kwa kukatisha mkataba wa matengenezo ya eneo la maegesho ya meli "berth No.1-11" kwa mkandarasi. Malipo haya yangeweza kuepukika kama mkataba ungesimamiwa ipasavyo.

Ilielezwa kuwa tozo la malipo lilisababishwa na menejimenti kushindwa kukabidhi eneo la maegesho Na.7 (berth No.7) kwa mkandarasi kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano.

Vi Usimamizi wa Rasilimali

Nilibaini kwamba mafao yote ya PSPF yaliyokomaa katika miaka mitano ya kipindi cha mpito kutoka tarehe 1 Julai, 1999 hadi tarehe 30 julai, 2004 yalilipwa na Wizara ya Fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund). Katika mtazamo huu, hakuna mafao yaliyolipwa kutokana na Mfuko katika kipindi cha mpito. Malipo ya mafao chini ya kifungu kilichotolewa yalianza rasmi tarehe 1 Julai, 2004. Ukadiriaji wa thamani uliofanyika mara ya mwisho na kukamilika tarehe 30 Juni, 2010, uliashiria kwamba uwezo wa kifedha wa PSPF uliendelea kushuka. Ukadiriaji wa thamani ulibaini hasara halisi ya Shilingi bilioni 6,487 kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010. Hivyo hali ya mfuko wa hifadhi ya jamii uko katika hatari ya kutokuendelea kama hatua madhubuti hazitachukuliwa na pande zinazohusika.

Pia nilibaini kwamba Shirika la Utangazaji Tanzania limeripoti hasara ya kiuendeshaji ya Shilingi 1.6 bilioni (Mwaka 2011; Shilingi 3.5 Bilioni). Mwishoni mwa mwaka, Shirika lilikuwa na hali ya kutoweza kulipa madeni yake likiwa na deni halisi la Shilingi bilioni 2.7 (Mwaka 2011, bilioni 1.1) na kiasi kikubwa linategemea Serikali kwa usaidizi wa kifedha katika kujiendesha na kulipia madeni kwa wakati ujao. Hali hii inaleta wasiwasi mkubwa kuhusiana na uwezo wa Shirika kuendelea kujiendesha lenyewe katika kipindi kijacho.

Wakati wa ukaguzi wa Chuo kikuu cha Dodoma, nilibaini mali ya kiasi cha Shilingi bilioni 452 iliyopo katika Chuo lakini haikujumuishwa katika vitabu vya mahesabu vya Chuo. Majengo ya chuo hiki yalikamilika na kukabidhiwa kwa viongozi wa Chuo kwa ajili ya matumizi. Mifuko ya Jamii ilifadhili ujenzi wa majengo ya Chuo chini ya maelekezo ya Serikali. Majengo hadi sasa hayajakabidhiwa rasmi kwa Chuo Kikuu Dodoma na Serikali ambayo ilisaini mkataba na Mifuko ya Jamii NSSF, PSPF, LAPF na PPF.

Pia nilibaini kuwa utengefu wa madeni yenye wasiwasi wa kulipwa na wadaiwa ya Shilingi 83 bilioni ulifanyika bila ya kupata idhini katika Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC). Utengefu wa Shilingi 83 bilioni unaowakilisha asilimia 85 ya madeni yote yenye kiasi cha Shilingi 98 bilioni ambayo yalilirithiwa na CHC kutoka PSRC. Utengefu wa kiasi kikubwa cha madeni uliofanyika na CHC kuhusu madeni haya unapunguza juhudi za urejeshaji wa mikopo hiyo toka kwa wadaiwa wa shirika.

Katika Chuo Kikuu Huria Tanzania, nilibaini madhaifu makubwa yakijumuisha udhaifu wa urari wa taarifa za kibenki zisizo sahihi ambazo zilileta wasiwasi juu ya usahihi wa kiasi cha Shilingi 7 bilioni kilichoripotiwa kama fedha taslimu na fedha taslimu linganifu. Taarifa za usuluhishi wa kibenki za akaunti tano kwa kipindi chote cha kuanzia Juni, 2011-Juni 2012 hazikutolewa kwa ajili ya uthibitisho wa ukaguzi. Ripoti Maalum ya ukaguzi wa ndani katika chuo Kikuu Huria Tanzania ulibaini matumizi mabaya ya fedha yenye jumla ya thamani ya Shilingi milioni 700.1. Ilielezwa kwamba kiasi hiki kimetokana na Shilingi 219.9 milioni ambazo zilipatikana kupitia fedha za Bodi ya Mikopo na Shilingi 480 milioni ambazo zilipatikana kupitia ofisi ya Msajili wa Hazina kwa njia ya malipo ya udanganyifu kwa watu wasiostahiki na ubadhilifu huu haukutolewa taarifa katika vitabu vya mahesabu vya Chuo.

Wakati wa ukaguzi wa TANAPA, nilibaini kuwa vitendo vya uwindaji haramu hususani kwa tembo viliongezeka na kufikia jumla ya tembo 110 waliouawa katika kipindi cha mwaka 2011/2012. Kuongezeka kwa matukio ya vitendo vya uwindaji haramu katika Hifadhi imechangiwa na kutofanyika kwa doria za kutosha za askari pori ambapo kuna kila dalili ya kusababisha ongezeko la wawindaji haramu katika mbuga za hifadhi zetu. Menejimenti ya TANAPA inapaswa kuhakikisha kwamba doria ya askari pori inaboreshwa na kutekelezwa ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya askari,

kuwapatia vifaa vya kisasa na vya kutosha kulinda rasilimali hizo za Taifa.

Vii Usimamizi wa Rasilimali Watu

Rasilimali watu ni kiungo muhimu katika idara mbalimbali za shirika na uhitaji uangalifu mkubwa katika kufikia mahitaji ya wafanyakazi. Ukaguzi ulibaini ucheleweshwaji wa michango ya watumishi kwenye mifuko ya pensheni, mapungufu katika kufanya tathmini za utendaji wa watumishi wa mashirika, majalada ya watumishi wa mashirika kukosa taarifa muhimu, kuwepo kwa nafasi nyeti kwenye mashirika ambazo hazijajazwa, baadhi ya mashirika kutokuwa na mpango wa mafunzo na ukosefu wa mpango wa kukasimisha madaraka kwenye mashirika na usimamizi usioridhisha. Maelezo ya mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi na mapendekezo yameelezewa kwenye sura ya saba ya ripoti hii.

Viii Utawala Bora katika Mashirika ya Umma

Kama nilivyoripoti katika ripoti iliyopita kuhusu wabunge kuteuliwa katika nyadhifa za Ujumbe wa Bodi katika Mashirika ya Umma mbalimbali, mwaka huu pia nimebaini kuendelea kwa utaratibu huo wa kuwateua wabunge kuwa wajumbe katika Bodi za wakurugenzi wa mashirika mbalimbali. Tatizo hili la wabunge kuwa katika Bodi za wakurugenzi limejitokeza katika Shirika la Madini la Taifa, Bodi ya Utalii, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Kituo cha Diplomasia, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi na Bodi ya Korosho Tanzania.

Kinyume na kanuni za utawala bora, kumekuwepo na kasumba ya Wizara mama kuingilia shughuli za kiutendaji za mashirika yaliyoko chini yake kwa kutoa maelekezo mbalimbali.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Maliasili na Utalii ilihamisha kiasi cha fedha Shilingi milioni

771.2 kwenda Bodi ya Utalii Tanzania na baadae yakatolewa maelekezo mbalimbali ya fedha hizo kitu cha kushangaza, kiasi cha fedha chenye jumla ya Shilingi milioni 416.1 kilichukuliwa na wafanyakazi wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa matumizi yasiohusiana na Bodi ya Utalii na kiasi cha jumla ya Shilingi milioni 355.1 kililipwa wazabuni, watoa huduma na Taasisi nyingine kwa maelekezo ya Wizara.

Mwingiliano wa Wizara katika shughuli za taasisi za umma unaondoa dhana ya uwajibikaji wa Bodi za Wakurugezi katika kutekeleza shughuli za usimamizi wa taasisi hizo.

Wizara ilitoa maagizo kama hayo kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuchanga Shilingi 34.9 milioni kwa Wizara ya Mali Asili na Utalii kwa ajili ya mishahara ya miezi 4 kwa mfanyakazi aliyeko nchini Japan. Mamlaka ya Ngorongoro ilipe gharama za wabunge kuhudhuria maonyesho ya biashara ya kimataifa, kuchanga Shilingi 340 milioni kwa ajili ya kutangaza utalii nchini Marekani, na kuchanga Shilingi 5.171 bilioni kwa ajili ya ununuzi wa helikopta aina ya Bell 407, japokuwa agizo hili halikutekelezwa. Mwingiliano mwingine wa wizara mama kwa mashirika umeonekana pale ambapo Wizara ya Maji ilihamisha Shilingi milioni 28.6 kwenda Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara na baadaye Mhasibu kutoka Wizara akaenda kuzichukua kwa matumizi yasiyokuwa ya mamlaka ya maji.

Katika Shirika la Masoko Kariakoo, kumekuwepo na uteuzi wa Bodi ya Wakurugenzi kinyume na Sheria. Sheria iliyoanzisha shirika inataka Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ateuliwe na Rais na wajumbe wengine wateuliwe na Waziri mwenye dhamana, badala yake wajumbe hao waliteuliwa na Jiji la Dar es Salaam.

ix Vitega Uchumi vya Serikali Pamoja na Mchakato wa Ubinafsishaji

Kulingana na mapitio ya utendaji katika vitega uchumi vya serikali pamoja na maendeleo ya ubinafsishaji nilibaini kuwa,

Vitega uchumi vya ndani viliongezeka kwa Shilingi trilioni 1.939, ikiwa ni ongezeko kutoka Shilingi trilioni 10.276 tarehe 30 Juni, 2011 hadi kufikia Shilingi trilioni 12.215 katika mwaka huu wa ukaguzi. Ongezeko kubwa limetokana na kuongezeka kwa Mashirika ya Umma/ Taasisi za serikali kutoka 204 kwa mwaka 2010/2011 hadi 213 kwa mwaka 2011/2012 na ongezeko la thamani ya mali zilizothaminishwa upya.

Mapato ya Serikali yaliyokusanywa na Msajili wa Hazina kama gawiwo, malipo ya mikopo na mapato mengineyo yaliongezeka kwa Shilingi bilioni 179.3 ambayo ni sawa na asilimia 622.8 kutoka Shilingi bilioni 28.8 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 mpaka kufikia Shilingi bilioni 208.1 katika mwaka huu wa ukaguzi. Ongezeko hilo limesababishwa na utendaji mzuri wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, usisitizaji katika utekelezi wa waraka No. 8 wa Hazina ambao unahitaji Sekta na mashirika ya umma kuchangia asilimia 10 ya jumla ya mapato kwa serikali uliosababisha uongezekaji wa mapato na ulipaji wa madeni ya Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa serikali.

Lengo kuu la ubinafsishaji wa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ni kuhakikisha kuwa malengo yanafikiwa kwa ufanisi mkubwa pamoja na kupunguza hasara katika mashirika. Mpaka muda wa kuandika ripoti hii, mashirika 34 ambayo yalishatengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji yalikuwa bado yapo kwenye hatua mbalimbali za ubinafsishaji. Hii inaashiria aidha ufanyaji kazi usioridhisha wa Shirika Hodhi la Mali za Umma au matatizo kwenye sehemu nyingine zinazo husika katika mchakato wa ubinafsishaji. Serikali inapaswa iamue ama kuharakisha utaratibu wa kukamilisha zoezi la ubinafsishaji kwa mashirika yaliyosalia ili kuepusha kuharibika kwa rasilimali zilizopo au ibadilishe maamuzi yake na kuyapa mashirika hayo mtaji ili yaweze kufanya kazi kwa ufanisi. Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2012 jumla ya mashirika 274 yalikuwa yamebinafsishwa. Mfano wa

mashirika yaliyobinafsishwa ni yale ya sekta ya kilimo, miundombinu, maliasili na utalii.

X Matokeo ya Kaguzi Maalum

Katika mwaka huu wa fedha nilifanya Kaguzi Maalum katika Shirika la Ugavi wa Umeme Nchini (TANESCO) na katika Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA). Matokeo ya kaguzi Maalum yameonyeshwa kwa Muhtasari hapa chini. Matokeo hayo yameelezewa katika sura ya kumi ya ripoti hii.

Ukaguzi Maalum TANESCO, uligawanyika katika awamu kuu mbili na matokeo ya ukaguzi huo kwa mhutasari ni kama ifuatavyo;

Awamu ya kwanza ya ukaguzi maalum wa TANESCO ulionyesha kuwa, Kampuni ya 'Santa Clara' ilipewa mkataba Na. PA/001/11/HQ/G/011 wa ugavi wa vifaa vya ofisini (Stationaries), vifaa vya Kompyuta na mashine za kudurufu kwa mwaka mmoja kuanzia tarehe 20 Disemba, 2011. Mkurugenzi Mkuu wa Santa Clara akiwa mke wa aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO na pia aliwahi kuwa mfanyakazi wa TANESCO kabla ya kuacha kazi. Biashara kati ya Santa Clara Supplies na TANESCO ilikuwa na utaratibu usioridhisha, Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO hakuweka hadharani mgongano wake wa kimasilahi na Kampuni hiyo, pia mke wa Mkurugenzi hakuweka hadharani mgongano wa kimasilahi aliokuwa nao na TANESCO kwenye taarifa za zabuni kama ilivyotakiwa.

McDonald Live Line Technology Limited ilipewa zabuni na TANESCO wakati ilikuwa na makubaliano ya ubia na Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO. Kampuni hiyo ilipewa mikataba ya matengenezo (repairs) ya njia za umeme hai iliyosainiwa kwa mwaka 2008, 2009, 2010 na 2011. Ilikuwa kinyume na Kanuni za maadili za TANESCO na Kanuni za Maadili za Viongozi za mwaka 1995 kwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO kuipa mikataba kampuni ya MacDonald 2008

ambayo alikuwakwenye ubia nayo, na bila kutoa taarifa ya mahusiano hayo.

Ukaguzi wa Awamu ya pili ulionyesha kuwa, TANESCO ilikiuka sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005. Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO ambaye ndiye mwenye maamuzi kwenye manunuzi ya Shirika alishindwa kuzuia ukiukwaji wa sheria za manunuzi, na aliidhinisha manunuzi kwa njia ya chanzo kimoja (single source procurement) au kufanya manunuzi kwa wakandarasi au watoaji huduma wachache (restricted procurement) bila kufuata ushindani. Manunuzi ya TANESCO mara nyingi, hayakuzingatia makadirio ya wahandisi wa Shirika hilo katika kufanya uchaguzi wa zabuni zenye bei nafuu na kwa viwango vya ubora vinavyotakiwa.

Ukaguzi Maalum wa uuzwaji wa hisa za UDA kwa mwekezaji ulibaini kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya UDA haikuzingatia taratibu za Sheria ya Manunuzi katika kuuza hisa za UDA kwa muwekezaji. Hisa za UDA zilifanyiwa makadirio ya thamani ya Shilingi 744.79 mwezi Octoba, 2009 na shiling 656.15 mwezi Novemba, 2010 kwa hisa moja. Hata hivyo, hisa hizo ziliuzwa kwa Shilingi 145 kwa hisa moja bila kuzingatia makadirio ya thamani yaliyokwisha fanyika. Pamoja na mafungu yaliyojitokeza, kiasi cha fedha kilichotakiwa kulipwa kwa bei hiyo ya punguzo ilikuwa ni Shilingi bilioni 1.1 lakini ni kiasi cha Shilingi milioni 285 tu ndizo zilizolipwa na salio lililobaki bado halijalipwa na Kampuni hiyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa UDA alipokea kiasi cha Shilingi milioni 320 kwa kile kilichoelezwa ni malipo ya kutoa huduma za ushauri (consultancy services) kwa mwekezaji, na kiasi hicho cha fedha kililipwa kwenye akaunti binafsi ya Benki ya Mwenyekiti huyo wa Bodi (personal account). Kitendo hicho kinaashiria kuwepo kwa mgongano mkubwa wa kimasilahi katika uuzaji wa hisa za UDA. Kiasi hicho cha fedha kilielezwa na mwekezaji kuwa ni malipo ya

awali ya kuonyesha nia ya kuingia kwenye makubaliano ya kununua hisa za UDA.

xi Thamani Kutokana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa sasa kwa mara ya kwanza ilitolewa mwaka 2006/2007. Kuanzia kutolewa kwake kwa mara ya kwanza, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali imeibua mapendekezo mengi ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge na Menejimenti ya mashirika ya umma. Pia mapendekezo hayo yalitolewa katika kupata ufumbuzi wa hoja zilizoainishwa. Nimekuwa nikiguswa na imani ya serikali kwa jinsi ambavyo imekuwa ikitekeleza baadhi ya mapendekezo yangu ambayo ni muhimu hali iliyopeleka kuzaa matunda kwa serikali, mashirika ya umma na nchi kwa ujumla. Baadhi ya mambo ambayo yametokana na mapendekezo yangu ni uanzishwaji wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, kurekebishwa kwa Sheria ya Msajili wa Hazina, Kuanzishwa kwa kamati ya Mahesabu ya mashirika ya umma (POAC), Mapitio ya Mkataba wa TICTS, kuongezeka kwa idadi ya mashirika ya umma yanayokaguliwa, kutoyabinafsisha baadhi ya Mashirika, kuongezeka kwa uzingatifu wa Sheria mbalimbali. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba kuna idadi ya mapendekezo kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu Wa Hesabu za Serikali ambayo hayajatekelezwa ambayo yataendelea kuripotiwa hadi hapo yatakapotekelezwa.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA

1.0 Uanzishwaji wa Kazi ya Ukaguzi wa Umma Kisheria

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ofisi ya kikatiba iliyoanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kama inavyorekebishwa. Ukaguzi wa Umma Tanzania umeelezewa zaidi kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 na sehemu ya 44 (2) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlamka ya Kisheria kukagua Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali angalau mara moja kwa kila mwaka wa fedha kama ilivyoainishwa katika ibara ya 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyorekebishwa na kama ilivyoelezwa kwenye kifungu Na. 32 cha Sheria ya Ukaguzi ya Umma Na. 11 ya mwaka 2008. Vilevile sehemu ya 33 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 inampa Mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kumruhusu mtu yeyote ambaye anaweza kuchaguliwa kuwa mkaguzi wa Shirika ama Afisa yeyote kukagua kwa niaba yake vitabu vya hesabu vya Taasisi i yeyote ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anapaswa kukagua kwa mujibu wa Sheria.

Katika kuelewa muongozo wa kisheria unaoongoza kaguzi za Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine, ni vizuri kuelewa pia Mashirika mengi yanafuata viwango vya Kimataifa vya utayarishaji wa Taarifa za Hesabu au viwango vya kimataifa vya kuandaa taarifa za Hesabu za Umma. Kwa hali hiyo, miongozo ya kisheria inayotumika kuandaa mahesabu na kaguzi ni ama sheria ya makampuni Na. 12 ya mwaka 2002 au sheria yeyote iliyopitishwa na Bunge inayohusu shirika husika.

1.1 Mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu

1.1.1 Mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ya Kuandaa Taarifa

Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kama inavyorekebishwa inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha taarifa ya mwaka ya Ukaguzi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikapo tarehe 31 Machi ya kila Mwaka. Baada ya kupokea taarifa atawaelekeza watu wanaohusika kuwasilisha taarifa hizo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge ambacho kitafanyika baada ya Rais kupokea taarifa hizo na lazima taarifa hii iwakilishwe ndani ya siku saba tangu kikao hicho cha Bunge kilipoanza. Kama Rais hatachukuwa hatua zozote za kuwasilisha taarifa hizo Bungeni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu atawasilisha nakala ya taarifa kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano (au Naibu wa Spika ikiwa kiti cha Spika kiko wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yeyote Spika hawezi kutekeleza majukumu yake) ambaye atawasilisha taarifa hiyo Bungeni. Kimsingi taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu zinazohusu Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali hujadiliwa na Kamati ya Bunge inayohusika na Mashirika ya Umma na kuandaa ripoti ambayo itawasilishwa Bungeni.

1.1.2 Mamlaka ya Ukaguzi

Sehemu ya 30 na 32 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kufanya ukaguzi wa hesabu na ukaguzi wa thamani ya fedha wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Sehemu ya 12 ya Sheria hiyo inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kutoa maoni kwa nia ya:-

- Kuzuia na kupunguza matumizi ya fedha za Umma yasiyokuwa na tija,
- Kuongeza makusanyo ya maduhuli ya Umma,
- Kuzuia hasara inayoweza kutokea kwa uzembe, wizi, kukosa uaminifu udanganyifu au rushwa kuhusiana na fedha na raslimali za Umma.

- Kuongeza Uwekevu, Tija na Ufanisi katika kutumia fedha za umma.

1.2 Wigo na Matumizi ya Viwango katika Kuandaa Hesabu

1.2.1 Wigo wa Ukaguzi

Wigo wa ukaguzi unamaanisha mwelekeo na maeneo ambayo yatakaguliwa kwa kaguzi husika. Wigo wa ukaguzi unajumuisha maeneo yatakayokaguliwa, sehemu zitakazokaguliwa, mbinu za ukaguzi, aina ya ukaguzi, kazi zitakazokaguliwa na muda utakaotumika.

Nia na madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kutimiza jukumu la kutoa maoni huru kwenye hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka 2011/2012 kama zimeandaliwa kutokana na viwango vya kimataifa vya kuandaa hesabu. Ukaguzi huu unahusiana na hesabu zilizokaguliwa kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Septemba, 2011, tarehe 31 Disemba, 2011 na tarehe 30 Juni, 2012. Pia inajumuisha mapendekezo yaliotolewa kwa taarifa za kaguzi ya miaka iliopita ambayo hayakufanyiwa kazi.

Ukaguzi unaangalia ubora wa mifumo ya kiuhasibu, ubora wa mifumo ya udhibiti wa ndani, ubora wa hesabu, taarifa za utendaji kazi na mbinu nyingine za kiukaguzi zinazoonekana ni muhimu katika kutoa maoni ya ukaguzi. Ukaguzi huu umefanywa kwa kuangalia sehemu zenye mashaka na uzito unaoweza kutoonyesha hesabu zenye usahihi. Hoja za ukaguzi zimetokana na nyaraka mbalimbali ambazo niliziomba wakati wa ukaguzi kwa kuzichambua kwa umakini.

1.2.2 Utumiaji wa Viwango vya Kimataifa

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama katika Shirikisho la Asasi Kuu za Ukaguzi Duniani (INTOSAI), (AFROSAI-E) na Jumuia nyingine za Kimataifa katika taaluma ya ukaguzi. Hivyo, tunatumia viwango vilivyotolewa na INTOSAI, Viwango vya Kimataifa

vya Ukaguzi (ISA) vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC). Hivyo, wakati wa kufanya kaguzi zetu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ina jukumu la pekee la kuhakikisha kunakuwepo na nidhamu katika matumizi, uwajibikaji na uwazi. Pia, ofisi ina jukumu la kutoa ripoti iliyo bora na kwa wakati unaofaa inayoelezea namna rasilimali za Taifa zilivyotumika.

1.3 Majukumu ya Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu

Kila Bodi ya Wakurugenzi na Watendaji wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi husika wanalo jukumu la kutayarisha na kuwasilisha hesabu. Jukumu la kuhakikisha taarifa za hesabu zinaandaliwa kwa kiwango cha kimataifa kama kuweka, kutekeleza na kudumisha mifumo thabiti ya ndani itayowezesha kuandaa mahesabu yaliyo huru yasiyo na makosa yatokanayo na udanganyifu au makosa, kupanga na kutumia sera za mahesabu, na makadirio ya mahesabu yanayoendana na mazingira halisi. Uandaaji na uwasilishaji wa hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ni jukumu la kisheria lililoainishwa kwenye Sheria zilizoanzisha Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine husika, Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002. Pia Sehemu ya 31 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Kiwango Na. 1 cha Kimataifa cha utayarishaji wa Taarifa za Hesabu na kiwango Na.1 cha Kimataifa cha Uhasibu vinaelezea aina za taarifa za fedha zinazotakiwa kutayarishwa. Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hapa nchini zinatakiwa kutayarisha hesabu zao kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vya utayarishaji wa Taarifa za Hesabu (IFRS) au viwango vya Kimataifa vya uhasibu katika sekta ya Umma (IPSAS) kulingana na hali halisi na majukumu ya Mashirika ya Umma na Taasisi husika. Hii ni kutokana na uamuzi uliofanywa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na kuungwa mkono na Serikali kuwa kuanzia Julai, 2004 Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma Tanzania yalitakiwa kutengeneza hesabu zake kwa kufuata viwango

vya Uhasibu vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu (IFRS) na ukaguzi utafuata Viwango vya Ukaguzi vya Kimataifa (ISA), na Sheria nyingine zinazotolewa mara kwa mara na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

Ripoti ya mwaka ya Mashirika ya Umma inatoa taarifa ambazo zinasaidia umma kutathmini ustawi wa mashirika na uwajibikaji wa Watendaji Wakuu katika kutumia rasilimali za taifa. Kwa hali hiyo kupata taarifa kwa wakati muafaka ni kitu muhimu. Hii ndio dhima nzima ya uwazi na uwajibikaji katika kutumia rasilimali za umma.

1.4 Mifumo ya Udhibiti ya Ndani

Mifumo ya udhibiti ya ndani ni namna ambavyo Mashirika ya Umma yanapangilia mifumo katika kuhakikisha kuwa rasilimali za Umma zinatumika ipasavyo. Udhibiti wa ndani unatumika kama chombo muhimu katika kudhibiti ubadhirifu na matumizi mabaya ya mali za umma. Kwenye taasisi yeyote lengo la udhibiti wa ndani ni kuhakikisha uaminifu katika kutoa ripoti ya mahesabu, kupata majibu kwa wakati kuhusu mafanikio ya malengo iliyojiwekea, na kuhakikisha sheria na kanuni zinatekelezwa.

Tukiongelea malipo na manunuzi mbalimbali katika Mashirika ya Umma, udhibiti wa ndani una maana ya hatua zilizochukuliwa ili kufikia malengo mbalimbali yaliyowekwa mfano, namna ya kuhakikisha malipo yanayolipwa kwa ajili ya huduma na mali za shirika ni halali.

1.5 Majukumu ya Msajili wa Hazina

Kulingana na Sheria ya Msajili wa Hazina na kifungu Na. 6 cha Sheria ya Mashirika ya Umma Na.16 ya mwaka 1992, Msajili wa Hazina ana kazi na majukumu ya kusimamia vyema uendeshaji wa shughuli za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa kushirikiana na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika husika.

1.6 Mpangilio wa Kazi ya Ukaguzi

Ripoti hii inaelekeza kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi uliofanywa katika Mashirika kwa kipindi husika. Ili kutimiza malengo ya kazi zangu kikatiba, niliamua kushirikiana na makampuni binafsi ya ukaguzi katika kufanya kazi. Katika kutekeleza wajibu huu, tulifanya kazi hizo kwa kushirikiana, au kwa kuziachia kampuni binafsi zenyewe kufanya ukaguzi chini ya usimamizi wa ofisi yangu.

Kazi za ukaguzi zilizofanywa na makampuni binafsi kwa niaba yangu ziliwasilishwa kwenye ofisi yangu ili kuhakikiwa ubora wake na kusainiwa. Katika mwaka husika, ofisi yangu ilifanya kazi kwa pamoja na kampuni binafsi za ukaguzi 51 ambazo ziliomba kufanya kazi na ofisi yangu kwa mwaka husika na ambazo zimesajiliwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) kama inavyoonyeshwa kwenye **kiambatanisho I** cha ripoti hii.

1.7 Kuwasilisha Hesabu kwa Ajili ya Ukaguzi

Kifungu 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008, kinawataka Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma kutayarisha hesabu katika kipindi cha ndani ya miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

1.8 Uteuzi wa Makampuni Binafsi ya Ukaguzi

Kifungu Na. 33(5) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008, kinampa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mamlaka ya kumruhusu mtu au kampuni yeyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Wakaguzi wa Hesabu na Wahasibu Na. 33 ya mwaka1972 (iliyorekebishwa mwaka 1995) kufanya ukaguzi kwa niaba yake na kumuwezesha kupeleka ripoti kwa wakati Bungeni. Wakaguzi watakaoteuliwa watafuata Sheria kama inavyotakiwa na hawatakuwa na mgongano wa kimaslahi katika kutekeleza wajibu wao na pia hawatatoa siri za mashirika zinayoyakagua. Wajibu wa kutoa maoni ya ukaguzi ni wa

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwenyewe. Katika mwaka husika ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma 176 ulifanyika katika mpangilio ufuatao:

Jedwali Na 1:Mgawanyo wa Kazi za Ukaguzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa Mwaka 2011/2012

Na	Maelezo	Mashirika	Asilimia
1.	Mashirika yaliyokaguliwa na Ofisi yangu	21	12
2.	Mashirika yaliyokaguliwa kwa kushirikiana na Makampuni Binasfi ya Ukaguzi	15	9
3.	Mashirika yaliyokaguliwa na kampuni binafsi kwa niaba yangu chini ya usimamizi wa Ofisi yangu	140	79
Jumla		**176**	**100**

Maelezo hayo yanaweza kuonyeshwa kwenye kielelezo kama ifuatavyo:

Kielelezo Na 1: Mgawanyo wa Kazi za Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka 2011/2012



Idadi ndogo ya Mashirika ya Umma, yaani asilimia 12% ndiyo yaliyokaguliwa na ofisi yangu. Hii ni ishara ya upungufu mkubwa wa wafanyakazi. Ofisi yangu inahitaji wafanyakazi wa kutosha na wenye ujuzi ili kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali inazokumbana nazo.

Majina ya makampuni binafsi ya ukaguzi yaliyotumiwa na ofisi yangu yameorodheshwa kwenye kiambatanisho Na.1 cha taarifa hii.

1.9 Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

Muundo wa Ofisi ya Taifa kwa upande wa Ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyininezo hautoshelezi kumfanya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutimiza majukumu yake kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 143(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyofafanuliwa zaidi katika kifungu cha 32 cha Sheria ya Ukaguzi ya Mashirika ya Umma Na 11 ya 2008. Matokeo yake kaguzi chache ndizo zinazokaguliwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na asilimia 79% ya kaguzi zinafanywa na makampuni binafsi kwa niaba yangu.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina idara ya Mashirika ya Umma inayohusika na Ukaguzi, kuandaa, kuratibu na kusimamia kaguzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinazofanywa na ofisi yenyewe, ukaguzi wa pamoja na ukaguzi wa kampuni binafsi. Kaguzi zikikamilika, wajibu wa kutoa maoni ya ukaguzi ni wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwenyewe kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 33(3) cha sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008. Idara ina upungufu wa wafanyakazi, kwa hiyo, ili kukidhi matarajio ya umma katika uwajibikaji wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma inabidi idara hii ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iimarishwe zaidi.

SURA YA PILI

AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

2.0 Utangulizi

Hati ya ukaguzi ni maoni ya mkaguzi kuhusu Hesabu zilizokaguliwa ili kumwezesha mtumiaji kujua kama Hesabu hizo zimeandaliwa kwa kufuata viwango vinavyokubalika vya uhasibu, vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu na vile vinavyotolewa na Bodi za Taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi za Kimataifa.

Kulingana na kanuni za ukaguzi, nia ya kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mkaguzi kutoa maoni ya ukaguzi yanayoeleza iwapo hesabu zinaonyesha hali halisi ya kifedha ya shirika na zimeandaliwa kwa kufuata viwango vinavyokubalika.

Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumuongezea imani mtumiaji juu ya Hesabu husika kwamba zimetengenezwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika, na kumfanya Mkaguzi kupata sababu za uhakika ya kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina makosa makubwa yanayotokana na wizi ama makosa na pia kutoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi.

Ukaguzi wa taarifa za hesabu za sekta ya Umma hapa nchini ni kwa mujibu wa matakwa ya sheria ambayo yameelezwa na Ibara ya 143 (2) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyofafanuliwa na kifungu cha 43 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 ambayo inaeleza kuwa "baada ya kupokea taarifa za hesabu kwa mujibu wa sheria, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakagua hesabu hizo ndani ya miezi tisa (9) baada ya tarehe ya mwisho ya mwaka wa hesabu husika na kutoa maoni ya ukaguzi wa kila hesabu na matokeo ya ukaguzi".

2.1 Aina za Hati za Kaguzi

2.1.1 Hati Inayoridhisha (*Unqualified Opinion)*

Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa, na vile vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika kimataifa.

2.1.2 Hati Inayoridhisha na Yenye Suala la Msisitizo (*Unqualified Opinion with Emphasis of Matters)*

Suala la msisitizo halibadilishi hati ya ukaguzi kutoka hati inayoridhisha, bali kuleta uelewa zaidi wa hali ilivyo ndani ya Taasisi iliyokaguliwa ingawa imepewa hati inayoridhisha.

2.1.3 Hati Yenye Shaka (*Qualified Opinion*)

Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapokutana na mazingira ya kutokukubaliana na menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa hesabu. Maelezo ya hati yenye shaka yanafanana sana na hati inayoridhisha lakini aya ya ufafanuzi inaongezwa ili kuelezea sababu zinazoleta shaka. Kwa hiyo, hati itaonyesha kuwa hesabu kwa ujumla zinaonyesha vizuri hali ya kifedha isipokuwa kwa kasoro zitokanazo na masuala yaliyohojiwa.

2.1.4 Hati Yenye Shaka na Suala la Msisitizo (*Qualified Opinion with Matters of Emphasis)*

Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapokutana na mazingira ya kutokukubaliana na menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa hesabu.

Aya ya suala la msisitizo inaambatanishwa wakati kunahitajika uzingatiaji wa haraka kutoka kwa Watendaji Wakuu na watumiaji wa taarifa za fedha kuwatahadharisha kuhusu masuala hayo yanayohitaji kushughulikiwa haraka. Hata hivyo, lengo kuu la suala la msisitizo ni kuleta karibu

uelewa wa hali ilivyo ndani ya Shirika au Taasisi iliyokaguliwa ingawa imepewa hati yenye shaka.

2.1.5 Hati Mbaya (*Disclaimer Opinion)*

Aina hii ya hati ni moja wapo ya sababu zinazoweza kubadilisha hati ya ukaguzi. Hati hii hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu hesabu zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri hesabu kiasi cha kushindwa kutoa maoni kuhusiana na hesabu hizo. Katika hali ambayo hati hii inatolewa ni pamoja na kukosa uhuru wa kufanya kazi ya ukaguzi ipasavyo kunapokuwa na wigo finyu wa kupata taarifa kwa ajili ya ukaguzi ama kwa kukusudia au kutokukusudia ambako kunazuia kazi ya mkaguzi kupata vielelezo vya kutosha.

2.1.6 Hati Isiyoridhisha (*Adverse Opinion*)

Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapoona kuwa, taarifa za fedha za Shirika la Umma au Taasisi nyinginezo kwa kiasi kikubwa zina makosa, na zikiangaliwa kwa ujumla wake hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uhasibu vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, na zile zinazotolewa na Taasisi Taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi za Kimataifa. Hati hii inaonekana kuwa ni kinyume cha hati inayoridhisha. Kimsingi hati hii hueleza kwamba, taarifa zilizomo katika hesabu za Shirika au Taasisi kwa kiasi kikubwa si sahihi wala za kuaminika kwa ajili ya kutathmini hali ya kifedha na matokeo ya kiutendaji ya Shirika au Taasisi husika.

2.2 Hali Halisi ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma

Ripoti hii ya Mashirika ya Umma kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 kwa ujumla itajadili ripoti 176 za Mashirika ya Umma na Taasisi Zingine. Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2012 Watendaji Wakuu wa mashirika 174 waliwasilisha hesabu zao kwenye ofisi yangu kwa ajili ya kukaguliwa. Mashirika mawili (2) ambayo ni Benki ya Azania na Usafiri Dar es Salaam hayakuwasilisha

hesabu zake. Usafiri Dar es salaam haikuwasilisha hesabu zake kwa mantiki kuwa umiliki wake haueleweki. Kwa upande mwingine Azania Bank Limited ilianzishwa kama kampuni binafsi mwaka 1995 ikiwa inajulikana kama 1st Adili Bancorp ambayo mpaka sasa umiliki wake wa umma una utata.Kwa sasa hisa za benki hiyo zinamilikiwa kwa asilimia 91% na Mifuko ya Pensheni ambayo inamilikiwa na serikali kwa asilimia 100%,hali inayopelekea umiliki wa benki hii uangukie mikononi mwa serikali.

Kaguzi 126 zilihitimishwa na kutolewa kwa mashirika husika. Kati ya hizo kaguzi zilizohitimishwa,kaguzi 95 zilitolewa na hati za ukaguzi wakati kaguzi 31 zilikuwa zinasubiri kupitishwa na bodi za wakurugenzi, kaguzi 10 zipo katika uboreshaji, kaguzi 24 zinaendelea na mashirika mawili hayakuwasilisha hesabu zake.

Kwa kifupi, taarifa hii inaonyeshwa kwenye jedwali kama ifuatavyo:

Jedwali Na 2: Kuwasilisha Hesabu

Na	Kundi la Shirika	Idadi ya Mashirika Niliyo Paswa Kukagua	Ripoti Zilizo Kamilika	Ripoti za Ukaguzi Zinazosubiri Kupitishwa Na Bodi za Wakurugenzi	Kuhakiki Ubora Wa Ukaguzi	Kaguzi Zinazoen-delea	Hesabu ambazo Hazija-wasili Shwa
1.	Taasisi za fedha, Mifuko ya pensheni na mashirika mengineyo.	47	26	11	4	5	1
2	Bodi, Mabaraza, Kamisheni na Mamlaka za Udhibiti.	49	25	9	2	9	0
3	Vyuo vya elimu ya juu, Tafiti, Mafunzo.	40	19	9	2	9	0
4.	Mashirika ya kutoa huduma.	40	25	2	2	1	1
Jumla		**176**	**95**	**31**	**10**	**24**	**2**
			126				

Hali halisi ya uwasilishaji wa hesabu na ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma kufikia tarehe 28 Februari, 2013 ni kama ilivyoonyeshwa kwenye Kiambatanisho Na. II cha taarifa hii.

2.3 Hati Zilizotolewa kwa Mashirika ya Umma

Kufikia tarehe 28 Februari, 2013 nimefanikiwa kuhitimisha kaguzi 126 (71.6%) kati ya kaguzi 176 zinazotakiwa kukakaguliwa na ofisi yangu. Katika kaguzi zilizokamilika, mashirika 95 ripoti zake zilikuwa zimeshasainiwa wakati mashirika 31 yalikuwa yanasubiri hesabu kuridhiwa na kusainiwa na Bodi za Wakurugenzi za mashirika husika. Kati ya kaguzi zilizosainiwa, kaguzi 62 (65.3%) zilipata hati inayoridhisha, kaguzi 23 (24.2%) zilipata hati zinazoridhisha zenye masuala ya msisitizo. Kaguzi 2 (2.1%) zilipata hati zenye shaka, kaguzi 7 (7.4%) zilipata hati zenye shaka zenye masuala ya msisitizo. Shirika 1 (1.%) lilipata hati mbaya na hakuna shirika lililopata hati isiyoridhisha.

Aina ya Hati zilizotolewa na Mashirika husika ni kama ilivyoonyeshwa kwenye kiambatanisho Na.III cha ripoti hii.

Jedwali Na 3: Mchanganuo wa Hati Zilizotolewa kwa Mashirika ya Umma kwa Miaka Mitatu Mfululizo

Kaguzi ya mwaka	Hati inayor-idhisha	Hati inayori-dhisha yenye msisitizo	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka na msisitizo	Hati kushindwa kutolewa (Hati mbaya)	Hati isiyori-dhisha	Mashirika
2009/2010	**92**	**12**	**10**	**7**	**1**	**0**	**122**
	75.4%	9.8%	8.2%	5.8%	0.8%	0	100%
2010/2011	**84**	**12**	**7**	**4**	**0**	**0**	**107**
	78.5%	11.3%	6.5%	3.7%	0%	0%	100%
2011/2012	**62**	**23**	**2**	**7**	**1**	**0**	**95**
	65.3%	24.2%	2.1%	7.4%	1%	0%	100%

Mchanganuo Hapo juu Unaweza Kuoneshwa Kwenye Grafu na Pai Chati kama Ifuatavyo

Kielelezo Na 2: Mchanganuo wa Hati Zilizotolewa kwa Kipindi cha Miaka Mitatu Mfululizo Kutoka 2009/2010 Hadi 2011/2012



Kielelezo Na 3: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi kwa Kila Mwaka (Miaka 3 Kuanzia 2009/10 hadi 2011/12)







SURA YA TATU

MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MIAKA ILIYOPITA

3.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha kwa muhtasari mapendekezo ya Ukaguzi wa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma za miaka iliyopita, ambayo bado hayajatekelezwa. Mapendekezo hayo yapo aidha kwenye hatua za utekelezaji au hayakutekelezwa kabisa hadi ilipofikia wakati wa kuandaa ripoti hii. Ili kuongeza uwajibikaji na utawala bora katika Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali, ni jukumu la kila shirika kuchukua hatua ya kutekeleza mapendekezo ambayo hayajatekelezwa. Hata hivyo ifahamike kuwa, maagizo hayo ambayo hayajatekelezwa yanahitaji kupewa kipaumbele siyo tu na Serikali bali pia kwa kushirikiana na Kamati ya Bunge inayohusika na hesabu za mashirika ya umma, Wakurugenzi wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinazohusika.

3.1 Majibu ya Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka Uliopita (2010/2011)

Nakiri kupokea majibu ya ripoti ya mwaka uliopita kupitia barua ya Katibu Mkuu Hazina na Mlipaji Mkuu wa Serikali yenye kumbukumbu Na. EB/AG/AUDIT/12/VOL.I/53 ya tarehe 20 Juni, 2012. Napenda kutambua juhudi zilizofanywa na Mlipaji Mkuu wa Serkali kwa majibu aliyotoa kwa mapendekezo yaliyotolewa kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ijapokuwa baadhi ya mapendekezo bado hayajatekelezwa. Kwa hali hiyo malengo na madhumuni yanayotarajiwa hayatafikiwa kama mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu hayatatekelezwa kikamilifu.

Ningependa kuifahamisha Serikali kwamba mapendekezo ninayoyatoa yana lengo la kuhakikisha uwepo wa umakini katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali, uangalizi, utoaji na matumizi mazuri ya mali za umma. Mapendekezo hayo pia yanalenga kuhakisha matumizi ya fedha za umma yanaidhinishwa na wenye madaraka na fedha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuhakikisha, tija na ufanisi katika kutumia rasilimali za Taifa kwa kuzingatia sheria.

Kwa kuzingatia misingi hiyo nimeona ni vyema kuyarudia tena mapendekezo niliyoyatoa katika ripoti zilizopita ambayo hayajatekelezwa au yametekelezwa kidogo. Ni vizuri Serikali, Kamati ya Bunge ya kusimamia mahesabu ya Mashirika ya Umma, Bodi za Wakurugenzi, Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma kufahamu kuwa bado kuna mapendekezo ambayo bado hayajatekelezwa na yanahitaji nguvu za pamoja ili kuyatekeleza.

3.2 Muhtasari wa Mapendekezo Ambayo Hayajatekelezwa Katika Mwaka wa Fedha 2007/2008:-

3.2.1 Kuongezewa Mtaji kwa Mashirika ya Umma yenye Mtaji Mdogo

Msajili wa Hazina anapaswa kuhakikisha kuwa Mashirika ambayo hayana mitaji ya kutosha, yanapatiwa fedha kwa ajili ya kuyaendesha. Hili linaweza kufanyika kwa kuanzisha vyanzo mbalimbali vya mapato ili yaweze kufanya kazi kwa ufanisi na kutoa huduma bora kwa umma.

3.2.2 Haja ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina Kuendana na Tamko la Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya.418

Endapo Ofisi ya Msajili wa Hazina haitafanya kazi kwa mujibu wa Sura ya 418 ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Serikali itapaswa kuangalia uwezekano wa kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi itakayokuwa na jukumu la kudhibiti, na kusimamia uendeshaji wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma 176 zenye hisa/mtaji ya jumla ya

Shilingi tirioni 12.2 katika kukuza uwajibikaji na uwazi katika kutoa huduma nzuri kwa Umma.

3.2.3 Kuongeza wigo wa Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma

Katika ripoti zangu za mwaka zilizopita nilimshauri Mheshimiwa Spika afikirie kupanua majukumu ya Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma na kuipa jina la Kamati ya Uwekezaji wa Umma ili iweze kuangalia na kuhoji maswala ya taarifa za fedha za Taasisi na makampuni yote ambayo Serikali ina hisa, hata kama ni chini ya asilimia 50.

Kwa kuwa Mheshimiwa Spika ameona ni vizuri mahesabu ya Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali yajadiliwe na PAC, kuna haja ya kuona umuhimu wa kuongeza wigo wa kamati na kuiongezea wajumbe na vitendea kazi ili kuweza kutekeleza majukumu makubwa ya kusimamia rasilimali za Umma.

Kwa upande mwingine napenda Mheshimiwa Spika afahamu kwamba, pia kwa kuwa Ofisi yangu imetumia kiasi kikubwa cha fedha katika kujenga uwezo wa kamati iliyokuwa inasimamia hesabu za Mashirika ya Umma kwa kuwapeleka katika mafunzo mbalimabali. Hii imesaidia kuongeza uelewa wa wajumbe wa kamati kuhusiana na Mashirika ya Umma na hesabu zake. Kwa hali hiyo napenda kumshauri Mheshimiwa Spika kuangalia umuhimu wa kubakiza baadhi ya waliokuwa wajumbe katika Kamati iliyopita kama kamati mpya itaundwa kwa ajili ya muendelezo wa majukumu waliyokuwa wameshaanza ya kamati ya PAC.

3.2.4 Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika

Kanuni za Utawala Bora zinataka Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wateuliwe na Bodi za Wakurugenzi badala ya kuteuliwa na Rais. Ili kumpunguzia mzigo mheshimiwa Rais, ninashauri Rais angeachiwa jukumu la kuteua wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi wakati uteuzi wa Maafisa Watendaji, Wakuu wa Mashirika na Taasisi

Nyinginezo za Umma lingekuwa ni jukumu la Bodi za Wakurugenzi ili Bodi za Wakurugenzi ziweze kuziwajibisha menejimenti za Mashirika pale ambapo viongozi hao watashindwa kuwajibika ipasavyo.

3.2.5 Uwekezaji DAWASCO

Menejimenti ya Shirika la Maji Dar es Salaam (DAWASCO) inapaswa iharakishe uwekezaji wake kwa kuwekeza kwenye uchimbaji wa maji ardhini ili yatumike kwa eneo kubwa la Jiji la Dar es Salaam ambalo halina maji ya kutosha. Pia, Shirika lipitie upya viwango vya ankara za maji ili kuiwezesha DAWASCO kulipa gharama zake za uendeshaji.

3.3 Ufuatao ni Muhtasari wa Mapendekezo ya Mwaka 2008/2009 Ambayo Bado Hayajatekelezwa:-

3.3.1 Mgongano wa Kimaslahi kwa Wabunge Kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Bunge ndicho chombo kikuu kinachowakilisha wananchi na chenye majukumu ya kutathmini utendaji kazi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kupitia Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo basi, ni kinyume na matakwa ya kanuni za utawala bora kwa Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma. Katika mkutano wa Uwajibikaji uliofanyika tarehe 23 hadi tarehe 24 Januari, 2009 iliamuliwa kuwa Wabunge wasiteuliwe kuwa wajumbe katika Bodi za Mashirika ya Umma. Ili kuondoa mgongano wa kimaslahi, Wabunge hawapaswi kuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Mwenendo huu ni wa kipekee na upo tu Tanzania na hautumiki mahali popote katika Jumuiya ambayo Tanzania ni mwanachama, kwa mfano EAC, SADCOPAC, SADC, AFROSAI-E, AU na hautumiki katika nchi yoyote duniani.

3.3.2 Mikataba ya Uwajibikaji wa Bodi za Wakurugenzi

Serikali inapaswa kuingia mikataba ya utendaji na Wakurugenzi wa Bodi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Wakurugenzi hao wanapaswa kuwajibika kwa Serikali kwa matokeo ya utendaji kazi wao. Vilevile Wakurugenzi wa Bodi hizo wanatakiwa kuingia mikataba na Watendaji Wakuu ambao nao wataingia mikataba na wafanyakazi waliopo chini yao katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo. Kwa kufanya hivyo ni dhahiri kuwa itaboresha uwajibikaji na utendaji kazi katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

Mlipaji Mkuu wa serikali amejibu mapendekezo haya kwa kutoa maelekezo kwenye waraka wa Msajili wa Hazina Na 1 ya mwaka 2012 wenye Kumb Na. TYC/T/200/566/29 wa tarehe 5 Januari, 2012. Hata hivyo waraka huo haujaanza kufanyiwa kazi. Ni vizuri Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma wanasaini mkataba wa utendaji na zile bodi ambazo hazitasaini zichukuliwe hatua za kinidhamu.

3.3.3 Haja ya Kuanzishwa Mfuko wa Umma wa Uwekezaji

Ni dhahiri kwamba Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zimegubikwa na matatizo mengi, kubwa ikiwa ni ukosefu wa mitaji ya kutosha ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Serikali inapaswa kuanzisha Mfuko wa Umma wa Uwekezaji ili kuweza kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazokabiliana na uwekezaji wa serikali kwenye taasisi mbali mbali. Gawio na misaada ya wahisani inayopatikana katika nyanja hii zinaweza kuwekwa katika mfuko huu. Fedha hizo hazipaswi kutumiwa katika shughuli za matumizi ya kawaida bali zinaweza kutumika kwenye miradi ya maendeleo kama vile miradi mipya, kuongeza mitaji na kutoa mikopo nafuu kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinazohitaji.

3.3.4 Kuchelewa Kuteua Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali

Ijapokuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali amekiri kutuma waraka kwa Wizara Mama za Mashirika husika kuwataka waweze kuchagua Bodi mpya za Wakugenzi mara Bodi iliyopo inapomaliza muda wake,tatizo hili bado linaendelea. Napenda kusisitiza kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kuendelea kuwasisitiza Mamlaka husika kuhakikisha Bodi za Wakurugenzi zinateuliwa mapema pale muda wa Bodi unapokwisha kutokana na ukweli kwamba, kuna madhara makubwa yanayotokana na kuchelewa kuteua Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Madhara hayo ni pamoja na kuchelewa kufanya maamuzi ya kiutendaji, kutoweza kupitisha mahesabu na kutoweza kupitisha bajeti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo.

3.3.5 Kutokuwepo kwa Usawa Katika Marupurupu Yatolewayo na Mashirika ya Umma

Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wanafanya kazi zinazofanana katika Mashirika wanayosimamia. Kwa maana hiyo kuna haja ya Serikali kuhakikisha kuwa kuna uwiano katika marupurupu wanayopata Menejimenti na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma, na Taasisi Nyinginezo, kutokana na ukweli kwamba rasilimali wanazotumia ni rasilimali za Umma. Ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma katika kutumia rasilimali za Taifa ni vyema kuondoa tofauti zilizopo katika marupurupu hayo.

3.3.6 Malipo ya Nyongeza ya Mishahara - TRL

Kiasi kilichotakiwa kudaiwa na TRL na kulipwa na Serikali kama nyongeza ya mishahara kwa kipindi cha mwezi Machi hadi Julai 2008 kingelikuwa sahihi kama kingekuwa Shilingi bilioni 1.4 na siyo Shilingi bilioni 9.8 zilizodaiwa. Kwa hiyo, TRL ilidai zaidi Shilingi bilioni 8.4 kutoka Serikalini. Jibu la Mlipaji Mkuu wa Serikali haliridhishi kujibu mapungufu yaliyojitokeza kwa kulipa malipo ya ziada bali limejaribu kurekebisha kipindi cha ulipaji malipo yalipofanyika badala

ya kueleza hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kwa menejimenti ya TRL.

3.3.7 Ada ya Makubaliano ya Maridhiano Kati ya Serikali na TRL Isiyolipwa Shilingi Bilioni 16.1

Serikali inapaswa kufanya tathmini ya ubia wake na kampuni ya RITES, na Serikali ihakikishe kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 16.1 kinalipwa.

Kutokana na jibu la Mlipaji Mkuu wa Serikali, Serikali imeshajitoa ubia na kampuni ya RITES na hatima ya kiasi cha Sh. 16.1 bilioni ambacho hakijalipwa kinasubiri maamuzi ya Baraza la Mawaziri.

3.3.8 Mkopo wa PSPF Shilingi Bilioni 58 kwa Bodi ya Mikopo na Marejesho ya Mikopo ya Wanafunzi Shilingi Bilioni 51.1

Serikali kuingilia maamuzi katika mifuko ya Pensheni ndio chanzo cha matatizo ya kifedha katika Mifuko hii. Mikopo ambayo Serikali imedhamini Taasisi za Serikali kutoka Mifuko ya Jamii inachukua muda mrefu kulipwa. Ningependa kusisitiza kuwa serikali inapaswa ichukue hatua kuhakikisha kwamba bakaa ya deni lote la mkopo (ikiwa ni kiasi cha mkopo na riba) uliokopwa kutoka PSPF unalipwa, ili kuepuka gharama zaidi za riba na adhabu itokanayo na kuchelewa kulipa mkopo huo. Bodi ya Mikopo inapaswa kuanza kutekeleza hatua za kisheria kwa waajiri na wakopaji binafsi ambao hawatoi ushirikiano kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 19A-23 ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya mwaka 2004 na kuhakikisha Mfuko unarudishiwa hela za wanachama zilizokopwa.

3.4 Katika ripoti ya mwaka 2009/2010, nilitoa mapendekezo mengi ambayo hayajatekelezwa, na Serikali haikutoa majibu yanayopelekea kufanyia kazi mapendekezo hayo ambayo yanatolewa kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

3.4.1 Ucheleweshwaji wa Fedha za Bajeti Kutoka Hazina

Ili kupunguza migogoro ya Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu, ambayo inaathiri elimu ya wanafunzi katika vyuo hivyo na maendeleo ya Taifa, Hazina inapaswa kutafuta njia na mikakati madhubuti ya kuhakikisha fedha za mikopo ya wanafunzi zinapelekwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya juu kwa wakati bila kuchelewa.

3.4.2 Kupima Utendaji Kazi wa Mashirika Yaliyopo na Yaliyobinafsishwa

Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa madeni ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo marejesho yake yalikuwa yameiva lakini yalikuwa hayajarejeshwa, yanarejeshwa ili kuepuka Serikali kulipa mikopo hiyo na bakaa ya mapato ya kipindi cha nyuma yanayokusanywa bila kuchelewa.

Shirika Hodhi la Mali za Serikali zilizobinafsishwa (CHC) linapaswa kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kuwa Mashirika yaliyobinafsishwa yanajiendesha kulingana na makubaliano ya mikataba ya mauzo, na kuchukua hatua madhubuti kwa kampuni zote zinazojiendesha bila kuzingatia makubaliano ya mikataba ya mauzo.

3.4.3 Kanuni za Mgawanyo wa Kazi Katika Utendaji wa Mashirika ya Umma

Serikali, Bunge na Mahakama zinapaswa kusimamia suala la mgawanyo wa kazi na majukumu katika utendaji wa Serikali na taasisi zake. Kumekuwa na muingiliano wa kimaslahi katika utendaji kazi wa kila siku kati ya Bodi ya Wakurugenzi na Wabunge katika kutoa maelekezo na maagizo yasiyo na mipaka kwa menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Pia, juhudi zaidi zinahitajika kuhakikisha kuwa kanuni za utawala bora katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo zinaelekezwa hadi ngazi za chini za utendaji.

3.4.4 Bodi za Wakurugenzi Kuingilia Kazi za Menejimenti

Masuala ya kiutendaji ya shirika yanatakiwa kutekelezwa na menejimenti ya shirika husika. Bodi za Wakurugenzi zinapaswa kutathmini utendaji wa menejimenti katika kufikia mpango kazi wa mwaka na mpango mkakati wa shirika. Bodi za Wakurugenzi zinatakiwa zipate mafunzo kuhusu majukumu na wajibu wao na kuwe na mkataba unaolezea wajibu na majukumu yao.

Majibu ya Mlipaji Mkuu yaliyotolewa kupitia waraka Na TYC/T/200/583 wa tarehe 28 Julai, 2004 hayakutoa ufumbuzi wa swala hili. Serikali inashauriwa kutafuta jinsi ya kutatua tatizo hilo au hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa Bodi ya Wakurugenzi wanaoingilia watendaji wakuu wa Mashirika katika kazi zao za kiutendaji za kila siku.

3.4 5 Kutofuata Waraka wa Msajili wa Hazina (Waraka Na.8)

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinapaswa kuhakikisha kuwa zinafuata maagizo yanayotolewa na Serikali na pia kutoa michango yao kwa Hazina kama waraka ulivyoeleza. Pale ambapo Mamlaka haziwezi kutimiza maagizo ya serikali, basi zitoe taarifa kwa mamlaka husika ili kupata idhini ya kufanya vinginevyo. Msajili wa Hazina anapaswa kuonyesha kuwa, ndiye mmiliki wa Mashirika na aanzishe sera za kudumu za kuwa mmiliki. Zaidi ya hayo, Msajili ahakikishe utawala wa Mashirika ya Umma unakuwa wa uwazi na endelevu na wa ufanisi. Inategemewa kuwa Msajili wa Hazina ataanzisha sera ya umiliki ambayo itaainisha malengo ya Msajili wa Hazina na majukumu ya utawala bora kwenye Mashirika ya Umma na namna ya utekelezaji wa sera hiyo.

3.4.6 Mashirika Yaliyotengwa kwa Ajili ya Kubinafsishwa

Serikali inapaswa kuangalia upya ubinafsishwaji wa mashirika 34 yaliyotengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji yaliyotoka PSRC na kuchukuliwa na CHC ili kuepuka uharibifu na uchakavu wa rasilimali zinazomilikiwa na

mashirika haya au Serikali kutoyabinafsisha na kuyaongezea mitaji ili yaanze kazi upya.

3.5 Katika Ripoti Yangu ya Mwaka ya 2010/2011 nilitoa Mapendekezo Mengi Ambapo Mengi Bado Hajatekelezwa kama ifuatavyo;

3.5.1 Usimamizi wa Rasilimali

Katika ukaguzi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) nilibaini kwamba mfuko ulitumia Shilingi bilioni 234.1 kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), chini ya makubaliano ya buni, jenga, miliki na hamisha miliki baada ya miaka kumi (10). Mifuko mingine iliyochangia ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa makubaliano hayo hayo ni Mfuko wa Pensheni kwa wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF), Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mtaa (LAPF), Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma (PPF) ambayo yalichangia jumla ya Shilingi bilioni 181.3.
Majengo haya hayako kwenye vitabu vya Chuo Kikuu cha Dodoma wala katika vitabu vya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hii inatokana na uelewa tofauti uliopo kati ya pande mbili zinazohusika. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inafahamu kwamba kiasi cha fedha kilichotumika kujenga majengo hayo kilikuwa ni mikopo kwa Serikali wakati Serikali inafahamu kwamba kilikuwa ni uwekezaji wa mifuko hiyo.

Mikopo mingine isiyolipika yenye udhamini wa Serikali ni ya jumla ya Shilingi bilioni 91.7 na dola za Kimarekani milioni 9.65 ikiwa ni mikopo ya ujenzi wa ukumbi wa Bunge Dodoma, Nyumba za Polisi, Jengo la Machinga, Kiwanda cha Matairi cha Arusha ambapo makampuni binafsi ambayo mikopo yake hailipiki kwa mujibu wa makubaliano ni Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira, Kiwanda cha Saruji Dar es Salaam, Continental Venture Ltd, Kiwanda cha Sukari Kagera na Medtch Industrial Co.Ltd yote yakiwa na udhamini wa Serikali.

Kutolipika kwa mikopo hii iliyodhaminiwa na Serikali kunaiweka mifuko hii ya hifadhi katika hatari ya kupoteza fedha za wanachama na kuhatarisha uwezo wa mifuko kufanya uwekezaji zaidi.

Zaidi ya hayo, nimebaini kwamba kutokurejeshwa kwa mikopo hii kwenye Mifuko ya Hifadhi na Serikali kutolipa dhamana iliyoweka kwenye mikopo hii ni kinyume na Sheria ya Udhamini ya mwaka 1974.

Serikali, Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na taasisi za Serikali wanatakiwa kuhakikisha kwamba hatua madhubuti zinachukuliwa ili kuhakikisha madeni yaliyokaa kwa muda mrefu yanaweza kukusanywa na vile vile kuweza kusimamia fedha pamoja na mali za mashirika haya. Kuna haja ya kuwa makini kwenye maeneo ya kuwekeza na kuangalia uwezekano wa kuwekeza kwenye vitega uchumi tofauti kwa kuzingatia uchambuzi madhubuti wa vihatarishi katika eneo hilo la uwekezaji.

3.5.2 Usimamizi wa Rasilimali Watu

Kuhusiana na upungufu wa wafanyakazi, hasa nafasi za uongozi, tunashauri kwamba nafasi zote zilizo wazi kama ilivyo katika muundo wa uongozi na zile zinazokaimiwa zijazwe. Pia, mashirika yahakikishe kuwepo kwa mpango mzuri wa kukasimisha madaraka.

Menejimenti za Mashirika ya Umma zichukue hatua zinazofaa kwa lengo la kupitia upya mishahara na marupurupu ya wafanyakazi ili yaendane na masharti ya ajira ya mamlaka husika pamoja na maelekezo ya Serikali. Mashirika ya umma yahakikishe kuwa mishahara inalipwa kwa wakati. Usimamizi mzuri katika suala la ulipaji mishahara utawapa motisha wafanyakazi kuendelea kufanya kazi kwa muda mrefu na itasaidia kupunguza idadi ya wafanyakazi wanaoacha kazi na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

3.5.3 Bodi za Wakurugenzi

Bodi za wakurugenzi za Mashirika ya Umma zihakikishe zinafuata sheria zilizoanzisha mashirika ya umma kuhusu suala la idadi inayotakiwa ya wajumbe wa bodi. Inashauriwa kwamba shughuli za kiutendaji za shirika zitekelezwe na menejimenti na bodi iachwe kushughulikia upimaji wa utendaji kazi wa menejimenti kufikia mpango kazi wa mwaka na mpango mkakati wa shirika.

3.5.4 Haja ya Kuwa na Taarifa za Msingi (Database) kwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma

Kwa kuzingatia ukweli kwamba Bodi za Wakurugenzi humaliza muda wake kwa nyakati tofauti, inakuwa vigumu kwa mamlaka za uteuzi kufuatilia kwa urahisi. Hivyo basi, ni maoni yangu kuwa Msajili wa Hazina anapaswa atengeneze kumbukumbu "database" ya bodi zote za wakurugenzi ambayo itakuwa imeandaliwa ili kutoa ishara ya kumalizika kwa muda wa bodi ya wakurugenzi na kuiwezesha mamlaka ya uteuzi kupata taarifa mapema kwa ajili ya uteuzi wa bodi mpya.

3.5.5 Maswala ya Ubinafsishaji

Serikali inatakiwa kuharakisha suala la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ambayo yapo kwenye ufilisi ili fedha zitakazopatikana zitumike kulipa madeni ili fedha hizo zisaidie Serikali kulipa mikopo iliyoidhamini na kusaidia kulinda mali za mashirika.

3.5.6 Uhakika wa Vyanzo vya Fedha za Uwekezaji

Tanzania ikiwa ni nchi inayoendelea, inatakiwa kuwa na mpango wa namna ya kuwa na fedha za kuwekeza kwa masharti nafuu. Kuna haja ya Serikali kupitisha sheria ya kuyataka Mashirika muhimu kuwekeza kwenye soko la hisa la Dar es Salaam mfano kampuni za madini, kampuni za simu, kampuni za saruji na kampuni za vinywaji.

SURA YA NNE

MASUALA MUHIMU AMBAYO HAYAKUTOLEWA TAARIFA KATIKA RIPOTI YA MWAKA ULIOTANGULIA

4.0 Utangulizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ni wajibu wa kila Shirika la Umma kuwasilisha hesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kufunga mwaka wa fedha. Kwa vile kumekuwa na kiasi kikubwa cha kutokuzingatia kwa matakwa haya ya sheria katika baadhi ya Mashirika ya Umma, ukaguzi katika baadhi ya Mashirika ya Umma umekuwa unachelewa kuanza na hivyo kusababisha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kushindwa kuripoti kuhusu kaguzi hizo katika mwaka husika. Ni muhimu ikaeleweka kuwa Mashirika ya Umma ambayo kaguzi zake zitashindwa kukamilika katika kipindi kinachotakiwa na hivyo kutoripotiwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka husika, kaguzi hizo zitaripotiwa katika mwaka unaofuata.

Hadi kufikia kipindi cha kuandaa ripoti ya mwaka jana iliyowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais mwishoni mwa mwezi Machi, 2012, ni kaguzi za mashirika 126 tu zilikuwa zimekamilika na kuingizwa katika ripoti na kaguzi za Mashirika yaliyobaki yapatayo 31 hazikuwa zimekamilika kutokana na masuala mbalimbali ikiwemo kuchelewa kuwasilisha hesabu, kutokuwepo kwa Bodi za Wakurugenzi baada ya zile za awali kumaliza muda wake, menejimenti za mashirika husika kushindwa kujibu kwa wakati hoja za ukaguzi na masuala mengine.

Kutokana na hali hiyo, sura hii inaelezea kwa kifupi masuala muhimu ambayo yapo katika ripoti za baadhi ya mashirika zilizokuwa hazikukamilika mwaka jana na hivyo kutoingia katika ripoti ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2009 iliyotolewa tarehe 26 Machi, 2010.

4.1 Upungufu wa Nyumba Tanzania

Mahitaji ya nyumba Tanzania yanakadriwa kukua kwa kasi na hivyo kuhitaji uwekezaji mkubwa wa ujenzi wa nyumba kwa ajili ya jamii. Upungufu wa nyumba Tanzania unakadiriwa kufikia nyumba milioni tatu (3) na upungufu huu utakuwa kwa kiasi cha nyumba laki mbili (200,000) kwa mwaka. Upungufu huu unatokana na ukuaji mkubwa wa mahitaji ya nyumba kwa mwaka, na ukuaji mkubwa wa idadi ya watu mijini, kitu kinachotoa fursa ya ukuaji mkubwa wa uchumi kutokana na soko la nyumba. Tatizo la ukosefu wa nyumba liko zaidi mijini, kutokana na takwimu, idadi ya watu mijini imekua kwa asilimia 14.8% mwaka 1980 na kuongezeka hadi asilimia 37.5% mwaka 2005 na inatarajiwa kufikia asilimia 46.8% ifikapo mwaka 2015. Uongezekaji wa nyumba za kupanga na za kuuza si mkubwa sana kiasi kwamba hautoshelezi mahitaji ya nyumba. Uchangiaji wa sekta ya nyumba kwenye pato la ndani la Taifa ni mdogo sana. Pia mchango wa sekta ya nyumba kwenye pato la ndani la nchi zilizoendelea ni kati ya asilimia 50% hadi 60% kwa mwaka. Nchi hizo ni pamoja Uingereza na Marekani zenye asilimia 50% na 60% kila moja. Kwa Nchi za Asia, ni kati ya asilimia 7% na 31%, Malaysia (31%), China (15%) na India (7%). Kwa Tanzania, Sekta ya Nyumba huchangia chini ya asilimia moja (1%) katika pato la taifa kwa mwaka.

Pamoja na kwamba Serikali imefanya juhudi mbali mbali ili kupunguza upungufu wa nyumba kwa kutunga na kubadilisha sheria mbali mbali kwa ajili ya kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya ushirikishwaji wa sekta binafsi, bado sekta ya nyumba haifanyi vizuri.

4.2 Usuluhishi wa Taarifa za Madawa Kati ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (MoHSW) na Bohari ya Madawa Tanzania (MSD)

Bohari ya Madawa (MSD) ni Idara inayojitegemea chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kazi yake kubwa ni kununua, kutunza na kusambaza madawa na vifaa vya

hospitali vyenye viwango vizuri kwa bei ya chini. Madawa haya yanasambazwa kupitia kwa mawakala walioidhinishwa na Serilkali kwenye nchi nzima. Kazi kubwa za Idara hii ni kununua, kutunza na kusambaza vifaa vya hospitali vyenye viwango vizuri nchi nzima. Idara hii inafanya kazi zingine za dharura zinazohusiana na kazi zao.

Ili kutekeleza majukumu yake, bohari ya Madawa inahitaji mtiririko mzuri wa fedha, toka wizara ya Afya kwenda Bohari ya Madawa baada ya fedha hizo kuombwa kutoka Wizara ya Fedha. Baada ya kupokea fedha hizo, Wizara ya Afya huzituma kwenda Bohari ya Madawa. Ucheleweshwaji wa fedha toka wizara ya Afya kwenda Bohari ya Madawa upatikanaji wa madawa kwenye ghala la MSD, hivyo kusababisha kukosekana kwa madawa na vifaa vya hospitali nchini kwa wakati.

Mbali na hayo, kuna vizuizi vingine vinavyorudisha nyuma usambaaji wa madawa, vizuizi hivyo ni pamoja na; ufuatiliaji wa madeni usioridhisha unaosababisha baadhi ya wadaiwa kutolipa hata kwa miezi 12 na wengine mpaka miezi 48. Hali ni mbaya zaidi kwenye deni la Wizara ya Afya. Ulipaji wa deni hili hauridhishi kabisa. Deni limekuwa likipanda kwa kasi kutoka Shilingi milioni 579 mwaka 2005/06 mpaka Shilingi 30.996 bilioni mwaka 2010/2011. Angalia kielelezo hapa chini.

Kielelezo Na. 4 Ongezeko la Deni la Wizara ya Afya Wanalodaiwa na MSD



Pamoja na ugumu ambao MSD inaupata katika kukusanya fedha toka Wizarani, Idara pia hutoa huduma za kusafirisha vifaa na madawa kwa ajili ya Wizara ya Afya. Kwa mfano, Wizara hutuma fedha kwenda Bohari ya Madawa kwa ajili ya kuinunulia dawa Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili lakini kuna ugumu wa usuluhishi wa takwimu. Vitabu vya Bohari ya Madawa vinaonyesha kwamba kiasi kinachodaiwa toka Taasisi ya Mifupa ni totauti na kiasi kinachoonyeshwa kwamba kilitumwa na wizara na kiasi kilichotumwa na MSD kwenda MOI. Hata hivyo, Wizara ya Afya haitoi taarifa sahihi ya kiasi cha fedha kilichotumwa kwenda MSD Kwa ajili ya MOI. MOI wanapata taarifa kutoka MSD. Kuna hatari kwamba, kiasi ambacho MSD inadai huenda kikawa sio sahihi kwa sababu MSD hawawezi kuonyesha kiasi sahihi cha fedha zilitoka Wizara ya Afya kwa ajili ya kununulia madawa ya MOI.

Wakati MSD ikiwa inashindwa kusuluhisha taarifa mbali mbali za fedha kati yake na wadau wake wengine, ufanisi wake vile vile unarudishwa nyuma na mambo mbali mbali

yakiwa ni pamoja na; uwezo mdogo wa ORION (Mfumo wa Kompyuta wa uhasibu unaotumiwa na Bohari ya Madawa) kutoa takwimu za manunuzi kwa mwaka mzima na kwa kutenganisha aina mbalimbali za madawa yaliyo nunuliwa na mauzo yaliyofanyika, ikiwa ni pamoja yale yanayonunuliwa na kusambazwa na bohari ya madawa kwa niaba ya Wizara ya Afya. Vile vile haiwezi kutoa takwimu za jumla za manunuzi kutokana na mipango mbali mbali ya mauzo, kutoweza kuchukua tarakimu zinazotokana na manunuzi kutoka kwenye mfumo huu wa uhasibu wa kompyuta. Hali hii inasababisha ugumu wakati wa uhakiki wa uhalali wa manunuzi yaliyofanyika kwani takwimu muhimu haziwezi kufuatiliwa kwa kufanya ulinganifu na vielelezo vingine kama vielelezo vya kupokelea Madawa kwa bidhaa nyingine za hospitali.

Vile vile muda unaotumiwa kwa ajili ya kutoa Madawa na bidhaa zingine Bandarini na Uwanja wa Ndege ni mrefu sana. Kwa wastani muda unaotumiwa na Idara kwa ajili ya kutoa bidhaa uwanja wa ndege ni siku 9 na bandarini ni siku 24. Lakini idara hutumia siku 14 tangu meli inapotia nanga bandarini na siku 5 uwanja wa ndege. Ucheleweshaji huu unaongeza gharama za utunzaji na faini bandarini au uwanja wa ndege. Siku zinazotumika kwa kanda mbalimbali kupata Madawa toka makao makuu ya bohari tangu kuagizwa huchukua siku 24 ukilinganisha na siku 14 zilizopangwa. Kwa sababu ya ugumu wa kupata fedha toka wizara ya Afya, Bohari ya Madawa inapata ugumu wa kupanga manunuzi na hivyo basi kupelekea kutokuwepo na Madawa ya kutosha nchini.

4.3 Muundo wa VETA, Mifumo na Michakato Isiyo Mizuri

VETA ina ofisi kwenye kanda zipatazo tisa (9) nchi nzima, na vituo vipatavyo ishirini na moja (21). Hivyo basi, wafanyakazi wake wamesambaa kwenye vituo vyote hivyo na kanda hizo ambazo zimesambaa nchi nzima. Kwa maana hiyo, muundo wake ni lazima uwezeshe kuwa na viwango thabiti na ambao una mtiririko mzuri wa maamuzi toka ofisi

kuu kwenda kwenye kanda na vituo husika. Kwa miaka kadhaa, VETA imekuwa ikikua kwa kasi, lakini muundo wake haukuwahi kupitiwa ili uweze kukidhi hali halisi iliyofikiwa na ukuaji wa wakala.

Pamoja na hayo, mfumo wa Kompyuta wa hesabu wa VETA, hauunganishi kanda na vituo vingine na makao makuu, hivyo hausaidii kutoa msingi mzuri ambao unaweza kutumika kwa ajili ya usimamizi na kufanya maamuzi kwa ajili ya nchi nzima.

Kwa kuwa vituo na waajiriwa vinaongezeka pia muundo, mifumo na nafasi katika mamlaka vinatakiwa kupitiwa upya na unahitaji kuonyesha sura na vipaumbele vya mamlaka. Muundo mzuri wenye miongozo mizuri ya Utumishi kwa kila nafasi ya kazi na kanuni za utumishi zenye uwiano na mantiki nzuri vinahitajika kwa ajili ya utendaji kazi mzuri wa watumishi wa Mamlaka.
Kukosekana kwa miundo mizuri ya mamlaka na kutopitia mpangilio wa idara vinaweza kurudisha nyuma utendaji wa mamlaka.

4.4 Kutotengwa kwa Madeni Chechefu ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iliripoti kiasi cha Shilingi bilioni 793.4 kikiwa ni kiasi cha deni kinachodaiwa toka kwa wanafunzi waliokopeshwa kwa ajili ya masomo ya elimu ya juu. Kiasi hiki kinajumuisha kiasi chote kilichokopeshwa kwa wanafunzi tangu mwaka 1994. Kiwango cha uhasibu cha Kimataifa Na. 36 kinataka shirika kukadiria kiasi ambacho rasilimali za shirika zimepungua thamani yake. Rasilimali zote za kifedha ukiachia zile zote zinazopimwa thamani halisi kwa kutumia faida na hasara, zinatakiwa kupimwa mara kwa mara ili kujua kama zimepungua thamani yake. Hivyo basi, pale ambapo kuna ushahidi wa kutosha kwamba rasilimali hizo zimepungua thamami yake, thamani

iliyopungua hukokotolewa na kuwekwa kwenye taarifa za hesabu za mapato.

Baada ya kupitia taarifa mbali mbali iligundulika kuwa, kuna baadhi ya wadeni ambao wana hali mbaya kifedha na madeni yao hayalipiki na wadaiwa wamesambaa nchi nzima. Kutokana na ushahidi huu napendekeza ufanyike uhakiki wa madeni ili madeni chechefu yaombewe kibali na kuondolewa kwenye vitabu vya bodi ya mikopo.

4.5 Udhibiti wa Ndani wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ni Dhaifu

Baada ya kupitia ripoti za ukaguzi wa ndani iligundulika kwamba baadhi ya taratibu na kanuni za uendeshaji wa Bodi hazifuatwi. Ilibainika kwamba kiasi cha Shilingi milioni 317.8 zililipwa ikiwa ni madeni kwa wakopaji mbalimbali bila kuwepo kwa taratibu maalum. Baadhi ya taarifa muhimu hazikupitiwa kabla ya kuidhinisha malipo na malipo, vilevile hayakuwa yamepata kibali cha maofisa wa juu.

Mtumishi wa Bodi ya Mikopo makao makuu alikuwa akituhumiwa kwa wizi wa fedha za Bodi kiasi cha Shilingi milioni 90.7. Vile vile kulikuwa na wizi wa fedha uliofanyika wakati wa kupeleka fedha za wanafunzi wa Chuo kikuu cha Mkwawa zipatazo Shilingi milioni 66.1.

Pamoja na hayo, Bodi ya Mikopo imekuwa ikitoa mikopo kwa wanafunzi mbali mbali bila kuangalia vielelezo muhimu vya mikopo hiyo. Kwa mfano, Bodi ilitoa fedha kwa ajili ya mkopo wa Utafiti kwa wanafunzi wa mwaka wa tatu wa Chuo Kikuu Mkwawa kiasi cha Shilingi milioni 15.5.

Vile vile iligundulika kwamba, mfumo wa kompyuta wa kusimamaia mikopo haukutengenezwa kwa namna ya kuruhusu kazi mbalimbali kufanywa na watu tofauti (segregation of duties). Kazi ya uhakiki wa taarifa za mkopaji na makadirio ya mkopo atakaopewa mkopaji

zinafanywa na mtu mmoja. Kazi nyingine kwenye mfumo huu hufanywa na mtu yeyote mwenye namba ya siri. Pamoja na hayo, hakuna sera inayotoa mwongozo ili kusaidia namna ya kutenganisha takwimu mbali mbali kitu ambacho kingesaidia katika swala zima la mgawanyo wa majukumu.

Mfumo wa kompyuta wa ALMS unatumika katika kugawa mikopo ya wanafunzi pekee wakati kazi nyingine kama vile ulipaji na urejeshaji wa mikopo haufanywi kwenye mfumo huo. Wengi wa watumiaji huamua kutumia mifumo mingine kama vile "Microsoft Excel" kwa kulipa na urejeshwaji wa mikopo. Hata hivyo, waandaji wa mikopo wa wanafunzi wa stashahada ya kwanza hufanyika kupitia mifumo ya OLAS na ALSM wakati ambapo waandaaji wa mikopo ya wanafunzi wa masomo ya stashahada ya pili hupitia mfumo wa ALSM peke yake. Uandaaji wa taarifa za mikopo ya wanafunzi stashahada ya pili hutunzwa kwenye mafaili ya "Excel".

SURA YA TANO

USIMAMIZI WA SHERIA YA MANUNUZI NA MIKATABA

5.0 Utangulizi

Tanzania imefanya mabadiliko makubwa ya sheria ya manunuzi na kupelekea kuanzishwa kwa sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Ili kuhakikisha manunuzi yanafuata taratibu katika Tanzania, kifungu Na. 44 (2) cha sheria ya manunuzi kinamtaka mkaguzi wa Taasisi yeyote ya umma kuainisha katika ripoti yake ya mwaka kama taratibu zote za manunuzi zimefuatwa katika Taasisi husika.

Vilevile, kanuni ya 31 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma (Bidhaa, Ujenzi, Huduma zisizo za kiushauri na uuzaji wa mali za Umma kwa zabuni), inamtaka Mkaguzi wa Hesabu wa Taasisi ya Umma kuainisha katika ripoti yake ya mwaka kama manunuzi yaliyofanyika yalifuata taratibu za Zabuni na yaliidhinishwa kwa mujibu wa sheria ya manunuzi.

Kwa kuzingatia mamlaka niliyopewa katika vifungu vya sheria vilivyoainishwa hapo juu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu imekagua taratibu za manunuzi katika mashirika 126 katika ukaguzi wake wa kawaida kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Hivyo, sura hii inajumuisha matokeo na mapendekezo ya kaguzi zilizofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi husika. Pia Mamlaka ya Udhibiti wa manunuzi (PPRA) ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa hoja za ukaguzi wa manunuzi uliofanyika katika Mashirika 51 ambayo matokeo yake yamejumuishwa kwenye kurasa za sura hii.

Pia sura hii, inatoa majumuisho ya taarifa za ukaguzi na utekelezaji wa mikataba iliyoonekana muhimu kutolewa taarifa katika mwaka husika. Ukaguzi wa mikataba ulifanyika sambasamba na ukaguzi wa kawaida wa hesabu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Septemba, 2011, 31

Disemba 2011 na 30 Juni 2012. Matokeo ya zoezi la ukaguzi wa mikataba iliyoingiwa na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yameainishwa sehemu ya 5.2 ya sura hii.

5.1 Usimamizi wa Manunuzi

Kulingana na Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004, manunuzi inamaanisha kununua, kukodisha, kupata bidhaa, ujenzi au huduma inayofanywa na taasisi kwa kutumia fedha za umma, kwa niaba ya Wizara au Idara ya Serikali au Shirika la Umma na ikijumuisha na kazi zote zinazohusiana na kupatikana kwa bidhaa au huduma ikiwa ni pamoja na kuainisha mahitaji, kuteua na kutangaza zabuni na kutoa mikataba. Yafuatayo ni mambo ambayo yalionekana kuwa na kasoro kwenye kaguzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

5.1.1 Manunuzi ya Dharura Yasiyokuwa na Kibali Kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali

Kanuni ya 42 ya tangazo la Serikali namba 97 inaruhusu Mkuu wa Taasisi ya Umma kufanya manunuzi ya kiwango kinachopitiliza mamlaka aliyopewa kisheria pale tu itakapothibitika kuwa manunuzi hayo ni kwa manufaa ya umma. Kwa kufanya hivyo mkuu wa taasisi husika anaelekezwa na sheria kuomba kibali mrejesho kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi wangu katika nyaraka mbali mbali za manunuzi ndani ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ulibaini mapungufu katika utekelezaji wa kanuni hii. Mapungufu haya yalibainika katika Mashirika mawili ambayo ni Mamlaka ya Bandari Tanzania na Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Katika Mamlaka ya Bandari Tanzania ukaguzi ulibaini kuwa mamlaka kupitia Bodi ya Manunuzi ilifanya manunuzi ya dharura ya mitambo ya kupakulia mizigo bandarini yenye thamani ya dola za Kimarekani 810,000 na Euro milioni 13.9 bila idhini mrejesho kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hali kadhalika ukaguzi ulibaini kuwa Chuo Kikuu Mzumbe

kilifanya manunuzi ya dharura yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.987 bila idhini mrejesho kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

5.1.2 Utekelezaji wa Manunuzi Bila Uwepo wa Mikataba Halali na Watoa Huduma

Mkataba ni makubaliano ya hiari kati ya pande mbili ambapo kila upande una hiari kuweka wajibu wa kisheria miongoni mwao. Wajibu wa kisheria wa kuweka sahihi katika mikataba na usimamizi wa utekelezaji wake ni jukumu la watendaji wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 33 (h) na (k) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya Mwaka 2004.

Katika ukaguzi wa hesabu za Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha, nilibaini kuwepo manunuzi ya huduma za madaktari na washauri mbali mbali katika kituo cha afya kinachosimamiwa na taasisi hii bila kuwepo na makubaliano ya kimkataba kati ya madaktari na utawala wa kituo. Chini ya uvunjifu huu wa sheria nilishindwa kuridhika na uhalali wa malipo yaliyolipwa kwa madaktari yenye thamani ya Shilingi milioni 170.95. Katika Mamlaka ya Bandari Tanzania ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ilipokea huduma za matibabu zenye thamani ya Shilingi milioni 725.1 kutoka hospitali binafsi za Tumaini, Hindu Mandal, Regency na Family Care zote za Jijini Dar es Salaam bila kuwa na mikataba ya kisheria na watoa huduma.

Kasoro kama hizi zimebainika pia katika Chuo Cha Ushirika na Mafunzo ya Biashara ambapo kiasi cha Shilingi milioni 201.1 kililipwa kwa wadhamini wa shule ya sekondari ya Wazalendo ikiwa ni kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya shule ndani ya eneo la chuo. Kwa mujibu wa nyaraka mbali mbali zilizokaguliwa majengo haya yatakuwa ni mali ya chuo baada ya ujenzi wake kukamilika. Hata hivyo hapakuwa na mkataba wowote ulioandikwa na kutiwa sahihi kati ya wadhamini wa shule na uongozi wa chuo. Hali kama hii

ilibainika katika ukaguzi wa hesabu za Chuo Cha Biashara ambapo chuo kiliingia makubaliano yasio na mkataba wa kimaandishi na wahadhiri wasio wafanyakazi wa kudumu.Chuo Kikuu Mzumbe kilipokea huduma ya utengenezaji wa magari ya chuo kutoka karakana binafsi bila kuwa na mkataba. Vivyo hivyo Shirika la Nyumba la Taifa lilipokea huduma za matibabu Shilingi 196.4, huduma za ulinzi Shilingi milioni 292.5 na huduma za tiketi za ndege Shilingi 289.4 bila kuwa na mkataba na watoa huduma.

5.1.3 Manunuzi ya Bidhaa na Huduma Nje ya Mpango wa Mwaka wa Manunuzi

Mapitio ya nyaraka mbalimbali za manunuzi katika Chuo cha Elimu ya Biashara yalibaini kuwepo kwa ukiukwaji wa Sheria ya Umma ya Manunuzi ya Mwaka 2004 katika manunuzi ya bidhaa na huduma mbali mbali kwa ajili ya sherehe ya mahafali kwa gharama ya Shilingi milioni 162.2. Ukiukwaji huu ulitokana na manunuzi hayo kutokuwepo kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka ulioidhinishwa na Bodi ya Manunuzi ya Chuo. Manunuzi ya aina hii yalibainika pia kufanyika katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma ambapo Shilingi milioni 116.5 zilitumika kununulia mabomba na viunganishi vyake nje ya mpango wa manunuzi ulioidhinishwa. Katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara Shilingi milioni 16.6 zilibainika kugharamia miradi ya maji nje ya mpango wa manunuzi wakati katika Bohari ya Madawa Shilingi bilioni 1.1 zilitumika kununulia bidhaa na huduma mbalimbali nje ya mpango wa manunuzi ulioidhinishwa. Kadhalika ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ulibaini ukiukwaji wa sheria ya manunuzi ambapo manunuzi ya Shilingi bilioni 1.2 yalifanyika nje ya mpango wa manunuzi ulioidhishwa na Mamlaka.

Mapitio ya nyaraka za zabuni na mpango wa manunuzi wa mwaka katika Benki Kuu tawi la Mbeya ulibaini uwepo wa manunuzi nje ya mpango wa mwaka wa manunuzi kutoka kwa Mkandarasi TECHNIX (T) Ltd yanayofikia kiasi cha

Shilingi milioni 207.3. Sambamba na hilo zabuni ya ukarabati wa jengo la zahanati iliyogharimu Shilingi milioni 48.8 haikuwemo kwenye mpango wa manunuzi. Shirika la Hifadhi ya Jamii lilitumia Shilingi bilioni 1.1 kulipia bidhaa na huduma nje ya mpango wa ununuzi ulioidhinishwa na Mamlaka.

5.1.4 Kukosekana kwa Uwazi Katika Zabuni Zilizoidhinishwa MWAUWASA

Kanuni ya 97 (12) ya tangazo la Serikali Na.97 la Kanuni za Sheria ya Manunuzi ya 2005 inataka matokeo ya zabuni yatangazwe katika tuvuti ya Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Manunuzi ya Umma, gazeti la serikali na angalau magazeti mawili yanayotoka kila siku na kuwafikia wananchi wengi au katika chombo cha uhakika cha mawasiliano. Pia kanuni ya 116 ya sheria hii inamtaka mkuu wa taasisi husika kuhakikisha kuwa nakala za mikataba ya kandarasi zinapelekwa kwa Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Manunuzi ya Umma, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mhakiki Mali za Serikali, Kitengo cha ukaguzi kilicho chini ya Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania ndani ya siku thelathini kutoka tarehe mkataba uliposainiwa. Mapitio ya utekelezaji wa sheria hii katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Jiji la Mwanza yalibaini ukiukwaji wa sheria ambapo manunuzi ya Shilingi bilioni 1.8 zabuni zake hazikuwekwa wazi kwa umma.

5.1.5 Muingiliano wa Utendaji Kati ya Mihimili Mikuu ya Manunuzi (Mtendaji Mkuu, Bodi ya Zabuni, Kitengo cha Manunuzi)

Kwa mujibu wa kifungu cha 38 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 mihimili mikuu ya manunuzi yaani Mtendaji Mkuu, Bodi ya Zabuni, Kitengo cha Manunuzi, Kamati ya Tathmini na Mtumiaji vinapaswa kufanya kazi kwa uhuru bila kuingiliana. Katika mapitio ya nyaraka za manunuzi katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Jiji la Mwanza nilibaini baadhi ya mapendekezo ya kamati ya

tathmini na yale ya Kitengo cha Manunuzi yalikataliwa na Bodi ya Zabuni bila kuzingatia vigezo vilivyotumika kufanya maamuzi. Kasoro hii ilibainika katika mapitio ya muhtasari Na.81 wa kikao cha Bodi ya Zabuni kilichokaa tarehe 30 Septemba, 2011 na kupitisha kampuni ya PLACCO kuiuzia mamlaka vifaa vya mabomba na viunganishi vyake.

Hali kama hii pia ilijitokeza katika Shirika la Bandari Tanzania ambapo maamuzi yaliyopitishwa na kamati ya tathimini hayakuzingatiwa na Bodi ya Zabuni ya mamlaka kwa kutoa zabuni ya ujenzi wa jengo la kuhifadhia mizigo bandarini kwa kampuni ya ujenzi ya Kiure badala ya kampuni ya Satellite iliyopendekezwa na kamati ya tathmini. Zabuni hii ilikuwa ni ya thamani ya Shilingi milioni 132.7. Katika mazingira yanayofanana na hayo wafanyakazi wa kitengo cha manunuzi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro waliteuliwa kuwa wenyeviti katika kamati ya tathmini. Hali kama hii ilijitokeza pia katika shirika la Hifadhi ya Jamii ambapo wajumbe wa kitengo cha manunuzi walihusishwa kwenye kamati za tathmini za zabuni.

5.1.6 Manunuzi ya Madawa ya Ukimwi na Vifaa ya Ubora wa Chini MSD

Katika ukaguzi niliofanya kwenye Bohari ya Madawa nilibaini mapungufu katika ukaguzi na upokeaji madawa na vifaa tiba tatizo linalopelekea kuharibika kwa madawa na kutobaini salio la dawa. Bohari inakabiliwa na tatizo la kutokuwa na maabara Maalum kwa ajili ya kuhakiki ubora wa madawa yanayonunuliwa. Hii inapelekea uhakiki wa ubora wa madawa yanayonunuliwa na Bohari kuhusisha taasisi nyingine kama Taasisi ya Chakula na Lishe, Shirika la Viwango na Mkemia Mkuu wa Serikali ambapo hakuna taratibu zilizoanishwa ni dawa zipi zipelekwe kwenye hizi maabara na zipi hazihitaji kupelekwa. Kwa mfano madawa yanayosambazwa na kampuni ya Zenufa yalizuiliwa kutumika baada ya kupimwa na Mamlaka ya Chakula na Lishe wakati dawa hizo hizo zilishakaguliwa na kupata kibali cha kutumika na Bohari ya

Madawa. Hali kadhalika madawa ya kurefusha maisha kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI (ARVs LAMIVUDINE 150MG+ STAVUDINE 30MG+NEVIRAPINE 200MG (TT-VIR 30) yalizuiliwa kusambazwa baada ya kutokidhi viwango wakati kwa mujibu wa ukaguzi wa Bohari dawa hizi hazikuonekana kuwa na tatizo. Dosari hizi zinaweza kupelekea upokeaji na usambazaji wa dawa zisizo na kiwango na hivyo kusababisha madhara makubwa kwa watumiaji.

5.1.7 Kutokuwepo na Uwazi kwenye Manunuzi Yaliyofanywa Kupitia GPSA

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini ni Wakala Mkuu chini ya Wizara ya Fedha iliyoanzishwa kwa sheria ya wakala Na.30 ya mwaka 1997 kupitia tangazo la Serikali Na.235 la tarehe 7 Disemba,2007. Kazi za Wakala zimeainishwa kuwa ni kununua, kutunza na kusambaza bidhaa zenye ubora kwa Serikali kupitia Makao yake Makuu yaliyoko Dar es Salaam na kwenye mikoa ishirini na moja (21) ya Tanzania Bara ikiwa ni pamoja na kutoa huduma ya kupokea na kupeleka mizigo nje ya nchi. Kazi nyingine ni kupanga manunuzi ya bidhaa zinazotumiwa mara kwa mara na serikali na taasisi zake chini ya mkataba maalum na watoa huduma mbalimbali nchini.

Mapitio ya manunuzi mbalimbali yaliyofanyika katika Mashirika ya Umma kupitia Wakala wa Ununuzi ilibainika kuwa hapakuwa na uwazi katika manunuzi yaliyofanyika kwa mwaka husika. Mapungufu haya yalibainika kwenye manunuzi yaliyofanywa na Bohari ya Madawa kupitia Wakala wa manunuzi kwa mwaka 2011/2012 kwa kuteua moja kwa moja mtoa huduma toka kwenye orodha iliyopitishwa na Wakala na kumpa mkataba badala ya kuteua zaidi ya mmoja ili washindanishwe kwa misingi ya bei na ubora wa bidhaa. Utaratibu huu unaonekana kutokuwa sahihi kwani unaweza kutoa upendeleo kwa mtu aliye karibu na ofisa anayetoa zabuni. Katika Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro mamlaka ilimteua mtoa huduma kutoka orodha ya Mamlaka ya Ununuzi ambapo

alitoa huduma ya vifaa na huduma za thamani ya Shilingi bilioni.3.746 bila mkataba wowote kwa mtizamo usio sahihi kwamba mkataba wa Wakala wa Ununuzi ni toshelevu katika manunuzi yaliyofanyika.

5.1.8 Matumizi ya Njia Zisizo Sahihi Katika Manunuzi

Njia sahihi ya kuepukana na manunuzi yasiyofuata taratibu ni kutumia mfumo wa ushindani kama ilivyoanishwa katika tangazo Na.97 la kanuni za sheria ya manunuzi ya mwaka 2005 kifungu cha 63(1). Hata hivyo kwa mujibu wa vifungu vya 70,71,na 72 vya kanuni hizo, taasisi ya umma inaruhusiwa kisheria kutumia njia nyingine nje ya ile ya ushindani kama zilivyoainishwa kwenye sheria.Katika ukaguzi wa hesabu za Shirika la Nyumba kwa mwaka wa fedha 2011/2012 nilibaini kuwa shirika hutumia mfumo wa kandarasi mbalimbali (Force Accounting) lakini katika utaratibu ambao sio ule ulioainishwa kwenye sheria ya manunuzi. Nilibaini kuwa shirika lilitumia mfumo usio na ushindani katika kununua magari yenye thamani kati ya Shilingi bilioni.1.453 na Shilingi bilioni 1.878 bila ushindani kinyume na sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005 ambayo ilipelekea kuwepo kwa tofauti ya Shilingi milioni 425.5 zaidi ya makadirio.

Katika ukaguzi wa Shirika la Umeme Tanzania ukaguzi ulibaini kuwa shirika liliingia mkataba na kampuni ya Quality Trade and Distribution Ltd katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa njia za umeme kwenye mradi wa wateja 100,000 kwa gharama ya dola za kimarekani 23,189,146.54 na Shilingi milioni 976.8. Katika zabuni hii matakwa ya kanuni za sheria ya manunuzi Na.97 ya mwaka 2005 kifungu cha 42 na 69 hayakuzingatiwa.

Hali kadhalika ukaguzi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ulibaini manunuzi ya kandarasi za ujenzi zilizoigharimu Mamlaka Shilingi milioni 165 kutoka kampuni ya Mount Cliff General Enterprises; Shilingi milioni 205 kutoka kwa Tumaini Civil works na Dola za Kimarekani

35,430.68 kutoka kwa CMC Automobile. Pia ukaguzi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulibaini kiasi cha Shilingi bilioni 3.392 kilitumika kununulia bidhaa bila ushindani. Halikadhalika Shilingi bilioni. 1.079 zilikutumika kununua bidhaa mbalimbali katika Mfuko huu bila kufuata ushindani kwa mujibu wa jedwali la tatu la Kanununi za manunuzi za mwaka 2005.

5.1.9 Manunuzi Yasiyokuwa Kwenye Bajeti ya Manunuzi

Kifungu cha 46 (9) cha Kanuni ya Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2005 kinataka manunuzi katika taasisi za umma na Serikali kufanyika kuendana na uwezo wa bajeti ya mwaka husika. Kwa mujibu wa kifungu cha 25 (3) cha sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 hakuna manunuzi yatakayofanyika nje ya vifungu vilivyoidhinishwa na bajeti isipokuwa pale tu kama matumizi hayo yameidhinishwa na Bodi au kwa kutumia marudio ya bajeti. Kufuatana na taratibu hizo mpango wa utekelezaji unatakiwa kufuata mpango kazi wa mradi husika utakaoleleza utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mradi na jinsi ya upatikanaji wa fedha za kutekeleza mradi husika. Kinyume na taratibu zilizoanishwa hapo juu, nilibaini matumizi katika bajeti za baadhi ya Mashirika ya Umma nje ya mipango ya manunuzi iliyoidhinishwa na kuwasilishwa Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma. Haikuweza kubainika kama manunuzi haya yasiyofuata bajeti kama yaliwasilishwa katika malaka husika (PPRA) kwa ajili ya kuidhinishwa. Mifano halisi ya ukiukwaji wa sheria hii ni katika shirika la Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Shilingi milioni 47.093; Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro Shilingi bilioni 2.707 na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Shilingi milioni 253.4.

5.1.10 Manunuzi ya Huduma za Kisheria Bila Kuzingatia Sheria ya Manunuzi

Ukaguzi wa hesabu za Shirika la Umeme ulibaini kuwa Shirika lilinunua huduma za kisheria toka kampuni ya Rex Attorney and Reed Smith/ Matrix Chambers kusaidia maswala ya kisheria dhidi ya DOWANS.

Kwa mujibu wa kumbukumbu, sababu za TANESCO kushitakiwa katika mahakama ya kimataifa ya biashara na Dowans ni kutokana na mkataba ambao Dowans iliurithi kwa Richmond Development Company LLC kampuni ambayo baadae ilikuja kugundulika kuwa haipo. Endapo kama menejimenti ya TANESCO ingefanya utafiti kwa umakini ingeweza kugundua kuwa kampuni ya Dowans haipo kisheria. Licha ya TANESCO kutokuwa makini katika kuchunguza uhalali wa kuwepo kwa Dowans, shirika hili pia halikuwa makini kutambua kama Rex Attorney ilikuwa imesajiliwa na BRELA na kama Reed Smith/Matrix Chambers ilikuwa imesajiliwa na Wakala wake nchini Uingereza. Hata muungano wa kibiashara kati ya Rex Atorney na Reed Smith/Matrix Chambers haukuweza kuwekwa bayana. Kwa hali hiyo TANESCO iliingia mkataba na kampuni hizi bila ya kuhakiki na kuridhika na maswala ya kisheria ya kuwepo kwake. Manunuzi ya jinsi hii yanapaswa kuepukwa ili kulinda uhai wa shirika na rasilimali za Taifa.

5.1.11 Manunuzi ya Bidhaa Ambayo Hayakupitishwa na Bodi ya Zabuni

Kifungu cha 68 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 kinaelekeza wanunuaji kuhakikisha kuwa zabuni zote zinapitishwa na bodi ya zabuni.

Wakati wa ukaguzi wa hesabu za STAMICO nilibaini kuwa bodi ya zabuni haikuhusishwa katika manunuzi ya mashine mbili mbili (2) za kupasua miamba zilizonunuliwa kwa gharama ya Shilingi milioni 167.543 kutoka nchini China. Mashine hizi zilinunuliwa kwa kutumia mfumo wa manunuzi wa chanzo kimoja. Gharama za manunuzi zilijumuisha gharama nyingine za kufunga mashine zilizogharimu shirika Shilingi milioni 36.75. Pamoja na ghrama zote zilizotumika mashine hizi hazikufanya kazi katika mradi uliokusudiwa wa Mikindani/ Mtwara ambao muda wake uliisha Aprili, 2012. Ni wazi kuwa thamani ya fedha haikuzingatiwa kabla ya manunuzi.

Hali kadhalika mapitio ya hesabu za Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro yalibaini kwamba manunuzi ya zabuni Na.AE/055/2011-12/HQ/G/048 iliyohusiana na ununuzi wa huduma ya usafirishaji wa tani 99 za mahindi kupitia kampuni ya Marko Panga kwa gharama ya Shilingi milioni 69.532 hayakupitishwa na Bodi ya zabuni ya Mamlaka.

5.1.12 Utoaji wa Zabuni Nje ya Taratibu Zilizowekwa-NSSF

Ukaguzi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulibaini matumizi ya Shilingi milioni 230 ambayo yalipitishwa na bodi ya zabuni lakini hayakuwa sahihi kwa mujibu wa makisio yaliyoandaliwa na Wahandisi. Kwa mujibu wa vipimo vya Wahandisi gharama ya manunuzi ilikuwa Shilingi milioni 200 lakini Bodi ya zabuni ilipitisha Shilingi milioni 430 yaani Shilingi milioni 230 zaidi ya gharama za makadirio toka kwa Wahandisi. Matumizi haya yalikuwa ni kwa ajili ya kununulia vipooza hewa katika nyumba za shirika zilizoko Kaloleni Arusha. Katika maelezo yaliyotolewa na menejimenti ni kwamba makisio haya yalikuwa ni ya miaka ya nyuma na hivyo yalikuwa yameshaathiriwa na mfumuko wa bei. Hata hivyo sababu hii haikutosheleza kuelezea sababu za kupanda kwa gharama kwa zaidi ya asilimia mia moja (100%).

5.2 Usimamizi wa Mikataba

Kulingana na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004, mkataba wa manunuzi unamaanisha leseni, kibali au makubaliano ya aina yoyote yaliyoingiwa na taasisi za umma na wazabuni au mjenzi unaotokana na mchakato wa ununuzi kwa ajili ya kununua bidhaa, ujenzi au kupata huduma. Katika ukaguzi wa mikataba kwenye Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma mambo yafuatayo yalibainika:

5.2.1 Usimamizi Mbovu wa Mkataba wa Ujenzi wa Gati Katika Ziwa Tanganyika

Katika ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Bandari Tanzania ilibainika kuwa mnamo tarehe 20 Novemba, 2009 Mamlaka iliingia makubaliano na kampuni ya Modspan Enterprises Ltd kusanifu na kujenga Gati katika Ziwa Tanganyika kweye maeneo ya Logasa, Kyala, Karema and Kirando kwa gharama ya Shilingi bilioni 4.870. Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizokaguliwa mkataba huu ulikuwa wa miezi kumi na nane (18) uliotarajiwa kukoma mwezi Julai 2011.

Mapitio ya utekelezaji wa mkataba huu yaligundua kwamba mradi ulikutana na vikwazo vilivyosababishwa na mipango hafifu na kutokuwajibika kwa menejimenti ya Bandari. Kwa mfano nilibaini kuwa mradi ulipata vikwazo kadhaa ambavyo ni pamoja na mgogoro wa ardhi, mkandarasi kutoonyeshwa eneo sahihi la kufanyia kazi, eneo la mradi kuwa mbali kinyume na matarajio ya mkandarasi na hali ya hewa isiyoridhisha. Yote haya yalichangia mradi kutokamilika kwa wakati yaani Disemba 2012. Kwa maoni ya ukaguzi kasoro zote hizi zilipaswa kuainishwa mapema kabla ya mradi kuanza kitu ambacho menejimenti haikufanya.

Ukaguzi wa kina katika mradi huu ulibaini pia kwamba mkandarasi Modspan Enterprises Ltd hakuwajibika ipasavyo katika mradi aliopewa, kasoro iliyopelekea Wahandisi wa Mamlaka kutumia muda mwingi na gharama kubwa kumsimamia mkandarasi. Ukaguzi huu uligundua pia kulikuwa na tatizo la malipo duni kwa wafanyakazi wa mradi pamoja na kutopatikana kwa vitendea kazi kitu kilichopelekea kutoelewana kati ya msimamizi wa mradi na mkandarasi. Licha ya mapungufu yote haya menejimenti ilitoa nyongeza ya kazi kwa mkandarasi kwa kiasi cha Shilingi milioni 647.865 hivyo kupelekea gharama za mradi huu kuongezeka hadi kufikia Shilingi bilioni 5.518 kutoka gharama za awali za Shilingi bilioni 4.870. Kufikia kipindi nilichokuwa nakamilisha ukaguzi huu jumla ya Shilingi

bilioni 3.126 sawa na asilimia 56.6 ya jumla ya gharama za mradi zilishalipwa kwa mkandarasi ambapo sehemu ya kazi iliyokamilika ilikuwa asilimia 34 tu.

5.2.2 Ucheleweshwaji wa Kukamilika kwa Mkataba wa Marejeo ya Ikama na Muundo wa Mishahara Katika Mamlaka ya Bandari

Mamlaka ya Bandari Tanzania iliingia mkataba na kampuni ya Delloitte Consulting mnamo tarehe 19/1/2011. Kampuni ilitakiwa kupitia na kutoa ushauri kwenye ikama ya Mamlaka na muundo wa mishahara wa Mamlaka kwa gharama ya Shilingi milioni 67.881bila kodi ya ongezeko la thamani. Kazi hii ilitarajiwa kukamilika tarehe 4/3/2011 kwa mkandarasi kukabidhi ripoti ya mwisho kwa mamlaka. Ukaguzi wa kina juu ya kumbukumbu mbalimbali zilizowasilishwa kwa wakaguzi iligundulika kwamba kulikuwa na ucheleweshwaji uliosababishwa na ushiriki duni wa menejimenti katika kumpatia mkandarasi taarifa husika. Dosari hii ilibainika kwenye kumbukumbu za kikao cha 135 cha bodi ya zabuni kilichokaa tarehe 1/12/2011 ambacho kilithibitisha kuwa mradi unasuasua kutokana na ushiriki duni toka kwa Mamlaka. Zaidi ya hayo nilibaini pia kwamba mkataba ulikumbwa na tatizo la kusogezwa mbele mara kwa mara kwa tarehe ya kukamilika kwake. Mara ya mwisho ilikubalika kuwa mradi utakamilika tarehe 28/12/2011. Kusuasua huku kwa mradi kulipelekea gharama kuongezeka kwa Shilingi milioni 36.32 sawa na asilimia 54 ya bei ya awali.

5.2.3 Kukosekana kwa Umakini Katika Kuaandaa na Kusimamia Mikataba

Katika ukaguzi wa mikataba na usimamizi wake uliofanyika katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma niligundua udhaifu mkubwa katika usimamizi wa mikataba uliopelekea kuongezeka kwa gharama za manunuzi na hatimaye kushindikana kufikia malengo yaliyokusudiwa katika Taasisi husika. Haya yalibainika katika ukaguzi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania ambapo Mamlaka iliingia mkataba na

kampuni ya Edcat International Ltd kufanya marekebisho ya lango Na.2 na 3 pamoja na lango la makao makuu kwa gharama ya Shilingi milioni 214,698. Mkataba huu ulitiwa saini tarehe 5/05/2011 na ulitarajiwa kukamilika baada ya miezi minne.

Ukaguzi huu ulibaini kuwa mradi haukuweza kukamilika kama ilivyokubaliwa ndani ya mkataba kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara yaliyoongeza ukubwa wa kazi, kubadilika kwa aina ya vifaa vya ujenzi na mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa maoni ya mkaguzi mabadiliko haya yalitokana na kukosekana kwa umakini katika kuandaa na kusimamia mkataba huu hivyo kupelekea muda wa kukamilika kwa mradi kusogezwa mbele kutoka Septemba 2011 hadi Juni 2012 na malipo ya gharama za ziada kiasi cha Shilingi milioni 239.865 au asilimia 89.5 ya gharama za awali.

Usimamizi duni wa mikataba katika mamlaka hii ulibainika pia kwenye mkataba kati ya Mamlaka na kampuni ya Soft Tech Consultants Ltd. Mkataba huu ulihusu kuiuzia, kufunga na kufundisha watumiaji namna ya kutumia mifumo hii ya kompyuta katika kuandaa malipo ya mishahara, kutunza kumbukumbu za rasilimali watu, kutunza na kuaandaa ripoti za kihasibu na bohari. Mkataba huu ulitiwa sahihi tarehe 14 Julai, 2010 kati ya Mamlaka ya Bandari na kampuni ya Soft Tech Consultants kwa makubaliano kwamba utakamilika baada ya miezi mitano (5) yaani tarehe 14 Januari, 2011.

Mapitio ya utekelezaji wa mkataba huu yalibaini kuwepo kwa mfululizo wa kusogeza tarehe ya kumalizika kwa mkataba kulikosababishwa na mkandarasi kushindwa kuwajibika ipasavyo katika kuhakikisha anamaliza kazi kama ilivyokubaliwa katika mkataba. Katika ombi la kwanza tarehe ya kukamilika mkataba ilisogezwa mbele kwa miezi mitano (5) kisha miezi miwili (2) hadi tarehe 14 Julai, 2011. Pamoja na nyongeza hii ya muda mkandarasi hakuweza

kukamilisha kazi. Kwa kuliona hili Mamlaka na Mkandarasi waliingia makubaliano mapya tarehe 31 Agosti, 2011 ukiwa na kipengele cha kuongeza muda wa kukamilika kwa mkataba na pia kipengele kipya cha kutoa huduma ya mafunzo kwa watumiaji wa mifumo hii ya kompyuta kwa gharama ya dola za Kimarekani 31,860 kwa muda wa siku 54. Pia ukaguzi ulibaini kuwa Mkurugenzi wa mifumo ya kompyuta kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu alisogeza mbele tarehe ya kukamilika kwa mkataba hadi 31 Agosti 2012 akimsisitiza mkandarasi kumaliza na kukabidhi kazi kabla ya Agost 2012. Maamuzi haya hayakusaidia kuiwezesha mamlaka kupata ilichokusudia na hadi kufikia tarehe ya kukamilika kwa ukaguzi Novemba, 2012 hapakuwepo na dalili kwamba mkandarasi angemaliza kazi ya kufunga mifumo ya kompyuta katika Mamlaka ya Bandari.

5.2.4 Kusitishwa kwa Mkataba Kulikopelekea Malipo Yasio na Faida kwa Mamlaka ya Bandari

Mamlaka ya Bandari Tanzania iliingia mkataba na kampuni ya Oceana Advanced Industries Ltd mwezi Novemba 2008 kukarabati sehemu ya meli kutia nanga katika lango Na.1-11 na kituo cha kupakulia mafuta cha Kurasini katika Bandari ya Dar es Salaam. Kwa mujibu wa makubaliano gharama za mkataba huu ni Shilingi bilioni 4.633 bila kodi na ukarabati ulitakiwa ukamilike kufikia tarehe 11 Mei 2009. Mapitio niliyofanya katika mkataba huu nilibaini kuwa mkataba haukuweza kukamilika kwa muda hivyo kulazimu muda kuongezwa kwa miezi minne (4) hadi Agosti, 2009 kutokana na menejimenti ya Bandari kushindwa kumkabidhi Mkandarasi eneo husika la kazi (berth 7). Kushindwa kutekeleza kwa mkataba huu kulitokana na kutofanyika kwa utafiti wa kina kabla ya kutoa zabuni na hivyo kusababisha kuibuka kwa kazi za ziada zilizogharimu kiasi cha Dola za Kimarekani 753,807.60

Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2010 mkandarasi alikuwa hajakamilisha kazi na hivyo menejimenti iliamua kusitisha mkataba na Oceana Advanced Industries Ltd kwa kisingizio

kwamba kulikuwa na msongamano wa meli katika Bandari ya Dar es Salaam hivyo kazi isingeweza kuendelea. Kusitishwa kwa mkataba huu kuliilazimu Mamlaka kumlipa mkandarasi fidia ya Shilingi bilioni 1.657 zikiwa ni gharama za fidia kwa vitendea kazi vyake kukaa muda mrefu bila kufanya kazi. Hata hivyo malipo haya hayakulipwa kwa wakati hivyo kupelekea mkandarasi kutoza riba ya Shilingi milioni 584.634 na kupelekea malipo yaliyolipwa bila Mamlaka kunufaika kihuduma kuwa Shilingi bilioni 2.242.

5.2.5 Usimamizi Dhaifu wa Mkataba Katika Shirika la Hifadhi za Wanyama Pori

Katika ukaguzi wa hesabu za Shirika la Hifadhi ya Wanyama Pori nilibaini kuwa Shirika liliingia mkataba na kampuni ya Glocal Investment ya nchini Uturuki kutengeneza na kutangaza utajiri wa mali asili ya Tanzania katika hifadhi za wanyama pori kupitia magazeti, majarida na kupitia mbao za matangazo kwa gharama ya dola za Kimarekani 198,000. Kwa mujibu wa makubaliano mkataba huu ulimtaka mkandarasi kumpatia mwajiri (TANAPA) nakala za magazeti na majarida ambayo matangazo ya vivutio vya utalii vimetangazwa nchini Uturuki ikiwa ni pamoja na ratiba ya vipindi vya runinga ambapo matangazo hayo yatakuwepo. Hii ni pamoja na kmpatia mwajiri taarifa za kila robo mwaka kuhusiana na matangazo yaliyorushwa hewani.

Mapitio ya utekelezaji wa makubaliano katika mkataba huu yalibaini kwamba mkandarasi hakuweza kumpatia mwajiri taarifa muhimu kama walivyokubaliana yaani taarifa za kila mwezi za majarida na magazeti ambayo matangazo yaliwekwa na kusomwa nchini Uturuki. Kasoro hizi zilishindwa kuthibitisha kwamba matangazo yalitengenezwa na kurushwa na radio, runinga na matangazo mengine ya maeneo ya wazi. Hali kadhalika ziara tatu (3) za waandishi wa habari zilizopangwa kufanyika zikijumuisha wanahabari watano lakini haikuweza kufanyika badala yake ni safari moja tu iliyofanikiwa kinyume na mkataba kati ya TANAPA na kampuni ya Global Investment.

5.2.6 Ukiukwaji wa Makubaliano Katika Mikataba Inayoingiwa na Wanunuzi

Katika mapitio ya hesabu za Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kigoma Ujiji kwa mwaka wa fedha ulioishia 2011/2012 niligundua kuwepo kwa usimamizi dhaifu katika mkataba wa ununuzi wa mita za maji 500 kutoka kampuni ya CERAMIC Investment. Mapitio haya yalibaini kwamba mamlaka iliingia mkataba na mkandarasi kwa makubaliano kwamba mita 500 zilizoagizwa zitaifikia mamlaka wiki moja baada ya kusaini mkataba yaani tarehe 22 Juni, 2011. Kinyume na makubaliano mkandarasi alipeleka mita 200 tarehe 10/08/2011 badala ya mita 500 ambapo mita 300 zilizosalia hazikuletwa baada ya menejimenti kutokufanya malipo ya mita 200 zilizoletwa awali. Kwa kigezo cha kutotimiza masharti yaliyomo kwenye mkataba menejimenti iliamua kuuvunja mkataba huu na mpaka ukaguzi huu unahitimishwa hakuna tozo au adhabu yoyote iliyofanyika kwa mkandarasi.

Katika shirika la Hifadhi ya Jamii ilitolewa taarifa ya ucheleweshwaji wa manunuzi ya bidhaa za kiasi cha Shilingi milioni 676 na hakuna tozo lililofanyika kwa kosa la kuchelewa kuleta mali iliyoagizwa. Kwa mfano manunuzi ya vifaa vya kuunganisha na mfumo wa kompyuta kutoka kwa Computech ICS Ltd vyenye thamani ya Shilingi milioni 83.3 vilichelewa kwa siku 58 lakini hakuna hatua yeyote iliyochukuliwa na Shirika dhidi ya ucheleweshwaji huu ingawa mkataba unaanisha kuwepo kwa tozo ya asilimia 10 (10%). Hali kadhalika nilibaini kuwa usimamizi wa mikataba hauhusishi kitengo cha manunuzi kinyume na sheria ya Manunuzi. Hii imethibitishwa na ukweli kwamba kitengo cha manunuzi hakikuwa na daftari lenye kumbukumbu sahihi za utekelezaji wa mikataba.

5.2.7 Usimamizi Mbovu wa Mikataba Katika Shirika la Umeme

Kigezo kikuu cha mkataba kuwa halali ni pale ambapo unatiwa saini na pande mbili husika.Hali ilionekana tofauti kwa menejimenti ya TANESCO kama ilivyothibitishwa katika

zabuni Na. PA/001/10/HQ/G/001 inayohusiana na ununuzi wa nyaya, transfoma na mita. Katika kandarasi hii kampuni ya Landis and Gyr (Pty) iliiuzia TANESCO mita za malipo ya awali 100A-200A na mita za ARM kwa gharama ya Euro3,052,350 wakati kampuni ya Namjusa iliiuzia TANESCO nyaya za vipimo mbalimbali kwa gharama ya Dola za Kimarekani 375,210. Mikataba hii ilitiwa saini lakini haikutekelezwa kwa kile kilichoelezwa kuwa ni manunuzi ya nje na hapakuwa na fedha katika akaunti ya benki. Malipo ya awali yalilipwa Mwezi Novemba, 2011 kiasi cha Euro 152,617 (10& ya mkataba) kwa barua kumb.Na. Ref No CFO/MTS/PSO/63/74 iliyopelekwa benki ya CRDB ambapo ni miezi mitano tangu mkataba kusainiwa. Hii ni kinyume na kifungu cha 121 (1) cha sheria ya manunuzi kwa tangazo la serikali Na.97 la mwaka 2005 kinachotataka taasisi za umma kuhakikisha kuwa kuna fedha za kutosha kabla ya kuamua kununua bidhaa au huduma.

5.3 Matokeo ya Ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma Katika Mashirika 45

Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004 inaipa nguvu Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma kufanya ukaguzi wa manunuzi na kutoa ripoti. Kwa kipindi hiki cha ukaguzi, mamlaka ilifanya ukaguzi katika Mashirika ya Umma arobaini na tano (45). Kwa ujumla ukaguzi wa manunuzi katika mashirika haya ulilenga kutambua kama taratibu zote za manunuzi zimefuatwa kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 na kwamba manunuzi yaliyofanyika yalilenga kuleta tija kiuchumi na pia kama yalilenga kuleta ufanisi kwa kuhakikisha kuwa mikataba yote inatekelezwa kwa mujibu wa makubaliano yaliyopo.

Kwa ujumla matokeo ya utekelezaji wa sheria yameonyesha kuwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yanafuata sheria kwa asilimia sabini na sita (76%). Matokeo haya ni chini ya malengo yaliyowekwa ya asilimia themanini (80%). Hata hivyo matokeo haya yanaonyesha kiwango cha

utekelezaji wa sheria kimepanda kwa mwaka 2011/2012 asilimia sabini na nne (74%) ukilinganisha na mwaka 2010/2011 asilimia sitini na nane (68%) iliyotokana na upimaji wa viashiria vitano ambavyo ni: Uanzishwaji wa Bodi za zabuni (80%); Matangazo ya zabuni (85%); Muda wa kuandaa zabuni (90%); Matumizi ya njia sahihi ya nyaraka za zabuni (82%).

Hata hivyo kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma vipimo vya utekelezaji vinaonyesha Mashirika manne (4) ambayo ni sawa na 9% yalipata kiwango cha chini kabisa katika utekelezaji wa sheria; Mashirika 25 ambayo ni sawa na 54% yalipata kiwango cha wastani wakati Mashirika 17 ambayo ni sawa na 37% yalipata kiwango cha kizuri cha utekelezaji wa sheria hii ya manunuzi. Katika vipimo hivi Baraza la Mitihani la Taifa lilipata kiwango cha juu cha utekelezaji wa sheria yaani 94% wakati Shule ya Sheria ilifanya vibaya kwa kupata 51%.

Kwa muhtasari maeneo ambayo bado yanahitaji msukumo kwa mujibu wa ripoti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ni pamoja na:

(i) muundo wa bodi za zabuni kutokidhi matakwa ya sheria,
(ii) udhaifu katika uundwaji wa vitengo vya manunuzi,
(iii) utekelezaji usioridhisha wa mpango wa manunuzi,
(iv) kutotangaza matokeo ya zabuni,
(v) utunzaji mbovu wa kumbukumbu za manunuzi, na
(vi) udhaifu katika usimamizi wa mikataba ya manunuzi.

Ninatoa ushauri kwa menejimenti za Mashirika ya Umma kuongeza juhudi katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa sheria ya manunuzi unazingatiwa katika taasisi wanazoziongoza.

SURA YA SITA

USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA

6.0 Utangulizi

Rasilimali ni mali zinazomilikiwa na Taasisi au Shirika kwa ajili ya matumizi yake ya kila siku katika kuendesha shughuli zake. Rasilimali zinajumuisha mali zinazoshikika na zisizoshikika ambazo taasisi inazimiliki. Mali zisizohamishika, mitambo, vifaa mbalimbali, uwekezaji, fedha taslimu, madeni yanayodaiwa, akiba ya vifaa, mifumo ya ndani ya kompyuta, tovuti na malipo tangulizi.

Sura hii ni muhimu kwa sababu ya changamoto zinazoyakabili Mashirika ya Umma katika kufuatilia na kusimamia rasilimali za Taifa. Pia, pamoja na changamoto hizo, hapa ni mahali ambapo kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na wafanyakazi ambao sio waaminifu wanaoweza kufanya ubadhilifu wa mali za umma. Kwa mwaka huu wa ukaguzi, nimeainisha masuala ambayo ni muhimu kwa Serikali na Bunge kuyatolea maelekezo ya namna nzuri ya kuyatekeleza kama ifuatavyo:

6.1 Shirika la Utangazaji la Tanzania Katika Matatizo ya Ukwasi

Shirika la Utangazaji la Tanzania ni shirika la umma ambalo linawajibika kwa umma kupitia vipindi vyake inavyovitangaza nchi nzima bila ya kujali itikadi, dini, tabaka au maumbile.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nimebaini kwamba Shirika la Utangazaji la Tanzania limeripotiwa kuwa na hasara ya Shilingi za Kitanzania bilioni 1.589 (2011: Shilingi bilioni 1.135) na linaitegemea Serikali kwa kiasi kikubwa katika mahitaji yake ya kujiendesha na kulipia madeni mbalimbali. Hali hii inaleta wasiwasi kuhusiana na uwezo wa Shirika kuendelea kujiendesha lenyewe katika wakati ujao.

Shirika lipo shakani kushindwa kulipa madeni yake ya muda mfupi kwa madeni muhimu na matokeo yake Shirika linaweza kushindwa kutoa huduma yake ya matangazo kwa ufanisi. Endapo hali hii itaendelea kwa kipindi kirefu shirika linaweza kushindwa kuendelea na biashara au kujiendesha (going concern).

6.2 Hali Mbaya ya Mwenendo wa Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF)

Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF) ulianzishwa na unaongozwa na kifungu Na.2 cha sheria Mafao ya Wastaafu ya Watumishi wa Umma ya mwaka 1999. Mfuko huu wa mafao ya kustaafu ya wastaafu kwa watumishi wa muda mrefu na pensheni kwa Serikali Kuu ya Tanzania na Taasisi zilizoundwa kikatiba.

Ukaguzi wa Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF) ulibaini kwamba, "acturial valuation" ilifanyika mara ya mwisho tarehe 30 Juni, 2010 na Kampuni ya Genesis Actuarial Solutions ambayo ni, kampuni ya kujitegemea ya ukadiriaji thamani na ushauri ambayo ilionyesha kuwa hali ya kifedha ya Mfuko iliendelea kuwa mbaya. Ukadiriaji thamani ulibaini hasara halisi ya Shilingi trilioni 6.487 kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010.

Pia nilibaini kwamba katika mwaka wa fedha wa 2011, Serikali ilikubali kuanza kurejesha mafao yaliyolipwa awali na Mfuko kuanzia mwaka 2004 hadi 2010 kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 716. Kiasi hiki kilipaswa kurejeshwa kidogo kidogo na Serikali kila mwaka katika mgawanyo wa Shilingi bilioni 71.6 kwa muda wa miaka kumi kuanzia mwaka 2010. Kufikia mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 kulikuwa na malimbikizo ya marejesho katika kipindi cha mwaka 2011 hadi 2012 na kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 133.

Vile vile, ilibainika kwamba, Serikali ya Tanzania haikuweza kutoa fedha za kuziba pengo la upungufu uliojitokeza kama ilivyoonyeshwa katika barua yenye kumbukumbu Na CHC: 191/338/01/021 ya tarehe 15 Juni, 2009 ikiashiria kuwepo kwa shaka kuhusiana na uwezo wa Mfuko kuendelea kulipa madeni yake yanapokuwa tayari kwa kulipwa.

6.3 Ukosefu wa Umiliki Halali wa Mali

Umiliki wa mali zisizohamishika unamaanisha umiliki wa kisheria unaothibitishwa na hati miliki au nyaraka nyingine zinazoweza kuthibitishwa kisheria. Kinyume cha hapo shirika au taasisi haina uhalali wa kisheria juu ya mali inayomiliki endapo kutakuwa na madai ya umiliki na mtu mwingine. Uhakiki wa mitambo, vifaa na majengo yanayomilikiwa na Mashirka ya Umma na Taasisi Nyinginezo za umma ulibainisha kuwa mali nyingi hazikuwa na uthibitisho wa umiliki wa kisheria. Matokeo ya kutokuwa na umiliki halali kunafanya mkaguzi ashindwe kuthibitisha umiliki wa mali hizo na thamani zake katika vitabu vya hesabu. Kwa mfano, uchunguzi uliofanyika kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo hazikuwa na umiliki halali wa mali zao ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini;

Jedwali Na 4: Orodha ya Mashirika Yasio na Hati Miliki

Na	Jina la Shirika	Idadi ya Viwanja	Idadi ya Majengo
1	Mamlaka ya Bandari Tanzania	44	-
2	MWAUWASA	-	5
3	Chuo Kikuu Huria	8	7
4	COASCO	1	-
5	Chuo Kikuu cha Dodoma	2	-
6	TPDC	-	1
7	SIDO	19	-

Na	Jina la Shirika	Idadi ya Viwanja	Idadi ya Majengo
8	Shirika la Posta Tanzania	12	-
9	TAWIRI	-	1
10	BUWASA	-	22

6.4 Kushuka Kwa Uwezo wa kifedha na Mashirika ya BAKITA, MUWASA na TLSB

Katika ukaguzi wa kupima ufanisi wa kifedha wa BAKITA, nilibaini kwamba Baraza linajiendesha kwa hasara kwa miaka kadhaa kwa sababu ya kutopata fedha za kutosha kutoka Serikalini na kushuka kwa mapato ya ndani kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini;

Jedwali Na 5: Hali Mbaya ya Ufanisi Kifedha kwa BAKITA

Mwaka	2010	2011	2012
Malimbikizo ya Faida/Hasara	8,602,000	(37,194,000)	(110,425,000)
Matumizi Mengine	269,303,000	151,989,000	105,411,000
Mapato ya Ndani	84,800,000	68,978,000	54,723,000

Kwa mtazamo hapo juu, Baraza linaweza kushindwa kuendelea kujiendesha kama halitapata msaada wa kifedha kutoka Serikalini. Kwa upande mwingine, Baraza inabidi lichunguze sababu za kuendelea kushuka kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kila mwaka na kubuni mbinu mbadala za kuongeza vyanzo vya mapato.

Vivyo hivyo, nilibaini hali kama hii wakati wa ukaguzi wa MUWASA ambapo ufanisi wa Mamlaka kifedha kwa miaka mitatu hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 umeshuka. Mamlaka imekuwa na hasara endelevu, kushuka kwa mtaji halisi wa kujiendesha (Net Working Capital), madeni kutokusanywa, kuwepo madeni ya muda mrefu yasiyolipika na ongezeko la uvujaji wa maji na hasara kuongezeka. Kuongezeka mara kwa mara gharama za umeme ambazo haziendani na mapato yatokanayo na mauzo ya maji,

maunganisho mapya au mauzo ya maji yamekuwa mabaya zaidi. Katika ukaguzi wa mwaka husika, kuna tofauti kutokana na ukweli kwamba ingawa wateja wanaongezeka kutoka 8,168 hadi 9,155 ongezeko la asilimia 6, lakini mapato yatokanayo na kuuza maji yamepungua kwa Shilingi milioni 94.1 sawa na asilimia 7 na mtaji halisi wa kufanyia kazi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 ulikuwa ni pungufu kwa Shilingi milioni 44.6

Pia ukaguzi wa Bodi ya Huduma ya Maktaba Tanzania ilibainika kwamba mtaji wa kijiendesha wa Bodi unapungua. Madeni ya Muda mfupi (Current Liabilities) yaliongezeka kwa Shilingi milioni 193.6 ikilinganishwa na mwaka uliopita lakini rasilimali za muda mfupi (Current Assets) zilishuka kwa Shilingi milioni 69.4 ikiashiria tatizo la kifedha ambalo linapelekea Bodi kutoweza kulipa madeni yake ambayo yanaweza kusababisha uwepo/ustawi wa shirika kuyumba.

6.5 Ukadiriaji wa Madeni Chechefu (Provision for Doubtful debts) Bila Kufuata Utaratibu katika Shirika Hodhi la Mali za Umma (CHC) Kiasi cha Shilingi Bilioni 83.4

Ukaguzi wa madeni ambayo CHC iliyarithi kutoka PSRC ulibaini kwamba Shirika lilitoa madeni chechefu yanayofikia kiasi cha Shilingi bilioni 83.4 kutoka kwenye deni la Shilingi bilioni 98.1 ikiwa ni asilimia 85 ya jumla ya deni lote. Ukitazama asilimia ya makadirio ni wazi kwamba idara ya Ukusanyaji Madeni ikishirikiana na Wakala wa Ukusanyaji Madeni wameshindwa kuwajibika ipasavyo. Zaidi, imegundulika kuwa baadhi ya madeni yaliyofutwa ni yale yaliyotokana na riba ya madeni iliyokokotolewa kwa ajili ya malipo yaliyocheleweshwa ya ununuzi wa rasilimali au hisa. Katika ukaguzi hakuna ushahidi uliopatikana kuonyesha mawasiliano yeyote yaliyofanywa na wadeni kama wanakataa au wana malalamiko kuhusiana na kiasi cha riba waliyotozwa. Mbali na hilo, hakuna sera ya ufutaji madeni iliyopatikana kuthibitisha hatua zilizochukuliwa na Menejimenti ya CHC. Kiasi kikubwa cha ufutaji madeni bila

ya kufuata utaratibu rasmi unaweza kupunguza juhudi za ukusanyaji madeni na menejimenti inapaswa kuweka wazi mchanganuo ukiambatana na ushahidi wa kutosha wa ufutwaji wa madeni uliofanyika.

6.6 Mikopo Isiyolipika ya PSPF ya Kiasi cha Shilingi Bilioni 67.2

PSPF inatoa mikopo kwa Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine na mikopo hii imedhaminiwa kikamilifu kwa dhamana ya Serikali. Katika mapitio ya mwaka huu nilibaini kuwa mikopo isiyolipika kadha wa kadha ilitolewa kwa Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali na hakuna malipo yeyote yalifanywa kwa Mfuko katika kipindi chote cha mwaka. Hii inaweza kuharibu mtiririko wa fedha za Mfuko na matokeo yake kushindwa kulipa mafao yanapofikia wakati wa kulipwa. Menejimenti inapaswa kufuatilia kiasi cha madeni na kuhahakikisha kuwa yanakusanywa kutoka kwa waliokopeshwa. Madeni yasiyolipika yameonyeshwa katika jedwali hapa chini;

Jedwali Na 6: Mikopo Ambayo Hailipiki

Na	Jina la Mkopaji	Sekta	Salio (Tsh.)
1	HESLB	Taasisi ya Serikali	54,644,657,534
2	PCCB	Taasisi ya Serikali	6,678,150,000
3	Tan Power Resources	Taasisi isiyo ya Serikali	5,421,551,370
4	Kiwanda cha Madawa Tanzania	Taasisi isiyo ya Kiserikali	435,057,632
Jumla Kuu			**67,179,416,536**

6.7 Makubaliano ya Mkopo kwa Mifuko ya Pensheni na Chuo Kikuu cha Dodoma/Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mkataba wa Makubaliano ya kukopeshana fedha ni nyaraka muhimu katika kuweka masharti mbalimbali yanayohusiana na mkopo, kiwango cha riba na jinsi ya kurudisha mkopo. Makubaliano hayo yanapokosekana yanaweza kukasababisha

mifuko isiweze kulipwa fedha zake kama mgogoro utatokea.

Katika ukaguzi wa Mkataba wa Mkopo wa Mfuko, nimebaini baadhi ya madhaifu ya makubaliano ya mradi uliofadhiliwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na Serikali kama inavyoelezwa hapo chini;

(a) Mkataba wa Mkopo wa PSPF

Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF) umesaini mkataba na Serikali kupitia Wizara ya Elimu ya Juu na Mafunzo ya Ufundi kutoa fedha za kujenga Chuo Kikuu cha Elimu Dodoma. Zaidi ilibainika kwamba, kiini cha mkataba ni Mfuko kutoa fedha na kujenga Chuo kujumuisha mabweni, bwalo la chakula, vyumba vya mdahalo, madarasa, vyumba vya semina, majengo ya ofisi, maktaba, zahanati na majengo mengine kama ilivyodhihirishwa katika mkataba. Mapitio ya mkataba yalibaini mkanganyiko wa tafsiri ambao unahitaji kutatuliwa mapema. Kutokuwa na mkataba sahihi kunafanya kuwa na tafsiri mbalimbali ambazo matokeo yake ni hasara kwa Mfuko iwapo mgogoro utajitokeza. Mfuko unapaswa kushirikiana pamoja na Serikali na kuhakikisha mkataba wa mkopo unaandikwa vizuri na vifungu vyovyote ambavyo vinaweza kuleta utata virekebishwe.

(b) Mkataba wa Mkopo wa PPF

Katika ukaguzi nimebaini kuna mkopo wa muda mrefu ambao mfuko wa PPF umeshiriki kuchangia ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wenye jumla ya Shilingi bilioni 71 zilizokuwa zimewekezwa katika mradi kufikia tarehe 31 Disemba, 2011. Kutokana na mkataba, riba itaanza kujilimbikiza mara mradi utakapokamilika. Hata hivyo, nimebaini kwamba mkataba wa kutoa fedha kwa ajili ya mradi huu kati ya Mfuko na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania bado haujakamilika hadi ripoti hii inaandaliwa. Menejimenti ya PPF kupitia idara ya

uwekezaji inapaswa kuhakikisha kwamba mikataba yote iliyopo ya mkopo au miradi inatekelezwa kikamilifu.

6.8 Bodi ya Sukari Kutokuwa na Maamuzi Kwenye Nyumba Yake Anayoishi Waziri wa Zamani wa Kilimo, Hifadhi ya Chakula na Ushirika

Kila Mamlaka ina haki ya kutumia rasilimali zake inazozimiliki kwa ajili ya manufaa ya mamlaka husika. Katika ukaguzi wa Bodi ya Sukari Tanzania, nimebaini kwamba Bodi ina nyumba kwenye kiwanja Na 482 iliyopo katika Barabara ya Bray Masaki ambapo nyumba hiyo kwa muda mrefu anaishi Waziri wa zamani wa Kilimo, Hifadhi ya Chakula na Ushirika. Licha ya juhudi zilizofanywa na Bodi kumuandikia barua Katibu Mkuu Kiongozi kuomba kuimiliki tena nyumba hiyo, Waziri aliahidi kurudisha nyumba hiyo ifikapo Disemba, 2011, ila mpaka sasa hivi nyumba hiyo haijarudishwa kwenye Bodi. Waziri kuendelea kukaa katika nyumba hiyo ni kuinyima Bodi haki yake ya kutumia nyumba hiyo ili kujipatia mapato. Bodi inabidi iweke juhudi za zaidi za kufuatilia ili kuweza kurudisha nyumba ya shirika katika mamlaka ya Bodi.

6.9 Mali Zilizopo Chuo Kikuu cha Dodoma Hazikujumuishwa Katika Vitabu vya Hesabu vya Chuo Zenye Thamani ya Shilingi Bilioni 452.1.

Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na Mifuko ya Pensheni. Mifuko ya Pensheni ilikabidhi majengo hayo kwa Chuo kutokana na maelekezo ya Serikali. Hivyo, majengo yote yaliyokamilika na kazi inayoendelea kwa Vyuo Sita vya Chuo Kikuu cha Dodoma na mabweni ya wanafunzi yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania bilioni 452.1 thamani yake haijaingizwa katika vitabu vya hesabu vya Chuo. Zaidi ya hayo, tumebaini kwamba majengo mengi yalikuwa hayana bima tangu kipindi cha uangalizi kumalizika. Kwa sababu hiyo, Chuo kinaweza kupata hasara kubwa ya mali, mitambo na vifaa vyake iwapo kutatokea majanga kama vile moto.

6.10 Udhaifu Katika Malipo Yaliyofanywa kwa Waangalizi wa Mali Zinazosubiri Kubinafsishwa Shilingi za Kitanzania Milioni 523.5

Ili kuweza kuyadhibiti mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya kubinafsishwa inabidi kuwe na waangalizi/walinzi wa mali hizo. Ukaguzi uliofanyika mwaka huu umebaini kwamba CHC iliwalipa waangalizi sita kiasi cha Shilingi milioni 523.5. Hata hivyo, hakuna ripoti yeyote ya kifedha au maendeleo iliyopatikana kutoka kwa waangalizi hao au ofisa kutoka CHC anayewajibika kufuatilia utendaji wa waangalizi hao. Vilivile, katika kupitia ripoti ya tathmini na usimamizi nilibaini kwamba Shirika la Taifa la Usagishaji ni moja ya mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya kubinafsishwa ambalo linasimamiwa na CHC. Hata hivyo, hapakuwa na taarifa yeyote iliyotolewa kuonyesha kumbukumbu ya malipo, kumbukumbu ya mapato yatokanayo na shughuli za NMC. Ukaguzi ulibaini kwamba waangalizi hao hawafuatiliwi ili kuweza kujua kama fedha zinazolipwa kwao zinatumika kama ilivyo kusudiwa.

Waangalizi hawa wanapaswa kusimamiwa kwa karibu na kuhakikisha kuwa fedha wanazopelekewa wanaonyesha mchanganuo wa kazi husika. NMC ikiwa kama shirika ambalo limetengwa kwa ajili ya kubinafsishwa ni vizuri liangaliwe kwa karibu na waangalizi wake waweze kuingia mkataba na CHC, ambao utawafanya waweze kuonyesha mapato na matumizi kutoka NMC.

6.11 Usimamizi Hafifu Unaofanywa na CHC kwa Wakopaji wa Zamani wa NBC Shilingi za Kitanzania Milioni 630.733

Wakati wa kupitia kumbukumbu za mikopo ya waliokuwa wakopaji wa NBC wa Zamani, nilibaini kwamba kulikuwa na wateja wapya ambao hawakuwepo katika kumbukumbu za awali za mikopo ya CHC, lakini walikuwa wameorodheshwa kama wateja wapya. Wateja hao ni saba na akaunti zao zina jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 630.733 kama ilivyoonyeshwa katika jedwali hapa chini;

Jedwali Na 7: Wateja Wapya Ambao Hawapo Kwenye Kumbukumbu za Mikopo

Na	Jina la Mkopaji	Maelezo	Kiasi (Sh..)
1	Rashidi Mshalu	Akaunti Mpya	5,000,000.00
2	Andrea Ishengoma Makyai	Akaunti Mpya	457,383.90
3	C. K. Enterprises	Akaunti Mpya	39,994,865.00
4	H. N. Impex Port Ltd	Akaunti Mpya	17,238,689.00
5	Tanzania Tobacco Board	Akaunti Mpya	537,522,880.00
6	Fidel Emmanuel	Akaunti Mpya	1,363,312.10
7	Dor-Mohamed Issarahmat	Akaunti Mpya	29,155,971.65
	Jumla		**630,733,101.65**

Akaunti hizi za wateja wapya ambao walikuwa wanadaiwa na CHC lakini hawakuwa kwenye kumbukumbu za CHC za wadaiwa zilikuwa zimelipwa kufikia mwishoni mwa mwaka na hakuna deni lililobaki. Bila ya kuwapo na usimamizi madhubuti wa orodha ya wateja, kuna uwezekano wa salio la mkopo la hivi sasa kwa wakopaji wa NBC ya zamani kuwa siyo sahihi na la kuaminika.

6.12 Vifaa Ambavyo Havikupokelewa Bandarini kwa Muda Mrefu vya Shilingi Milioni 19.7

Wakati wa kuhakiki vifaa vya Bandari vilivyopo ghalani, nilibaini kwamba kuna bidhaa zilizokuwa kwenye mchakato wa kutolewa bandarini kwa muda mrefu kiasi cha Shilingi milioni 19.7. Bidhaa hizi zilikuwa ni spea za boti ya kufanya doria “Irimina Macha” ambavyo viliagizwa kupitia barua ya wazi ya mkopo (Open Letter of Credit) ya tarehe 23 Novemba, 2009. Barua ya mkopo ilikuwa kisheria halali hadi tarehe 26 Februari, 2010. Nilibaini kwamba mzigo uliotumwa ulipokelewa na Kampuni ya mizigo ya Swiss Port Tanzania Limited katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa

cha Julius Kambarage Nyerere na ndege namba ACP 060/5Y SAN ya tarehe 29 Mei, 2010, lakini yaligundulika kuwa mzigo uliotumwa umepotea katika mchakato wa kuuchukua ulipofaywa na Bandari. Zaidi, mapitio ya ukaguzi yalibaini kwamba upotevu hakuondolewa wala kuripotiwa katika vitabu vya mahesabu ya mwaka na Mamlaka husika. Hatua zinapaswa zichukuliwe kwa kuhakikisha kuwa mzigo au gharama zinarudishwa kutoka kwa "Cargo Handling Company" mapema iwezekanavyo na upotevu unapaswa uonyeshwe katika vitabu vya mahesabu vya Bandari.

6.13 Nyumba Inayotumiwa na NDC Kiwanja Na.2338 Iliyopo Mbezi Beach, Barabara ya Bagamoyo Haina Mkataba wa Pango

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kwamba Shirika halina mkataba wa pango na mpangaji wa sasa wa jingo. Messrs Vignan Education Foundation ambaye mkataba wake na Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) ulikwisha tangu mwezi wa Agosti 2011. Vignan Education Foundation alikataa kukubali masharti ya mkataba ulioandaliwa na NDC ambao pamoja na mambo mengine una kodi ya mwezi ya Shilingi milioni 60. Kodi ambayo ilikadiriwa na Mthamini (Valuer) aliyebobea. Menejimenti haikutoa maelezo ya kutosha kuhusiana na haki za Shirika za kumuondoa mpangaji katika jengo au kukusanya kodi iliyopendekezwa. Shirika lipo katika hatari ya kukosa kodi ambayo ingewezesha kuboresha hali ya kifedha ya Shirika. Menejimenti inapaswa kuchukua hatua za kumuondoa Vignan Education Foundation kutoka kwenye jengo au kutekeleza mkataba kama ulivyopendekezwa. Hii inapaswa kujumuisha marejesho ya riba ya kodi hadi tarehe ya kodi itakapokusanywa.

6.14 Kutokuwepo Kwa Orodha ya Makabidhiano ya Mali Kutoka Kwa Mamlaka ya Usambazaji Maji Kwenda Kwa KASHWASA

Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi ya Mji wa Kahama Shinyanga ilianzishwa ili kuendesha Mradi wa Kusambaza

Maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga ikijumuisha menejimenti ya miundo mbinu ya mpango wa usambazaji maji ambayo ni Mitambo na Vifaa vya Mamlaka. Katika ukaguzi, nilibaini kwamba ingawa mradi wa kusambaza maji umekabidhiwa kwa Mamlaka, mkataba wa Makubaliano (MoU) haukuonyesha orodha yenye maelezo ya kina ya baadhi ya rasilimali kuhusiana na gharama zake za awali ambazo bado hazijulikani. Nilibaini kwamba Menejimenti ya Mamlaka ilipokea barua kutoka Wizara ya Maji yenye kumbukumbu namba FC.449/599/02A/122 ya tarehe 21 Disemba, 2010 kupeleka rasimu ya Makubaliano ya Mkataba kwa ajili ya makabidhiano ya mradi wa kusambaza maji. Menejimenti ya KASHWASA iliiomba Wizara ya Maji kusaidia kupata maelezo ya rasilimali husika ikijumuisha thamani zake kupitia barua yenye kumbukumbu Na. AD.32/45/01B/44 ya tarehe 24 Agosti, 2012. Menejimenti kupitia barua tajwa iliiomba Wizara kumhusisha Mshauri ambaye angepitia rasilimali zote na kuzithaminisha. Hata hivyo, hadi muda wa ukaguzi, menejimenti ilikuwa bado haijapokea majibu yeyote kutoka Wizara ya Maji.

6.15 Udhaifu Katika Usimamizi wa Vifaa Ghalani

Kiwango cha pili aya ya 6(c) ya Viwango vya Kihasibu vya Kimataifa-IAS (2) inaeleza kuwa vifaa ghalani ni mali ambayo inategemewa kutumika katika mchakato wa uzalishaji au katika utoaji huduma. Vifaa ghalani vinawakilisha sehemu kubwa ya mali za shirika na hivyo zinahitaji kusimamiwa vyema ili kuondoa uwezekano wa upotevu, wizi au matumizi mabaya. Katika ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, udhaifu kadha wa kadha ulibainika kuhusiana na usimamizi wa vifaa ghalani. Nilibaini kwamba baadhi ya mashirika, yamekuwa yakiendesha zoezi la uhakiki mali za ghala bila ya kuwa na maelekezo ya uhakiki mali za ghala, kutoweka kumbukumbu za utoaji vifaa ghalani katika vitabu vya ghala au kadi za kuhifadhi kumbukumbu ghalani. Pia, tuliona baadhi ya vifaa vya ghala vilivyopangwa katika makabati na

havikuwa na kadi za kutunza mali ghalani. Ukaguzi ulibaini pia kuwa vibali vya kupokelea mali havitumiki wakati wa kupokea vifaa ghalani. Pia nilibaini kwamba kulikuwa na tofauti kati ya kumbukumbu ya ghala na uhalisia wa mali katika ghala na upangaji mbaya wa vifaa katika ghala. Kwa upande mwingine vifaa chakavu vilijumuishwa kwenye baadhi ya vitabu vya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama. Mifano hii ilibainika katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama vile Mamlaka ya Maji ya Mji wa Songea, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Bohari ya Madawa, Mamlaka ya Maji ya Mji wa Arusha na CAMARTEC.

6.16 Wadaiwa wa Muda Mrefu - Shilingi Bilioni 29. 9

Madeni ya kibiashara ni fedha zinazodaiwa na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa wateja na hurekodiwa kama mali kwenye taarifa ya biashara ya hali ya kifedha. Kwa upande mwingine madai ni sehemu ya mapato ya biashara, pamoja na mtiririko wa fedha na faida. Kwa mujibu wa uchambuzi wa kifedha, wastani wa kipindi cha ukusanyaji wa madeni kinachokubalika ni ndani au chini ya siku tisini (90) ili kuepuka kushikilia rasilimali za shirika mikononi mwa wadaiwa. Hata hivyo, ukaguzi wa madeni ya kibiashara katika taarifa ya kifedha ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ulibaini kwamba kuna madeni ya kibiashara ya muda mrefu ambayo yanayaweka Mashirika katika hatari ya hasara kwa sababu ya uwezekano wa kutolipwa, hivyo ni vyema ikaangaliwa upya ufutaji wa hasara za kibiashara na madeni mengineyo. Jedwali hapo chini linachanganua baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo zinadai madeni ya muda mrefu.

Jedwali Na 8: Madeni ya Biashara ya Muda Mrefu

Na	Jina la Shirika	Madeni (Sh.)	Kipindi cha Deni
1	TPA	3,423,242,460.00	2009 hadi 2012
2	TCRA	15,564,956,947.00	Zaidi ya Mwaka 1
3	NDC	104,600,794.00	Zaidi ya Mwaka 1

Na	Jina la Shirika	Madeni (Sh.)	Kipindi cha Deni
4	IPS	19,519,130.99	2003 hadi Des. 2011
5	IPS	42,805,099.00	Tangu mwaka 2010
6	DUCE	281,563,000.00	Zaidi ya Miaka 2
7	NIP	34,525,529.00	Zaidi ya Miaka 2
8	UDOM	154,854,160.00	Zaidi ya Miaka 2
9	KASHWASA	965,377,057.00	Zaidi ya mwaka 1
10	CBE-MWANZA	7,554,047.00	Tangu mwaka 2010
11	DAWASCO	8,163,108,795.00	Zaidi ya Miezi 6
12	IRUWASA	885,058,170.00	Zaidi ya mwaka 1
13	BUWASA	302,543,362.00	Zaidi ya miaka 4
Jumla		**29,949,708,550.99**	

Zaidi, ukaguzi ulibaini katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea (SOUWASA) kuwa ilifunga akaunti za wateja zikiwa na salio la madeni ya zaidi ya miaka mitano yenye kiasi cha Shilingi milioni 211.7 kwa mwaka husika. Hata hivyo, nilibaini kwamba hapakuwa na idhini ya Bodi ya Wakurugenzi ya kufuta madeni kama ambavyo Kanuni za Fedha za Mamlaka zinavyoelekeza. Naishauri Menejimenti iweze kuhakikisha kwamba madeni yote yaliyofutwa yanapata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi kama inavyoanishwa kwenye kanuni za fedha za Mamlaka. Kiasi kilichofutwa kinapaswa kupelekwa kwenye Bodi kwa ajili ya kupata idhini.

Jambo hili pia limejitokeza CHC ambapo jumla ya mkopo kiasi cha Shilingi milioni 98.6 ulikuwa umefutwa kutoka katika vitabu vya hesabu bila ya kupata kibali cha Bodi ya Wakurugenzi. Uongozi wa CHC unapaswa pia kufuata sera zilizowekwa na taratibu za kufuta madeni.

6.17 Kutolewa Kwa Madeni Chechefu Katika Kampuni ya Huduma ya Maji ya Jiji la Dar es Salaam Shilingi Bilioni 6.698

Ukaguzi uliofanywa katika madeni ya biashara ya DAWASA, ulibaini kwamba kulikuwa na ufutwaji wa madeni chechefu ya Shilingi bilioni 6.698 katika akaunti. Zaidi ya hayo,

ukaguzi ulionyesha kuwa kiasi hicho kilitolewa mahususi kwa Kampuni ya Huduma ya Maji ya Jiji (CWS) ambayo mkataba wake wa kukodishwa ulivunjwa Mei, 2005 kutokana na ufanisi mbovu wa mkataba wa ukodishwaji. Katika mkutano wa kumaliza ukaguzi wa Kampuni ya Huduma ya Maji ya Jiji (CWS) ilikubalika kuwa madeni yaliyosalia yanapaswa kulipwa na DAWASA kutokana na makusanyo ya madeni na hizo fedha zilipaswa kuwekwa katika akaunti maalum ya benki na malipo ya wadaiwa yalipaswa kulipwa kupitia akaunti hiyo. Kwa vile kiasi kilichokusanywa na kuwekwa katika akaunti hiyo hakikutosheleza kulipia madeni yaliyosalia, DAWASA ililipa madeni zaidi ya kiasi kilichokusanywa kwa Shilingi milioni 453.2 kwa matazamio kwamba Kampuni ya Huduma ya Maji ya Jiji italipa kiasi hicho. Ni takribani miaka saba tangu Kampuni ya Huduma ya Maji ya Jiji (CWS) ilipokoma na hakuna uwezekano wa kiasi hicho kurudishwa kutoka kwa mtoa huduma aliyesimamishwa. Matokeo yake rasilimali chechefu za DAWASA ziliandikwa kimakosa kwa kiasi cha ziada kilicholipwa kama deni.

6.18 Usimamizi Usioridhisha Katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania

Ukaguzi uliofanywa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania uligundua udhaifu mkubwa ambao unahitaji hatua za haraka kuchukuliwa kama ilivyoelezwa hapa chini;

Baadhi ya bakaa za benki zilizoonyeshwa kwenye taarifa za hesabu hazifanani na bakaa zilizopo kwenye taarifa ya benki. Katika kipindi cha ukaguzi wa mwaka husika, kulikuwa na tofauti kubwa katika taarifa za usuluhishi wa benki. Kwa hali hiyo, usahihi wa fedha taslimu Shilingi bilioni 7.118 zilizoonyeshwa kwenye taarifa za hesabu na ule wa fedha taslimu uliochukuliwa zaidi kwenye bakaa ya daftari la fedha taslimu ni Shilingi bilioni 1.534 unamashaka.

Vile vile, taarifa ya usuluhishi kwa akaunti tano kwa mwaka ulioishia tarehe 30, Juni, 2012 hazikuweza kupatikana kwa ajili ya uthibititisho wa bakaa zake kama vitabu vinanyoonyesha. Bila kutokuwepo kwa taarifa ya usuluhishi, usahihi wa bakaa za benki kama ilivyoonyeshwa kwenye vitabu vya hesabu ni wa mashaka.

Katika kupitia taarifa za mkaguzi wa ndani, nilibaini kwamba ripoti ya uchunguzi ya mkaguzi wa ndani ilikabidhiwa kwa Baraza la Uongozi wa Chuo ikitoa taarifa za ubadhilifu wa fedha za umma jumla ya Shilingi za kitanzania milioni 700.2. Ilielezwa kwamba kiasi hiki kimetokana na Shilingi milioni 219.9 ambazo zilipatikana kupitia Bodi ya Mikopo na Shilingi milioni 480.3 ambazo zilipatikana kupitia Msajili wa Hazina kwa njia ya malipo ya udanganyifu kwa watu wasiostahiki. Menejimenti ilieleza kwamba taratibu za kisheria kwa afisa mhusika tayari zilikwishaanza kuchukuliwa. Hata hivyo, ubadhilifu wa kifedha uliobainika haukuonyeshwa katika vitabu vya hesabu. Kulikuwa na udhaifu wa kiutendaji katika kuhakikisha kwamba fedha za Bodi ya Mikopo zilizolipwa kupitia Chuo zilipwe kwa wanafunzi stahiki. Inaonyesha hapakuwa na usimamizi wa kutosha katika mishahara iliyolipwa na Hazina kwa ajili ya wafanyakazi wa Chuo ambao ulitoa mwanya wa ubadhilifu kufanyika.

6.19 Kontena Mbili za Vitabu vya Maktaba Kutoka Shirika la Kimataifa la Kufadhili Watoto Hazijatolewa Bandari ya Dar es Salaam Tangu Mwaka 2009

Ukaguzi uliofanyika katika Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania ulibaini kwamba Bodi imeshindwa kutoa mzigo wa vitabu uliotumwa wenye thamani ya Shilingi milioni 147 tangu mwaka 2009.

Suala hili kuhusu hatima ya vitabu hivi linahitaji kutatuliwa ili vitabu hivyo viweze kupokelewa kwa ajili ya kusambazwa kwa wasomaji waliokusudiwa. Mahusiano kati ya wafadhili na TLSB yanahitaji kulindwa ili isije ikaharibu

uhusino na wafadhili ambao wanaweza kukataa kutoa msaada kipindi kingine. Vitabu vya Maktaba bado vipo bandarini vikisubiria malipo ya kodi na gharama za kuhifadhi mizigo bandarini. Kulingana na maelezo ya Menejimenti ya TLSB, kwa sasa gharama za kutoa mzigo zimefikia kiasi cha Shilingi za kitanzania milioni 147. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 haijulikani TLSB inadaiwa kiasi gani kwa kuwa hakuna uthibitisho uliotolewa kuonyesha kiasi halisi.

6.20 Kuongezeka Matukio ya Uwindaji Haramu Katika Hifadhi ya Taifa Tanzania

Katika kupitia taarifa zinazotokana na ripoti za robo mwaka za idara ya ulinzi imeonyesha kuwa vitendo vya uwindaji haramu hususani tembo vimeongezeka sana. Kutokana na taarifa zilizotolewa kutoka mbuga saba, jumla ya Tembo 110 waliuwawa katika kipindi cha mwaka 2011/2012. Ongezeko la uwindaji haramu hususani kwa Tembo unahatarisha hivyo, hatua madhubuti na za haraka zinahitajika kuchukuliwa ili kudhibiti kuwepo kwa tembo nchini hali hii kama inavyoonyeshwa hapa chini;

Jedwali Na 9: Matukio ya Ujangili TANAPA

Na	Mbuga	Robo ya 1	Robo ya 2	Robo ya 3	Robo ya 4	Jumla
1	Katavi	2	6	5	2	**15**
2	Ruaha	5	8	9	4	**26**
3	Mkomazi	3	0	0	2	**5**
4	Mikumi	1	3	5	1	**10**
5	L.Manyara	2	3	0	0	**5**
6	Serengeti	8	7	2	6	**23**
7	Tarangire	0	8	13	5	**26**
Total		**21**	**35**	**34**	**20**	**110**

Zaidi ya hayo ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya mbuga kama vile Katavi, Mikumi, Ziwa Manyara na Mkomazi doria

za askari pori hazifanyiki kama ilivyopangwa na mbuga zimeendelea kuwa na matukio ya ujangili na kiasi kikubwa cha tembo wameuwawa kwa mwaka husika kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini

Jedwali Na 10: Doria Zilizofanyika Katika Baadhi ya Hifadhi

Na	Jina la Mbuga	Doria Zilizofanywa Na Askari Pori (Ongezeko/Punguzo)%	Idadi Ya Matukio ya Uwindaji Haramu Yaliyoripotiwa	Idadi Ya Tembo Waliowindwa Na Kuuawa
1	Katavi	(43.2)	17	15
2	Mikumi	(29.9)	12	10
3	Ziwa Manyara	(57.5)	13	5
4	Mkomazi	(43.4)	1	5
Jumla				**35**

Mpango wa doria za askari pori katika kila mbuga hazikutekelezwa kama ilivyopangwa hivyo mbuga zilizotajwa hapo juu ziliendelea kuwa na upungufu katika doria na hivyo kusababisha matukio ya uwindaji haramu na idadi ya Tembo waliowindwa na kuuawa kuongezeka.

Ukaguzi pia ulibaini kwamba Mbuga ya Serengeti ilikuwa inafanya doria kwa kipindi chote cha mwaka lakini matukio ya uwindaji Tembo bado yalikuwa yanaongezeka jambo linaloashiria kuwa jitihada za ziada zinatakiwa zifanyike kwenye hifadhi ili kupunguza matukio hayo. Kwa upande mwingine, menejimenti ya TANAPA isiridhike na ripoti ya matukio machache ya ujangili katika Mbuga ya Mkomazi, doria za askari ziimarishwe katika mbuga ya Taifa ya Mkomazi ambayo ni mbuga yenye faru, wanyama waliohatarini kutoweka ambao wamewekwa chini ya hifadhi maalum hivyo kupunguza doria za askari katika pori hili kunaweza kuwafanya majangili kuivamia mbuga hii.

6.21 Leseni ya Biashara Iliyolipwa TCRA na TBC Kinyume na Mkataba Shilingi Milioni 618.300

Shirika la Utangazaji Tanzania na Star Communication Network Technologies Corporation Limited (Star) walisaini makubaliano ya uwekezaji mwezi Mei 2009.

Makubaliano yaliainisha kuwa asilimia 35 za mtaji wa mwanahisa zinazompa haki ya kupiga kura katika Star Media (Tanzania) Company imepewa Shirika la Utangazaji Tanzania na Star Communication Network Technologies Corporation Limited (Star) ina asilimia 65 ya hisa mara tu mgawanyo utakapokamilika. Hisa zilizoitishwa na kulipwa za Star Media (Tanzania) Company bado hazijagawanywa zikisubiri zoezi la uthamanishaji mali za Shirika la Utangazaji Tanzania na zile ambazo zimekwisha kutolewa na Star Communication Network Technologies Corporation Limited (Star) kulingana na vifungu vya sheria namba 3.2 na 3.3 vya makubaliano ya wanahisa.

Ukaguzi ulibaini kwamba Shilingi za Kitanzania milioni 618.3 zililipwa na TBC kwenye Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano ya Tanzania kwa niaba ya Star Media (Tanzania) Company katika mwaka wa fedha 2010 kwa ajili ya leseni ya biashara. Hata hivyo, Star Media (Tanzania) Company ina mkataba wa utendaji uliosainiwa na Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC) ambapo Star Media (Tanzania) Company imepewa msamaha wa kulipa leseni ya biashara kipindi cha miaka kumi na hii inaleta mgogoro wa kutambua kiasi kilichokwishalipwa na TBC kama malipo ya awali kwa TCRA kiwe kama Mtaji wa hisa za TBC katika Star Media (Tanzania) Company. Kiasi hiki hakijarudishwa na kuwa hasara kwa TBC. Hakuna kumbukumbu iliyoonyeshwa katika taarifa za hesabu kuhusiana na kiasi cha hasara ya hisa. Star Media (Tanzania) Company imepata hasara ya dola za Kimarekani 710,456 katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi. TBC haijapata thamani ya fedha kwa malipo iliyofanya kwa niaba ya Star Media (Tanzania) Company.

SURA YA SABA

USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU

7.0 Utangulizi

Usimamizi wa Rasilimali Watu ni mfumo wa uongozi katika taasisi unaohusika na kuajiri, kusimamia mafunzo, kufanya tathmini ya utendaji na kutoa motisha kwa watumishi na kusimamia upatikanaji wa maslahi ya watumishi. Pia ni kitengo kinachohusika na kutatua matatizo mbalimbali ya watumishi kupitia vyama mbalimbali vya watumishi.

Katika mazingira ambayo waajiriwa wanahaja na wanaruhusiwa kuwa na mazungumzo ya makubaliano, rasilimali watu huwa ni kiungo muhimu baina ya shirika husika na wawakilishi wa wafanyakazi (chama cha wafanyakazi).

Sura hii itazungumzia kwa muhtasari hoja zilizojitokeza katika ukaguzi wa Mashirika ya Umma ambazo zikipatiwa ufumbuzi zitaongeza ufanisi katika mashirika husika na Serikali kwa ujumla. Hoja zilizojitokeza zimeelezewa kama ifuatavyo:-

7.1 Ajira Zilizofanyika Bila Uwazi Katika Baadhi ya Mashirika

Katika utawala bora, uwazi katika ajira ni nyenzo muhimu katika kupata waajiriwa bora na wenye sifa zinazotakiwa. Bila kuwepo na uwazi na taratibu kufuatwa taasisi zinaweza kuajiri watumishi wasio na sifa. Katika ukaguzi nilioufanya, imebainika kuwa, pamoja na taasisi za umma kuwa na sheria na miongozo ya ajira, utekelezaji wake umekuwa ukikiukwa kama ilivyobainika kwa taasisi zifuatazo:

Katika ukaguzi wa Shirika la Magazeti Tanzania, nilibaini kuwa shirika lilimwajiri Mhasibu Mwandamizi katika ajira ya kudumu ya mafao badala ya ajira ya mkataba. Mhasibu aliajiriwa kupitia barua Na. FAM.32/772/06 ya tarehe 21/09/2006. Wakati anaajiriwa, alikuwa ametimiza umri

wa miaka 49, miezi 6 na siku sita. Utaratibu huu unakinzana na sehemu D.39 ya kanuni za kudumu za utumishi wa Umma ya mwaka 2009 na sehemu B.5.4.1, C 3.1 ya kanuni ya Watumishi ya Shirika la Magazeti. Utaratibu huu unaweza kupunguza ufanisi wa mwajiriwa na shirika kwa ujumla.

Pia Ilibainika kuwa Baraza la Biashara la Taifa lilimwajiri mfanyakazi mmoja katika ajira ya muda (temporary) kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2010 mpaka sasa. Ukaguzi ulibaini kuwa ajira yake ya muda umeshaongezwa muda mara tano. Ajira yake ya muda kwa mara ya mwisho uliishia tarehe 23 Machi, 2012 na anaendelea na kazi bila mkataba. Utaratibu huu ni kinyume na sheria ya ajira ya mwaka 2004 inayotaka ajira ya muda isizidi miezi mitatu.

7.2 Michango ya Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Kutowasilishwa kwa Wakati na Kukosa Stakabadhi za Kukiri Mapokezi

Moja ya kazi kubwa ya Mashirika ya Hifadhi za Jamii ni kusajili wanachama, kukusanya michango, kuwekeza fedha za michango, kulipa mafao ya kustaafu kwa wanachama na kulipa stahili nyingine za wanachama.

Katika ukaguzi nilibaini kuwa baadhi ya Mashirika hayawasilishi michango ya watumishi na Waajiri wao kwenye Mashirika ya Hifadhi ya Jamii kwa wakati kwa mujibu wa sheria kama inavyoonyeshwa hapo chini;

Ukaguzi wa Chuo Kikuu Huria ulibaini kuwa chuo hakijawasilisha michango yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.481 kwa mfuko husika. Mapungufu kama haya yalibainika pia katika ukaguzi uliofanyika Mamlaka ya Maji Mtwara, TEMDO, Mamlaka ya Maji Safi Dar es Salaam, Chuo cha Elimu ya Watu Wazima, CARMATEC, Mamlaka ya Maji Safi Singida na Mamlaka ya Udhibiti wa Hisa na Mitaji.

Kwa mujibu wa Waraka wa Hazina Na.C/BA 54/ 328/01/15 wa tarehe 19 Julai, 2011, Hazina ilizijulisha taasisi zote za umma kuwa jukumu la makato yote ya michango ya watumishi wa umma yatakatwa na kupelekwa moja kwa moja kwenye mifuko ya Hifadhi na Hazina. Ukaguzi ulibaini kuwa kwa michango iliyokatwa moja kwa moja na Hazina Mashirika hayakuwa na stakabadhi za uthibitisho kuwa fedha za watumishi wake zilipelekwa kwenye mifuko husika na Hazina.

Mapungufu hayo pia yalibainika katika ukaguzi uliofanyika Chuo Kikuu Moshi, Bodi ya Korosho Tanzania, Chuo Kikuu Huria, Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Chuo cha Wanyama Pori na Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam. Bila ya kuwa na Taarifa/uthibitisho unaoonyesha uwasilishwaji wa michango ya makato ya mwajiri kwenye mifuko ya Jamii ambayo umefanywa na Hazina, ni vigumu kuthibitisha kuwa michango hiyo ilitumwa na Hazina.

7.3 Upimaji wa Utendaji Kazi wa Wafanyakazi

Upimaji wa utendaji kazi ni mpango unaohusisha kujenga na kuendeleza makubaliano kati ya meneja na mtumishi ili kusaidia kupima utendaji wa wafanyakazi. Ili kupima utendaji kazi wa mtumishi, meneja huweka malengo kwa mtumishi ambayo katika kipindi husika mtumishi huyo anatakiwa kuyafikia. Mwisho au katikati ya mwaka meneja hukaa tena na mtumishi na kupima kama mtumishi amefikia malengo aliyowekewa. Ni vizuri na rahisi zaidi kupima utendaji mara kwa mara kuliko kusuburi mwisho wa mwaka.

Kutokana na kupima utendaji kazi wa watumishi, Menejimenti za Mashirika zitapata vigezo sahihi vya kumzawadia mfanyakazi kama kumpandisha cheo, kuongeza mshahara, kugundua mapungufu ya mtumishi husika na kuweka mpango wa kumsaidia.

Ukaguzi uliofanyika ulibaini kuwa, baadhi ya Mashirika ya Umma hayafanyi upimaji wa utendaji kazi kwa wafanyakazi wao. Kutokufanya upimaji wa utendaji kunaweza kupunguza ufanisi kwa wafanyakazi wenye juhudi ya kazi, na vilie vile waajiri hawawezi kujua vigezo vya kutumia katika kupandisha wafanyakazi vyeo na kuongeza mikataba kwa wale wenye ajira za mkataba. Hii ilithibitishwa na ukaguzi uliofanyika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro, Shirika Hodhi la Rasilimali za Mashirika ya Umma, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza, Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa, Shirika la Mafuta Tanzania, Shirika la Magazeti Tanzania, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi, Bodi ya Korosho Tanzania, Tume ya Sayansi na Teknolojia, Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Baraza la Taifa la Biashara Tanzania, Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma na Bodi ya Pamba Tanzania.

7.4 Majalada ya Watumishi wa Mashirika Kukosekana Kumbukumbu Muhimu

Kumbukumbu sahihi katika jalada la mtumishi husaidia kurahisisha kufanya maamuzi mbalimbali ya kiofisi kama kupandisha cheo, mafunzo, kuwajibisha na kupata taarifa mbalimbali za mtumishi.

Ukaguzi uliofanyika uligundua kuwa baadhi ya mashirika hayatunzi vizuri majalada. Majalada yalionekana kukosa kumbukumbu sahihi za watumishi kama barua za ajira, barua za kuthibitishwa kazini na vyeti vya shule. Mapungufu haya yalibainika kwenye kaguzi zilizofanyika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Moshi, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kigoma, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Tume ya Sayansi na Teknolojia. Mashirika yanaweza kupata ugumu wa kufanya maamuzi kuhusu

mtumishi kama hayatakuwa na kumbukumbu sahihi za mtumishi.

7.5 Upungufu wa Wafanyakazi Katika Baadhi ya Mashirika

Upungufu wa watumishi kwenye taasisi unaweza usionyeshe athari zozote katika muda mfupi. Hata hivyo, tatizo hili lisipopatiwa ufumbuzi mapema athari zake zinaweza kuzorotesha utendaji wa taasisi husika.Ukaguzi uliofanyika ulionyesha kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma yana nafasi muhimu za kiutendaji ambazo ziko wazi kwa muda mrefu sasa. Mamlaka ya Uendelezaji wa Mji Mkuu Dodoma ina nafasi muhimu 14 ambazo ziko wazi ikiwemo ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka.

Kutokana na muundo wa utumishi wa Bandari Kitengo cha usimamizi wa mifumo katika Mamlaka ya Bandari kilionyesha kuwa na nafasi 3 ambazo ziko wazi na hakuna jitihada zilizoonyeshwa na mamlaka kujaza nafasi hizo. Mamlaka inaweza kukumbwa na athari za kiutendaji kama hatua stahiki hazitachukuliwa mapema.

Taasisi ya NHC/PPF ilionekana kuwa na mhasibu mmoja tu ambaye anafanya kazi zote kama kutayarisha hesabu, kufanya usuluhishi wa akaunti, kuandika hundi, kupeleka pesa benki na kuchukua pesa benki. Kazi zote za kihasibu zilikamilishwa na mtu mmoja kinyume na utaratibu wa mgawanyo wa kazi wa kihasibu.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa, kitengo cha mauzo Bohari ya Madawa tawi la Mbeya kina upungufu wa watumishi. Kulingana na muundo wa kitengo cha mauzo Bohari ya Madawa Kanda ya Mbeya kilitakiwa kuwa na watumishi watatu. Ukaguzi ulibaini kuwa kanda ya Mbeya ina mtumishi mmoja tu anayefanya kazi Mikoa ya Katavi, Rukwa na Mbeya. Ni wazi kuwa ufanisi wa kazi wa mtumishi huyu utakuwa wa mashaka.

Ukaguzi uliofanyika kwenye Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Rufiji ulibaini kuwa Mamlaka haijaajiri Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi wa Fedha kwa muda mrefu sasa. Ukosefu wa watendaji Wakuu wa Shirika kama hawa unaweza kuleta athari za kiutendaji na kuzorotesha utekelezaji wa mipango ya shirika.

7.6 Mafunzo na Uendelezaji Wafanyakazi

Ili kuongeza ufanisi wa watumishi, taasisi inapaswa kuandaa mpango wa mafunzo. Mafunzo yatasaidia kuongeza maarifa na kumwezesha mfanyakazi kuwa na ubunifu katika utendaji wake. Ukaguzi uliofanyika ulibaini kuwa baadhi ya mashirika hayana mpango wa mafunzo kwa ajili ya watumishi. Bila kuwa na mpango wa mafunzo, utaratibu mzima wa mafunzo utagubikwa na upendeleo na hautazingatia mahitaji ya mafunzo kwa kila mtumishi. Mapungufu haya yalibainika katika ukaguzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza na Bodi ya Korosho Tanzania. Vile vile, Sera ya mafunzo haikuawa imeandaliwa.

7.7 Upungufu wa Manahodha wa Meli Shirika la Bandari

Wakati wa ukaguzi wa Mamlaka ya Bandari, timu ya wakaguzi ilitembelea mnara wa kuongozea meli ili kuangalia kwa ujumla utendaji katika kitengo hiki muhimu cha Bandari. Timu ya wakaguzi ilibaini kuwa kuna upungufu wa manahodha wa meli na ilielezwa kuwa Mamlaka ina manahodha saba ambao wote wamefikisha umri wa kustaafu. Uongozi wa Bandari haukuweza kuwasilisha mpango wa namna mamlaka ilivyojipanga kutatua tatizo hili. Bila kuchukua hatua za haraka, Mamlaka ya Bandari itakuwa na tatizo kubwa la manahodha wa meli na shughuli za Bandari zinaweza zisitekelezwe kwa ufanisi. Ifuatayo ni orodha ya Manahodha saba wa Mamlaka ya Bandari ambao wamefikisha umri wa kustaafu kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali Na 11: Manahodha Waliopo na Muda wao wa Kustaafu

Na	Jina	Daraja	Kituo cha kazi	Tarehe ya kustaafu
1.	Mwingamo Abdallah	1	Dar es Salaam	Disemba 2012
2.	Fredy Mwampeta	1	Dar es Salaam	Juni 2012
3.	Regnad Senyangwa	1	Dar es Salaam	Oktoba 2012
4.	Paul Paul	1	Dar es Salaam	Disemba 2012
5.	Kasoso Ramadhani	1	Tanga	Disemba 2012
6.	Henry Matily	1	Tanga	Machi 2012
7.	Hussein Kasigwa	1	Mtwara	Disemba 2012

Kazi ya kutoa na kuingiza meli bandarini hufanywa na Manahodha wa Bandari wenye daraja la I au la II. Bila kuwa na huduma ya manahodha hao utendaji katika bandari hauwezi kuendelea. Hata hivyo, sikuweza kupata hatua zozote zilizochukuliwa ili kujaza nafasi hizo zinazoweza kuweka shirika katika hali hatarishi.

7.8 Kutokuwepo Mpango wa Kukasimu Madaraka Katika Shirika la Mafuta Tanzania

Ukaguzi wa mpango mkakati wa Rasilimali watu wa Shirika ulibaini kuwa ajira za Shirika zilisitishwa na Serikali tangu mwaka 2005. Pamoja na serikali kusitisha ajira, Shirika limeonekana kutokuwa na mpango wa kukasimu madaraka endapo waliopo madarakani watastaafu. Kwa kuwa Serikali imejikita katika uzalishaji wa gesi Mtwara na Shirika linaonekana kutokuwa na mpango mkakati wa kuandaa watumishi wapya wakusimamia sekta hii, ni wazi kuwa shirika halitaweza kusimamia vizuri sekta ya gesi kwa siku za baadae kwa sababu ya kutokuwa na utaratibu wa kuajiri ili, pindi wafanyakazi wenye umri wa kustaafu

watakapoondoka wawe wameacha ujuzi wao kwa wafanyakazi wengine. Shirika lifanye juhudi za kupata mpango wa kukasimiana madaraka ili kuepuka mikwamo ya mipango ya shirika na nchi kwa ujumla.

7.9 Ukiukwaji wa Waraka wa Serikali Kutolipa Pensheni kwa Watumishi wa Mikataba katika Shirika la Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii

Kulingana na waraka wa Serikali Na. C/AC.45/257/01/Temp./26 wa tarehe 1 Disemba, 2009 unataka watumishi wa mikataba kulipwa kiinua mgongo baada ya mkataba na wasilipwe mafao ya pensheni kama watumishi wa ajira za kudumu. Wafanyakazi wa ajira ya kudumu wanatakiwa kulipwa mafao ya Pensheni inayotokana na asilimia fulani iliyopo kisheria na sio mafao ya mkataba.

Katika ukaguzi wa Shirika la Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ilibainika kuwa Shirika liliwalipa Shilingi za Kitanzania milioni 13.062 kwa watumishi wake wa mkataba na Shilingi za kitanzania bilioni 1.965 watumishi wa ajira ya kudumu kama malipo ya mkataba (gratuity) ambapo wafanyakazi wa Pensheni wanatakiwa kulipwa mafao ya kiinua mgongo peke yake. Ni wazi kuwa shirika limekiuka waraka wa serikali na limejiingiza kwenye matumizi yasiyokuwa ya lazima kwa kuongeza matumizi yasiyoleta tija kwa Shirika.

7.10 Mapungufu ya Kiutendaji Yaliyobainika Chuo Cha Elimu ya Biashara

(a) Kutokuwepo kwa Usuluhishi wa Idadi ya Wanafunzi Chuoni

Ukaguzi ulibaini kuwa Chuo hakina taarifa sahihi ya idadi ya wanafunzi wanaosoma chuoni hapo. Taarifa za Msajili wa Chuo na Taarifa za Idara ya fedha kuhusu wanafunzi waliopo chuoni kwa miaka miwili tangu 2009/2010 na 2010/2011 zinakinzana. Zaidi ya hayo msajili wa chuo alionyesha kuwa fedha zilizopokelewa kwa miaka miwili ni

Shilingi za Kitanzania bilioni 9 wakati taarifa ya idara ya fedha ilionyesha Shilingi za Kitanzania bilioni 11.

(b) Mikataba ya Ajira Iliyotolewa Bila Kufuata Utaratibu kwa Watumishi Waliostaafu

Mkurugenzi wa Raslimali Watu wa Chuo cha Biashara alikuwa ametimiza umri wa kustaafu tarehe 24 Novemba, 2008 kwa mujibu wa kipengele Na.F 42 cha Kanuni za Kudumu za Utumishi za mwaka 2009. Tarehe 18 Julai, 2008 Mkuu wa Chuo cha Biashara alimuandikia barua Msajili wa Hazina akimuomba amuongezee mkataba wa miaka miwili Mkurugenzi wa Raslimali Watu. Msajili wa Hazina hakujibu barua hiyo na Mkurugenzi wa Rasilimali watu aliendelea na nafasi yake bila kuwa na kibali kutoka kwa Msajili wa Hazina.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa kuna watumishi watatu waliokuwa wamefikisha umri wa miaka sitini na wanatakiwa kustaafu lakini waliendelea kufanya kazi na kupata mshahara. Watumishi hao walikaa miaka miwili hadi mitano wakiendelea kupata mishahara hadi mwezi Novemba 2010. Watumishi hawa walizidisha muda wa ajira zao bila kuwa na kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

(c) Matumizi Mabaya ya Mishahara Ambayo Haikuchukuliwa-Shilingi Milioni 349

Chuo cha Biashara kiliendelea kupokea kiasi cha Shilingi milioni 244 ikiwa ni mishahara ya watumishi kumi ambao walikua wamestaafu, Shilingi milioni 104 ikiwa ni kutokana na watumishi walio staafu na Shilingi milioni 1 ikiwa ni kwa ajili ya mtumishi mmoja aliyefariki. Ukaguzi ulibaini kuwa Chuo kilitumia fedha hizo Kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya chuo ambayo hayakutakiwa kufanyika kwa kutumia fedha hizi kutoka Hazina.

(d) Usimamizi Mbovu wa Posho za Kufundishia za Wahadhiri na Wakufunzi

Wakati wa ukaguzi, Ilibainika kuwa uongozi wa chuo umeshindwa kusimamia vizuri posho za kufundishia za wahadhiri na wakufunzi. Wakuu wa idara hawasimamii vizuri kuhakikisha kuwa wahadhiri na wakufunzi wanaingia madarasani kwa wakati na kufundisha. Kutokana na usimamizi mbovu Chuo kililipa fedha kiasi cha Shilingi milioni 74 zaidi ya bajeti ya Shilingi za Kitanzania milioni 300. Pia, Chuo kiliwalipa wakufunzi kiasi cha Shilingi milioni 147 kuanzia tarehe 1 Novemba ,2011 mpaka tarehe 30 Juni, 2012 bila ya kuwa na mikataba.

SURA YA NANE

UTAWALA BORA

8.0 Utangulizi

Utawala bora unahusu mfumo wa udhibiti, majukumu pamoja na mahusiano kati ya wafanyakazi, bodi za wakurugenzi, wamiliki pamoja na wadau wengine, ikiwa ni pamoja na majukumu ya shirika husika. Utawala bora ni mfumo wa kisheria ambao unaweka taratibu ambazo zinaongoza shirika ambazo msingi wake mkuu ni muundo wa uthibiti wa ndani na nje wenye nia ya kusimamia utawala wa shirika na wakurugenzi ili kuboresha uwajibikaji na kudhibiti uwezekano wa ubadhilifu. Nia kuu ya dhima ya utawala bora ni kuhakikisha uwajibikaji wa kila mtu katika shirika ili kuweza kukamilisha malengo ya uanzishwaji wa shirika. Mihimili mikuu ya utawala bora wa shirika ni pamoja na Ukaguzi wa ndani, Bodi ya wakurugenzi ikijumuisha kamati ya ukaguzi, utawala pamoja na wakaguzi wa nje.

Sura hii inaeleza maswala mbalimbali yaliyomo katika taarifa za ukaguzi zilizotolewa kwa mashirika ya umma katika vipindi vinavyoishia tarehe 30 Septemba, 2011, 31 Disemba, 2011 na 30 Juni, 2012.

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, yamekuwepo mapendekezo mbalimbali yanayoelekeza namna ya kuboresha utawala bora katika mashirika na kutolewa mapendekezo yanayolenga kutatua matatizo yaliyoainishwa. Baadhi ya mambo yaliyohojiwa yalifanyiwa kazi na mashirika husika na ama yametekelezwa au bado yanaendelea na utekelezaji. Baadhi ya mambo yaliyomo katika ripoti zilizotangulia ni pamoja na: Kutokuwepo mwongozo wa shughuli za Bodi za Wakurugenzi, Wabunge na Wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi kushiriki katika shughuli za kila siku za uendeshaji wa mashirika, kuingiliwa uhuru wa maamuzi ya bodi ya wakurugenzi katika

kusimamia shughuli za mashirika ya umma, mapungufu katika utendaji wa bodi za wakurugenzi katika maeneo ya utaalam wa wajumbe wa bodi, mpangilio wa vikao vya bodi na uwajibikaji wa bodi katika maswala ya usimamizi wa fedha na utoaji wa taarifa. Kwa upande mwingine, ripoti zimeonyesha kuwa hapakuwa na mwongozo juu ya uundaji wa kamati ndogo za bodi zinazoshughulikia ukaguzi na mkataba wa majukumu ya kamati hizo. Pia, baadhi ya kamati hizo hazikuwa na mtaalam wa maswala ya fedha kama ilivyoelekezwa katika kamati za uundaji wa kamati kama hizo. Katika baadhi ya mashirika, baadhi ya Idara za Ukaguzi wa ndani hazikuwa na idadi ya watumishi wa kutosha na miundo madhubuti ya utoaji wa ripoti, maandalizi yasiyoridhisha ya mpango kazi wa idara ya ukaguzi wa ndani, kutokagua maeneo ya kutosha, na kwa baadhi ya mashirika idara ya ukaguzi wa ndani inajihusisha na uhakiki wa nyaraka za malipo kabla ya kuandikwa hati ya malipo. Pia, nilibaini kutofuatwa kwa mwongozo juu ya malipo ya ada kwa wakurugenzi na upelekaji wa asilimia kumi (10%) kwenda Hazina na jingine ni lile la kuanzishwa kwa ofisi ya Msajili wa Hazina inayojitegemea.
Nimetambua uwepo wa juhudi za serikali katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti zilizotangulia. Hata hivyo, kuna mapendekezo mengi kwa mujibu wa majibu rasmi ya serikali kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2011 kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) yanayoonyeshwa kuwa, yametekelezwa ingawaje yamejitokeza tena katika Ukaguzi wa mwaka huu katika baadhi ya Mashirika ya Umma. Ninapenda kusisitiza utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo katika ripoti zilizotangulia, na kuishauri serikali kuongeza juhudi katika kutekeleza mapendekezo ambayo bado hayajatekelezwa.

8.1 Bodi ya Wakurugenzi

Bodi ya wakurugenzi ni chombo ambacho kimeteuliwa au wajumbe kuteuliwa ili kufanya kazi ya uangalizi na kutekeleza shughuli za shirika. Kazi za bodi zinatokana na nguvu, majukumu na uwajibikaji ambao bodi imekasimiwa

na wamiliki wa shirika. Zipo sheria na kanuni zinazoelekeza idadi ya wajumbe kwa kila bodi, utaratibu wa uteuzi na idadi ya mikutano ya bodi za wakurugenzi kwa mwaka.

Bodi ya wakurugenzi wa shirika ni chombo muhimu kwa uwepo na ustawi wa shirika. Katika ukaguzi wa mwaka huu, kuna mapungufu ambayo yamebainika katika utendaji wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kama inavyoonekana hapa chini ;

8.1.1 Mapitio ya Malengo ya Shirika kwa Mujibu ya Madhumuni ya Uanzishaji wa Shirika

Madhumuni ya uwepo wa shirika husika yanajidhihirisha katika mipango ambayo shirika limejiwekea na ambayo inaonekana katika maamuzi ya kimkakati yanayofanywa. Mipango mingi inayofanywa huonyesha muda wa utekelezaji wake na namna ambavyo mafanikio yake yatapimwa. Wakati wa kupitia mashirika ili kuona ambavyo mashirika yameweza kukamilisha mipango yake nimebaini kuwepo kwa mafanikio madogo katika kufanikisha mipango ya mashirika kutokana na upungufu wa mitaji. Mfano mmojawapo wa shirika ambalo halikuweza kukamilisha mipango yake kutokana upungufu wa fedha ni Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro.

8.1.2 Kutozingatia Idadi ya Wajumbe wa Bodi kwa Mujibu wa Sheria ya Kuanzishwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Majini na Nchi Kavu (SUMATRA)

Waziri mwenye dhamana ya usafiri anahusika katika uteuzi wa wajumbe wa Bodi na Mkurugenzi Mkuu baada ya kupokea mapendekezo kutoka kamati ya uteuzi. Mwenyekiti wa Bodi anateuliwa na Rais baada ya kupokea mapendekezo ya Waziri. Sehemu ya 7 kifungu kidogo cha 1 cha sheria iliyoanzisha SUMATRA kinatamka kuwa Bodi ya Wakurugenzi itaundwa na wajumbe 7 kama ifuatavyo: Mwenyekiti (ambaye atakuwa si mtendaji), wajumbe watano wa kawaida pamoja na Mkurugenzi Mkuu. Kinyume na matakwa ya sheria, bodi ya SUMATRA ina wajumbe

wanne, na mwenyekiti aliteuliwa kutoka katika wajumbe na Mkurugenzi Mkuu aliyepo anakaimu nafasi hiyo tangu Aprili, 2011. Kwa kuwepo Bodi kama hii ambayo haijaundwa kama inavyotakiwa kisheria inaathiri maamuzi ya bodi ya wakurugenzi na wakati mwingine kuwa vigumu kufanya mikutano kutokana na kutokamilika kwa idadi inayotosheleza kufanya vikao hasa pale mjumbe mmojawapo akiwa na udhulu.

8.1.3 Wajumbe wa Bodi Kushiriki Katika Shughuli za Kiutendaji

Ili wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi waweze kuwa na ufanisi katika kufanya kazi ya usimamizi wa shirika na kulielekeza vizuri, Bodi ya Wakurugenzi haina budi kujitenga na shughuli za kila siku za uendeshaji wa shirika. Katika Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) , Mwenyekiti wa Bodi anajihusisha na shughuli za kiutendaji kinyume na matakwa ya kanuni za utawala bora katika makampuni na Waraka wa Ikulu wenye Na. SHC/B.40/6/21 wa tarehe 28 Machi, 1994 aya ya 3 na ya 5. Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2011, Mwenyekiti alilipwa fedha sawa na lita 100 za mafuta kila juma ikiwa ni posho ya mafuta, asilimia 40 ya fedha hizo alilipwa kama gharama za matengenezo ya gari na alilipwa posho ya simu ya Shilingi laki tano (500,000) kila mwezi. Mwenyekiti pia alisafiri nje ya nchi pamoja na watendaji wa shirika. Kumhusisha mwenyekiti katika shughuli za kila siku za shirika kunapunguza uhuru wa Bodi na uwajibikaji wake.

Katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, nimekuta wajumbe wa Bodi wakienda mafunzo nje ya nchi kwa gharama za shirika, kuhudhuria maonyesho ya kimataifa na safari za kujifunza kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania 770, 770,405. Shughuli hizi zilizofanywa na wajumbe wa Bodi zilitakiwa kufanywa na watumishi wa Mamlaka. Pia, wakurugenzi walihudhuria mafunzo ya kadi za kisasa (smart cards) kwa utaratibu uleule. Kwa kufanya hivyo, ikitokea menejimenti wakashindwa kutimiza malengo waliyopewa na Bodi ya Wakurugenzi, hakutakuwa na mamlaka ya

kuihoji menejimenti kuhusu kushindwa kutimiza wajibu wao.

8.1.4 Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika Zina Wajumbe Ambao ni Wabunge Kinyume na Kanuni za Utawala Bora

Wabunge wanalo jukumu la kuangalia, kusimamia na kuhoji utendaji wa Mashirika ya Umma kwa ujumla. Katika ripoti zangu zilizotangulia nilihoji kuhusu uwepo wa baadhi ya wabunge katika Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma kinyume na kanuni za Utawala Bora. Mwaka huu pia, bado tatizo hilo limeendelea kuwepo kwani wabunge wameendelea kuteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma. Mifano ambapo tatizo la Bodi zenye wajumbe ambao ni wabunge limeonekana ni pamoja na STAMICO yenye wajumbe wanne (4) ambao ni wabunge. Uteuzi wa wabunge kuwa wajumbe wa bodi za mashirika husababisha mgongano wa kimaslahi kwa kuwa wabunge wanayo kazi muhimu ya uangalizi wa mashirika kwa ujumla ili kuhakikisha uwajibikaji kwenye rasilimali za umma unakuwepo. Hali hii ikitokea, husababisha mgongano wa kimaslahi kwa kuwa wabunge sasa hulazimika kufanya kazi ya utawala, uangalizi, usimamizi na kuhoji utendaji wa mashirika kwa ujumla. Mifano mingine ya mashirika ambayo yana wabunge katika Bodi zake za Wakurugenzi ni pamoja na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) ambao waliteuliwa tarehe 23 Machi, 2012, Kituo Cha Mikutano Cha Kimataifa Arusha (AICC), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, (NCAA), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Chuo cha Diplomasia, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi na Bodi ya Korosho.

8.1.5 Uteuzi wa Msajili wa Hazina Kuwa Mjumbe wa Bodi Katika Mashirika ya Umma

Msajili wa Hazina anayo kazi muhimu ya kuangalia na kusimamia maslahi ya serikali katika mashirika ya umma yote ambayo serikali inamiliki hisa. Ili kufanya kazi zake kwa ufanisi, Msajili wa Hazina anatakiwa kuwa na uhuru kutoka katika mashirika yanayomilikiwa na serikali.

Katika vipindi vya kaguzi zilizoishia tarehe 30 Septemba, 2011, 31 Disemba, 2011 na 30 Juni, 2012 nilibaini kuwa Msajili wa Hazina na baadhi ya watumishi chini yake, wamekuwepo katika Bodi za Mashirika ya Umma kinyume na matakwa ya Kifungu cha 34 kifungu kidogo cha 3a (3) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Powers and Functions) (Cap.370) kinachomtaka Msajili wa Hazina, yeye binafsi au kwa mujibu wa ofisi yake, kutoteuliwa kuwa Mjumbe au Mwenyekiti wa shirika lolote ambalo serikali inamiliki hisa. Mfano wa Mashirika ambayo Msajili wa Hazina ni mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ni pamoja na Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC), Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF), na Benki ya Rasilimali (TIB).

8.1.6 Kutokuwepo Mwongozo Unaoelekeza Maagizo ya Wizara Yanayotakiwa Kutolewa kwa Mashirika

Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) ni shirika huru ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa sheria ya Bunge yaani Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, CAP 364 ya mwaka 1962 na kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 1992. Jukumu kubwa la msingi likiwa ni kutangaza na kuendeleza utalii Tanzania. Shirika hili likiwa shirika huru, lina mamlaka ya kujiendesha lenyewe chini ya usimamizi na maelekezo ya Bodi ya Wakurugenzi bila kuingiliwa. Nimebaini kuwepo kwa shughuli zinazoashiria Wizara ya Mali Asili na Utalii kuingilia utendaji wa shughuli za Bodi ya Utalii. Kwa mfano Wizara ilihamisha jumla ya Shilingi milioni 771.2 (2011: Shilingi Milioni 591) kwenda Bodi ya Utalii kwa shughuli ambazo siyo za Bodi ya Utalii. Fedha hizi zilichukuliwa tena na kurudishwa Wizarani kwa maagizo ya Wizara. Jambo la kushangaza zaidi ni pale ambapo jumla ya Shilingi milioni 416.1 zilichukuliwa kutoka Bodi ya Utalii na mfanyakazi wa Wizara ya Mali Asili na Utalii na Shilingi milioni 355.096 zililipwa moja kwa moja kwa idara nyingine au watoa huduma wengine kama Wizara ilivyoelekeza. Muingiliano kama huu katika shughuli za kiutendaji unakwamisha uwajibikaji katika shughuli za Bodi ya Utalii.

Wizara ya Mali Asili na Utalii pia, ilitoa maagizo mbalimbali ili yatekelezwe na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Baadhi ya maagizo ya kiutekelezaji yaliyotolewa kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ni: Kutoa mchango wa Shilingi milioni 34.96 kwa Wizara ya Mali Asili na Utalii ikiwa ni kwa ajili ya mshahara wa miezi minne (4) wa Afisa Utalii ambaye kituo chake cha kazi ni Japan, Ngorongoro kulipa gharama za wabunge walioshiriki maonyesho ya utalii ya kimataifa. Zaidi ya hapo, Wizara ilielekeza kuwa Mbunge mmoja awe akilipiwa gharama za kuhudhuria maonyesho kama hayo kwa siku za mbele japo uongozi wa Ngorongoro haukuafiki jambo hilo. Ngorongoro ilielekezwa na Wizara kulipa Shilingi milioni 340 kwa ajili ya kutangaza utalii huko Marekani, kulipia gharama za watu watatu (wajumbe wawili wa Bodi na mfanyakazi mmoja) kuhudhuria mkutano wa kamataifa kwa ajili ya mafunzo ya kurejesha na kutunza vitu vya kiutamaduni ambao ulifanyika Roma kuanzia tarehe 14-16 Novemba, 2011. Pia, Wizara ilitoa maagizo ya kuchanga Shilingi bilioni 5.171 kwa ajili ya gharama ya kununua helicopter aina ya Bell 407 japokuwa agizo hili halikutekelezwa. Bodi katika kikao chake cha 101 tarehe 27 Oktoba, 2011 iliridhia na kuelekeza kuwa maagizo yote ya wizara yatekelezwe.

Mwingiliano mwingine umejitokeza katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara ambapo kiasi cha Shilingi milioni 28.616 ziilipokelewa kutoka Wizara ya Maji kwa ajili ya kuendeleza data za mifumo ya Kompyuta huko Mtwara. Fedha hizi ziliingizwa katika akaunti ya CRDB na kisha Mhasibu kutoka Wizarani alizichukua na kuzifanyia kazi huko Mtwara. Mwingiliano kama huu husababisha uwajibikaji hafifu katika matumizi ya rasilimali za umma.

8.1.7 Uteuzi Wenye Mapungufu wa Menejimenti ya Shirika la Masoko Kariakoo Uliofanywa na Halimashauri ya Jiji

Shirika la Masoko la Kariakoo lilianzishwa kwa sheria ya Bunge ya mwaka 1974 (Kariakoo Market Corporation Act 1974) na marekebisho yake ya mwaka 1984. Kifungu cha 5

kifungu kidogo cha 2(a) cha sheria iliyoanzisha shirika la masoko kimeelekeza kuwa Mwenyekiti wa Bodi atateuliwa na Rais na kifungu cha 5 kifungu kidogo 2(b) kinaeleza kuwa wajumbe wengine wa Bodi watateuliwa na Waziri mwenye dhamana.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa shirika la masoko limekuwa likiendeshwa bila ya Bodi ya Wakurugenzi ambayo imeundwa kwa mujibu wa Sheria tangu mwaka 2000 ambapo Bodi iliyopo iliwekwa madarakani na Halmsahsuri ya Jiji la Dar es Salaam. Pia Meneja Mkuu aliyetakiwa kuteuliwa na Rais aliwekwa madarakani na Waziri mwenye dhamana kinyume na Kifungu 5 (4) cha Sheria iliyoanzisha shirika. Mkanganyiko kama huo husababisha Bodi kushindwa kuwajibika katika matumizi ya rasilimali za umma.

8.1.8 Ucheleweshaji wa Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi na Wenyeviti

Sheria zinazoanzisha mashirika ya umma mara nyingi hutaja moja kwa moja kuwa Mwenyekiti wa Bodi atateuliwa na Rais na wajumbe wengine wa Bodi ya Wakurugenzi watateuliwa na Waziri mwenye dhamana. Uteuzi wa Wenyeviti na Wajumbe wengine wa Bodi za Wakurugenzi kwa wakati ni muhimu katika uendeshaji wa shughuli za shirika. Katika ukaguzi wa mwaka huu, nilibaini kuwa tatizo la kuchelewa kuteua Bodi mpya baada ya Bodi husika kumaliza muda wake limeendelea kuwepo katika baadhi ya mashirika. Mifano ya mashirika ambayo hayakuwa na Bodi za Wakurugenzi mpaka wakati nakamilisha ukaguzi wa mwaka huu ni Shirika la Bima la Taifa (NIC), Shirika la Viwango, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama na Mfuko wa Bima ya Afya. Kukosekana kwa Bodi ya Wakurugenzi siyo tu kunaathiri shughuli za uendeshaji wa shirika bali pia unasababisha kutokamilisha shughuli za ukaguzi wa hesabu za shirika kwa sababu kabla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kutia saini hati ya ukaguzi ni sharti Bodi iwe imeridhia hesabu zake.

8.2 Kamati ya Ukaguzi ya Bodi ya Wakurugenzi

Kamati ya Ukaguzi ni kamati ndogo ya Bodi ya Wakurugenzi ya kiufundi ambayo shughuli yake kubwa ni kusaidia Bodi kutimiza majukumu yake ya uangalizi na usimamizi wa shirika. Shughuli hizo zinahusu kupitia hesabu za shirika ili kuona kama zimeandaliwa vema na zina sifa zinazotakiwa, kusimamia zoezi la kuajiri, kujadili ripoti za wakaguzi wa nje, kutathimini uhuru wa wakaguzi wa nje na utendaji wa wakaguzi hao, kusimamia zoezi la uchaguzi wa kanuni na sera zinazoongoza uandaaji wa hesabu, kuangalia namna shirika linavyotimiza matakwa ya sheria mbalimbali, kusimamia maadili ya wafanyakazi na kujadili na kuamua juu ya mbinu za kulikinga shirika na mambo yanayoweza kulisababishia shirika kutokutimiza malengo yake.

Kulingana na taratibu zinazokubalika kama ambavyo zimetolewa na Chuo cha Wakaguzi wa Ndani Tanzania, Kamati ya Ukaguzi inatakiwa iwe angalau na wajumbe watatu na siyo zaidi ya wajumbe sita wa Bodi ya Wakurugenzi. Kila mjumbe anatakiwa awe huru na pia awe na ufahamu wa maswala ya taarifa za fedha. Katika Kamati hiyo ya Ukaguzi, anatakiwa awepo agalau mjumbe mmoja ambaye ana taaluma na amebobea katika maswala yanayohusu fedha. Licha ya umuhimu wa Kamati ya fedha katika usimamizi wa mashirika, bado kuna mapungufu ambayo yamejitokeza katika kamati za ukaguzi wa mashirika mbalimbali kama ifuatavyo:

8.2.1 Kutokuwepo Kamati Huru ya Ukaguzi

Kamati ya Ukaguzi yenye nguvu inahitaji wajumbe ambao ni huru, wasioukuwa na taasisi au idara nyingine ya kuwaingilia katika kazi yao. Wakati wa mapitio ya utendaji wa kamati za ukaguzi nilibaini kuwa shughuli za kamati ya ukaguzi zimechanganywa na kamati ya mipango na fedha. Mkanganyiko kama huu unasababisha utendaji usioridhisha wa Kamati ya Ukaguzi tofauti na ambavyo ingekuwa kama zingefanywa na kamati tofauti.

Wajibu wa kuandaa na kuwasilisha taarifa za hesabu ni jukumu la Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika husika, na kutokana na matakwa ya utawala kazi hii imekasimiwa kwa kamati ya ukaguzi na Bodi za Wakurugenzi ambapo kamati inapaswa kupitia na kuridhia hesabu hizo kabla hazijapelekwa kwa wakaguzi wa nje. Mapitio ya taarifa za hesabu yanayofanywa na kamati za hesabu yanalengo la kuhakikisha kuwa taarifa zimeandaliwa vizuri na kwamba hazina athari kubwa ambazo yatazifanya hesabu zisiwe nzuri.

8.2.2 Ukosefu wa Mpango Kazi wa Mwaka Katika Idara ya Ukaguzi wa Ndani

Ni wajibu wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani kufanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya utendaji wa shughuli za shirika. Kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya utendaji wa kitaalam, idara ya ukaguzi wa ndani inatakiwa kuwa na rejesta inayoonyesha orodha ya mambo ambayo yanahatarisha shirika kushindwa kufikia malengo yake na kufukia madhumuni ya uwepo wa shirika, ambayo yanatakiwa kujadiliwa na kuwa msingi wa uandaaji wa mpango kazi wa mwaka. Katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza hapakuwa na rejesta inayoonyesha orodha ya mambo ambayo yanaweza kusababisha shirika kushindwa kufikia malengo yake na hivyo ukaguzi wa ndani umeendelea kutokuwa na viwango vinavyotakiwa. Pia, imegundulika kuwa kitengo cha idara ya ukaguzi wa ndani hakina mpango kazi wa mwaka unaokidhi vigezo vya ukaguzi wa ndani wa kisasa. Kukosekana kwa mpango kazi huo, kunasababisha matumizi yasiyofaa ya nguvu kazi ya Idara ya ukaguzi wa ndani. Tatizo la ukosefu wa mpango kazi pia limejitokeza katika Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

8.2.3 Ukosefu wa Kitabu cha Mwongozo wa Ukaguzi na Programu za Ukaguzi

Kitabu cha mwongozo wa ukaguzi kinasaidia kuweka sera na taratibu za kufuata ili kuandaa na kufanya ukaguzi. Kitabu

hiki huonyesha kanuni na viwango vya ukaguzi na nidhamu ya kitaaluma ya ukaguzi wa ndani. Pamoja na umuhimu wa kitabu hiki nilibaini Idara ya Ukaguzi wa Ndani katika Mamlaka ya Maji safi na Maji Taka katika Jiji la Mwanza haina kitabu cha mwongozo wa ukaguzi wa ndani na programu za ukaguzi. Kukosekana mwongozo huu, kumesababisha mchakato wa ukaguzi kukosa mpango kazi, kukosa kumbukumbu za kazi iliyofanyika, na kukosa ushahidi wa waliopitia kazi za wakuguzi ili kuhakiki ubora na utoaji sahihi wa taarifa. Kwa kukosekana kwa mwongozo huu, imekuwa vigumu kuandaa programu ya ukaguzi na kuweka viwango madhubuti vya utunzaji kumbukumbu ya kazi ya ukaguzi iliyofanyika. Mashirika mengine yasiyokuwa na Kitabu cha Mwongozo wa ukaguzi ni pamoja na SIDO ambayo ina kitabu cha zamani sana, na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

8.2.4 Mapungufu Katika Idara ya Ukaguzi wa Ndani na Kamati ya Ukaguzi Katika Mfuko wa Bima ya Afya

Madhumuni ya Mkataba wa Ukaguzi wa Ndani (internal audit charter) katika shirika ni kuonyesha muundo, kazi, majukumu, na mamlaka ya Idara ya Ukaguzi wa Ndani na kuweka bayana maeneo yatakayofanyiwa kazi ya ukaguzi. Katika Mfuko wa Bima ya Afya nilibaini mapungufu kadhaa katika mkataba wa ukaguzi wa ndani, ambayo baadhi yake ni:

i. Kutokuwepo mapitio ya mkataba mara kwa mara ili kupima ubora wa mkataba kama inavyoeleza miongozo ya ukaguzi wa ndani. Mkataba huu haujawahi kufanyiwa mapitio tangu ulipotengenezwa mwaka 2009.
ii. Mkataba huu hauna mwongozo wa namna ya kutumia kazi za wataalam wengine mathalani katika uchunguzi wa jambo fulani.
iii. Mkataba huu umeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu kinyume na kanuni zinazosisitiza uhuru wa mkaguzi wa

ndani ambapo ilitakiwa mkataba huo uidhinishwe na Bodi ya Wakurugenzi.

Kwa upande mwingine, Mkataba wa Kamati ya Ukaguzi unaeleza juu ya mamlaka ya Kamati ya Ukaguzi katika uendeshaji wa shughuli za shirika. Pia unaeleza idadi ya wajumbe na muundo wa kamati ya ukaguzi, idadi ya mikutano itakayofanywa na kamati, mkaguzi wa ndani, mkaguzi wa nje pamoja na menejimenti. Zaidi ya hayo, mkataba wa kamati ya ukaguzi unaeleza majukumu ya kamati kuhusiana na maswala yanayohusu taarifa za fedha, mifumo ya udhibiti wa ndani, ukaguzi wa ndani, wakaguzi wa nje, ukubalifu, majukumu katika kutoa taarifa, na majukumu mengineyo kulingana na shirika husika. Hata hivyo, nilibaini kuwa Mfuko wa Bima ya Afya hauna Mkataba wa kamati ya ukaguzi ambao ungesaidia kamati kutimiza majukumu yake ya kusimamia shughuli za shirika katika kutoa taarifa za fedha, mifumo ya udhibiti wa ndani, ukaguzi na utaratibu wa kuhakikisha Mfuko wa Bima ya Afya unazingatia sheria na taratibu za utendaji kazi. Kukosekana kwa mkataba huu kunasababisha Kamati ya Ukaguzi ya Mfuko wa Bima kushindwa kupata maelekezo muhimu yanayohusu majukumu yanayotakiwa kutimizwa na kamati ya ukaguzi.

Pia nilibaini kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi ni mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi na Mkurugenzi Mkuu ni mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi kinyume na matakwa ya uongozi bora ambayo inamzuia Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi kuwa mwenyekiti wa kamati nyingine za Bodi. Wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi wanatakiwa kuwa wajumbe ambao hawahusiki na shughuli za kiutendaji. Zaidi, hakuna mawasiliano ya kutosha kati ya mkaguzi wa ndani na kamati ya ukaguzi kiasi kwamba ripoti zote hazikujadiliwa na kamati ya ukaguzi bali ziliwasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu pekee.

8.2.5 Ukosefu wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani Katika Mashirika

Kazi ya mkaguzi wa ndani ni kuhakikisha mifumo ya udhibiti wa ndani inazingatiwa na hivyo kuhakikisha mali za shirika hazipotei. Pamoja na umuhimu wa Idara hii ya ukaguzi wa ndani kwa shirika, imebainika kuwa nafasi ya kazi ya mkaguzi wa ndani katika Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) iko wazi kwa muda mrefu japokuwa jambo hili liliripotiwa katika barua ya ukaguzi kwa menejimenti ya STAMICO mwaka 2008. Nafasi hii imekuwa ikikainiwa tangu kipindi hicho ingawa hakuna kazi yoyote iliyofanyika, na wala hakukuwa na mchanganuo wa majukumu anayotakiwa kufanya. Ukosefu wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani madhubuti inaathiri uwezo wa kiutendaji na utunzaji wa mali za shirika.

Wakati huo huo, katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha, kukiwa na Idara ya Ukaguzi wa ndani, nilibaini kuwepo kwa Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani bila ya wafanyakazi wengine chini yake jambo linalokwamisha utendaji bora wa shughuli za ukaguzi wa ndani katika chuo.

8.2.6 Idadi Kubwa ya Wajumbe wa Bodi Kuzidi Inayotakiwa Katika Shirika la Maendeleo la Taifa

Sheria Na.90 ya mwaka 1969 iliyoanzisha shirika inatamka kuwa Bodi ya Wakurugenzi itakuwa na Mwenyekiti wa Bodi na wajumbe wengine wasiozidi tisa na hivyo kufanya jumla ya wajumbe wote kufikia kumi. Hata hivyo, katika ukaguzi niliofanya katika shirika mwaka huu, nilibaini kuwa Bodi ya wakurugenzi ina wajumbe wapatao kumi na mmoja kinyume na kanuni ya 90 ya sheria ya mwaka 1969. Kitendo hiki ni uvunjifu wa sheria na matokeo yake ni kuongeza gharama za uedeshaji kwa shirika la maendeleo pasipo sababu.

8.2.7 Changamoto Zinazoikabili Shirika la Bima la Taifa (NIC)

Shirika la Bima la Taifa lilifanyiwa marekebisho upya mwaka 2009 na Bodi ya Wakurugenzi ambayo muda wake ulikwisha mwezi Aprili, 2012. Kutoka kipindi hicho, Shirika

linaendeshwa chini ya Kaimu Mkurugenzi. Changamoto zinazoikabili shirika kwa kiasi kikubwa zimesababishwa na Shirika kukosa Bodi ya Wakurugenzi ya kusimamia utekelezaji wa mipango ya Shirika. Ukosefu wa Bodi ni ishara mbaya kuwa Serikali imeliachia shirika kujiendesha kwa maamuzi ya menejimenti. Maamuzi muhimu ambayo yalitakiwa kufanywa na Bodi yameshindikana kutekelezwa. Maamuzi haya ni pamoja na kutoweza kuajiri wafanyakazi katika nafasi za Meneja na ngazi za juu ambazo ni muhimu katika kufikia malengo ya shirika. Hatua za kinidhamu haziwezi kuchukuliwa kwa wafanyakazi wa ngazi za juu ambao wanakiuka maamuzi ya Shirika kwa sababu Bodi ndiyo yenye mamlaka ya kuwawajibisha. Menejimenti ya shirika imekosa miongozo mbalimbali ya kimkakati ambayo ingetolewa na Bodi baada ya kupitia taarifa mbalimbali za kiutendaji.

Bajeti ya shirika ya kila mwaka ni lazima iidhinishwe na bodi kabla ya kufanya matumizi yoyote ambayo yapo kwenye mpango kazi wa mwaka husika. Ukaguzi umebaini kuwa bajeti ya shirika ya mwaka 2013 haijapitishwa na Bodi lakini shirika linatumia bajeti hii katika shughuli zake. Ni wazi kuwa shirika linatumia bajeti ambayo haikuidhinishwa na Bodi. Menejimenti inasubiri Bodi iteuliwe ili kupeleka bajeti hii ipate idhini mrejeo. Hesabu za shirika kwa mwaka wa fedha unaoisha tarehe 31 Disemba, 2011 zimekamilika na zinasubiri kuidhinishwa na Bodi kabla ya kusainiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa kuwa shirika halina bodi, hesabu haziwezi kuidhinishwa wala kujadiliwa na Kamati ya Bunge. Hii ni ishara mbaya ya kurudisha nyuma maendeleo ya shirika hili.

Kaimu mkurugenzi wa shirika amekaimu cheo hiki kwa miaka minne sasa. Ni wazi kuwa Kaimu Mkurugenzi hataweza kuwa makini sana katika kutekeleza malengo ya Shirika kwa kuwa hana uhakika kama ataidhinishwa na Bodi kuwa Mkurugenzi wa shirika. Hali hii pia inaleta hali ya

wasiwasi na kuvunjika moyo kwa Afisa Mtendaji Mkuu na wafanyakazi anaowaongoza. Pia, kukosekana kwa Mtendaji Mkuu ambaye amethibitishwa kunaathiri utendaji wa shirika kimapato kwani wateja wengi wanakosa imani na mkakati wa Serikali wa kurekebisha Shirika hilo. Wafanyakazi wengi wa shirika wanafanya kazi kwa mkataba na mikataba hiyo imemalizika tarehe 31 Disemba, 2012. Menejimenti ilifanya tathmini ya utendaji wa wafanyakazi kutokana na muongozo waliopewa na Wizara ya Fedha na wale walioonekana wanastahili walirejeshwa kazini tarehe 2 Januari, 2013 kuanza kipindi kipya. Hata hivyo, mikataba yao bado haijasainiwa kutokana na kukosekana kwa Bodi ya Wakurugenzi.

Pia, nilibaini kuwa shirika linafanya biashara ndogo sana kutoka serikalini na taasisi zake kutokana na ukweli kwamba Taasisi chache za Serikali ndizo zimekata Bima ya mali zake kwenye Shirika la Bima la Taifa. Serikali iwe na mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kuwa Serikali na taasisi zake zinapata mahitaji ya bima kutoka Shirika la Bima. Jambo hili, litasaidia Shirika kukua ndani ya miaka michache ijayo.

SURA YA TISA

VITEGA UCHUMI VYA SERIKALI, UMILIKI/UWEKEZAJI WA SERIKALI NA MCHAKATO WA UBINAFSISHAJI

9.0 Utangulizi

Sura hii inatoa mwanga juu ya masuala yanayohusiana na vitega uchumi, riba na mchakato wa ubinafsishaji wa yaliyokuwa Mashirika ya umma ambayo serikali inamiliki hisa chini ya asilimia 50 na yale ambayo serikali inamiliki hisa zaidi ya asilimia 50. Masuala yanayohusiana na vitega uchumi vya serikali katika ripoti hii, yametolewa katika taarifa ya msajili wa Hazina kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012. Kwa upande mwingine, masuala yanayohusiana na mchakato wa ubinafsishaji, ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa, yametokana na taarifa ya ubinafsishaji na ripoti ya ufuatiliaji na tathmini ya mashirika yaliyokwishakubinafsishwa kwenye kipindi hiki cha mapitio.

Utendaji kazi wa Mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2011/2012 umepimwa kutokana na ukusanyaji wa mapato yanayotokana na madeni ambayo serikali imewawekea dhamana wakopaji. Mapato yaliyokusanywa na Msajili wa Hazina ni yale yele yatokanayo na gawio, makusanyo kutokana na malipo ya mikopo na mapato mengine. Mambo mengine yaliyoangaliwa ni pamoja na malimbikizo ya maduhuli.

Sura hii imegawanywa katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu masuala mbalimbali yanayohusiana na vitega uchumi vya serikali na sehemu ya pili inahusiana na mchakato wa ubinafsishaji wa mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya ubinafsishaji.

9.1 Vitega Uchumi Vya Serikali

9.1.1 Vitega Uchumi Katika Taasisi za Ndani

Uwekezaji wa serikali kwenye makampuni ya ndani umeongezeka kutoka Shilingi za kitanzania trilioni 10.276 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 hadi Shilingi trillioni 12.215 kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2012. Hizi ni hisa za Serikali na fedha nyingine za wanahisa katika makampuni 212. Ongezeko kubwa katika Mfuko wa wanahisa ulisababishwa na kuongezeka kwa Mashirika ya Umma na taasisi za Serikali ambazo ziliwasilisha Hesabu zao zilizokaguliwa. Taasisi nyingi za Serikali/Mashirika ya Umma yamekuwa yakiwasilisha hesabu zao zilizokaguliwa ambazo zinaonyesha tathmini ya sasa ya fedha za hisa, mtaji na fedha za wabia wengine. Sababu nyingine ni ongezeko la ziada litokanalo na tathmini ya ongezeko la taasisi za Serikali/ mashirika ya Umma kutoka 204 mwaka 2010/2011 hadi 213 ya mwaka 2011/2012.

9.1.2 Uwekezaji Katika Mashirika ya Nje

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012, Serikali ilikuwa imewekeza Shilingi za kitanzania bilioni 145.9 katika taasisi tisa za nje. Nafasi ya uwekezaji imepungua ikilinganishwa na Shilingi za kitanzania bilioni 157.5 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011. Hisa zinazomilikiwa na Serikali katika taasisi za nje, mara kwa mara zimekuwa zikibaki karibu sawa katika taasisi zote. Hata hivyo, thamani ya uwekezaji imepungua kutokana na kubadilika kwa kiwango cha kubadilisha fedha ya kigeni na kutokana na hasara ya uendeshaji katika baadhi ya Mashirika hayo.

9.1.3 Madeni Yaliyodhaminiwa na Serikali

Jumla ya madeni yaliyodhaminiwa na Serikali ya Tanzania kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 ni kiasi cha Shilingi za kitanzania bilioni 498.7 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 461.6 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011. Ongezeko hili linatokana na deni la riba ya mkopo wa TFC. Madeni haya yapo katika makundi kama ifuatavyo:

(a) Mashirika ya Umma ambayo hayaendelei na uzalishaji na bado yapo chini ya mpango wa mfilisi wa kampuni ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Mkonge Tanzania, State Motors Corporation, SUKITA na Kiwanda cha Matairi Arusha. Haya yote yana jumla ya Shilingi za kitanzania billioni 33.1 ambayo ni asilimia 6.64 ya jumla ya dhamana zote.

(b) Mashirika ya Umma ambayo utaratibu wa malipo yake ulibadilishwa ni pamoja na kiwanda cha nguo cha urafiki ambapo deni lake lililobakia kutokana na mkopo ni Shilingi za kitanzania bilioni 25.8, ambayo ni sawa na asilimia 5.17 ya jumla ya dhamana zote.

(c) Mashirika yenye matatizo ya kifedha ni pamoja na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ambayo ina dhamana ya jumla ya Shilingi za kitanzania billioni 121.7, Shirika la Ndege Tanzania Shilingi za kitanzania bilioni 48.8, Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) Shilingi za kitanzania bilioni 41.9 na Chama Kikuu cha Ushirika Mara Shilingi za kitanzania bilioni 8.5. Zote zina jumla ya Shilingi za kitanzania bilioni 220.9 ambazo ni sawa na asilimia 44.29 ya jumla ya dhamana yote.

(d) Mashirika ya Umma ambayo mikopo yake inafuata taratibu zilizowekwa ikiwa ni pamoja na mkopo wa TANESCO Shilingi za kitanzania bilioni 203.0, Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwa Kitivo cha Biashara kimebakiwa na deni la Shilingi za kitanzania milioni 894.8. Deni la mkopo lililobaki ni la thamani ya Shilingi za kitanzania bilioni 203.9 sawa na aslimia 40.89 ya jumla ya dhamana zote.

(e) Mashirika ya Umma ambayo mikopo yake haijalipwa katika mchakato wa mufilisi ni pamoja na Shirika la Magari Tanzania. Deni la mkopo lililobaki ni la thamani ya Shilingi za kitanzania bilioni 3.1, ambayo ni sawa na asilimia 0.61 ya jumla ya dhamana yote.

(f) Dhamana mpya ya Shilingi za kitanzania bilioni 15.0 iliyotolewa kwa NBAA ili kupata mkopo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha wataalam wa uhasibu na ukaguzi ambayo ni sawa na asilimia 3.01 ya jumla ya dhamana zote.

Kama ilivyobainishwa, jumla ya kiasi cha dhamana kimeongezeka kwa asilimia 7.43 au kwa Shilingi za kitanzania bilioni 37.1 kutoka Shilingi za kitanzania bilioni 461.6 mwaka 2010/2011 hadi Shilingi za kitanzania bilioni 498.7 kwa mwaka 2011/2012. Ongezeko limesababishwa na malimbikizo ya riba, adhabu, ubadilikaji wa kiwango cha fedha za kigeni pamoja na dhamana mpya zilizotolewa mwaka uliotangulia.

9.1.4 Mapato ya Serikali

Mapato yaliyokusanywa na ofisi ya Msajili wa Hazina kutokana na Gawio, urejeshaji wa mikopo na mapato mengine kutoka kwenye Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hadi tarehe 30 Juni, 2012 yaliongezeka kwa Shilingi za kitanzania bilioni 179.3 sawa na asilimia 622.8, kutoka Shilingi za kitanzania bilioni 28.8 ikilinganishwa na shillingi bilioni 208.1 zilizokusanywa kwa mwaka 2011/2012. Hata hivyo bajeti iliyopangwa kwa ajili ya mwaka huu ilikuwa ni Shilingi bilioni 204.9

(i) Ongezeko hili linatokana na sababu zifuatazo: Utendaji mzuri wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama vile Benki Kuu, Shirika La Posta Tanzania (TPC), NMB, TCC n.k ambayo limesababisha ongezeko la gawio na kulipwa Hazina ya Serikali kutoka Shilingi bilioni 19.8 katika mwaka 2010/2011 hadi Shilingi bilioni 186.8 katika mwaka 2011/2012 na kufanya tofauti ya Shilingi za kitanzania bilioni 167 ambazo ni sawa na asilimia 843.3.

(ii) Katika kuhimiza na kutilia msisitizo wa ufuatiliaji wa waraka wa Hazina Na.8 unaotaka mashirika kuchangia

asilimia 10 ya mapato ya shirika katika shughuli za kawaida umesababisha ongezeko la mapato kutoka Shilingi za kitanzania bilioni 6.7 kwa mwaka 2010/2011 hadi Shilingi za kitanzania bilioni 19.4 katika mwaka 2011/2012 na hivyo basi kufanya tofauti ya Shilingi bilioni 12.7 sawa na asilimia 193.

(iii) Ulipaji wa Madeni ya Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa Serikali, ulisababisha kupungua kwa kiasi cha mkopo na riba kutoka Shilingi za kitanzania bilioni 2.3 kwa mwaka 2010/2011 hadi Shilingi za kitanzania bilioni 1.8 kwa mwaka 2011/2012, ambayo inaleta tofauti ya Shilingi za kitanzania millioni 519 ambayo ni sawa na asilimia 22.

Kwa muhtasari, mapato yaliyokusanywa kutokana na gawio, ulipaji wa mkopo na mapato mengine kwa miaka minne iliyopita ilikuwa kama ifuatavyo:

Jedwali Na 12: Mwenendo wa Gawio, Ulipaji wa Mikopo na Mapato Mengine

Mwaka wa fedha	Gawio (Sh.)	Mikopo na Riba (Sh.)	Mapato mengine (Sh.)	Jumla (Sh.)
2008/2009	31,323,253,591	6,795,002,069	46,001,873,960	**84,120,129,621**
2009/2010	15,127,480,388	11,465,621,623	14,056,617,906	**40,649,719,917**
2010/2011	19,801,780,952	2,340,022,351	6,651,641,793	**28,793,445,096**
2011/2012	186,821,446,957	1,820,096,604	19,490,988,564	**208,132,532,126**

Maelezo hayo hapo juu yanaweza kuonyeshwa kwenye kielelezo kama ifuatavyo:

Kielelezo Na 5: Mwenendo wa Gawio, Ulipaji wa Mikopo na Mapato Mengineyo Kuanzia Mwaka wa Hesabu 2008/2009 hadi 2011/2012



9.1.5 Malimbikizo ya Mikopo

Kulikuwa na malimbikizo ya maduhuli yapatayo Shilingi za kitanzania bilioni 95.3 kati ya kiasi hicho cha Shilingi za kitanzania bilioni 94.5 zilitakiwa kuwa zimeshakusanywa. Malimbikizo hayo yamesababishwa na kuwa na Mashirika ya Umma ambayo hayafanyi vizuri kiutendaji. Mfano TANESCO, TRC (sasa ni Kampuni ya kusimamia Rasilimali za Shirika la Reli (RAHCO) na TTCL. Mashirika haya yana matatizo ya kifedha, hivyo kuwa vigumu kurejesha mikopo yao. Riba uamuzi wa malimbikizo yasiyolipwa ya malimbikizo ya mikopo ya Serikali ya Zanzibar bado haujatolewa na Serikali mbili. (Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar).

9.1.6 Deni La Serikali Kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Deni ambalo serikali inadai mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2012 limepungua na kufikia Shilingi za kitanzania bilioni 466.5 kutoka Shilingi za kitanzania bilioni 480.2 kwa mwaka 2010/2011. Upungufu huu kwa kiasi kikubwa unatokana na malipo yaliyofanywa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Shirika la Simu Tanzania (TTCL) na Shirika la Bima ya Taifa (NIC). Pia kulikuwa na malipo ya mkopo kutoka mashirika mengine kama Tanzania Automech Ltd, Mamlaka ya Anga Tanzania (TCAA) pamoja na Tanzania Portland Cement Company (TPCC). Mashirika hayo yamefuata taratibu katika ulipaji wa mkopo.

Jumla ya malimbikizo ya mikopo yalipungua kwa asilimia 2.86 kutoka Shilingi za kitanzania bilioni 98.3 kwa mwaka 2010/2011 hadi Shilingi za kitanzania bilioni 94.5 katika mwaka 2011/2012. Upungufu huo ulitokana na kumalizika kwa mikopo kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania, mikopo kutoka Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL) na Shirika la Bima la Taifa.

Kiwango cha mikopo kilichokusanywa kutoka katika mikopo na riba kimepungua kwa Shilingi za kitanzania milioni 211.1 ambayo ni sawa na asilimia 9.02 kutoka Shilingi bilioni 2.4 kwa mwaka 2010/2011 hadi Shilingi za kitanzania bilioni 2.1 katika mwaka 2011/2012. Jumla ya malimbikizo yenye thamani ya Shilingi za kitanzania bilioni 94.5 kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012. Shilingi za kitanzania bilioni 20.7 ilikuwa kwa ajili ya Zanzibar, Shilingi za kitanzania bilioni 48.9 kwa ajili ya mkopo wa TRC na Shilingi za kitanzania bilioni 21.3 ni kwa ajili ya mkopo wa TANESCO. Taasisi hizi tatu zinafikisha jumla ya asilimia 96.23 ya malimbikizo yote yaliyopaswa kulipwa kulingana na vipengele vya mkataba.

9.2 Maendeleo Ya Ubinafsishaji

Shirika Hodhi la Mali za Umma kutoka lilipoanzishwa hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2012 limeweza kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:
Uuzaji wa majengo ambayo umeliingizia shirika Shilingi za kitanzania bilioni 27.12 ambayo ni sawa na asilimia 109.8 ikilinganishwa na matarajio ya mpango wake ambao ulikadiria kupata Shilingi za kitanzania bilioni 24.7. Ukusanyaji wa madeni chechefu na ufilisi umeliingizia Shirika kiasi cha Shilingi za kitanzania bilioni 31.2 ambazo ni sawa na asilimia 133 ya matarajio ya mpango wake yaliyokadiriwa kukusanya Shilingi za kitanzania bilioni 23.5 kutoka lilipoundwa. Riba katika dhamana za Serikali zilizorithiwa kutoka iliyokuwa NBC, dhamana katika mabenki na gawio kutoka NBC Ltd ziliingiza jumla ya Shilingi za kitanzania bilioni 33.1. Jumla ya Shilingi za kitanzania bilioni 4.0 zilikusanywa kutokana na mapato ya pango na huduma mbalimbali. Shirika limefanikiwa kukamilisha ufilisi wa mashirika 12 ya Umma na kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 6.6. Shirika limeendelea kusimamia kesi 330 zilizofunguliwa katika mahakama mbalimbali hapa nchini. Kesi hizi ni zile zilizorithiwa kutoka kwenye taasisi za Serikali ambazo muda wake ulifikia ukomo kwa mfano; ATHCO, SIMU 2000 Ltd; PSRC.

Shirika lilirithi mashirika 34 yaliyokuwa kwenye mchakato wa ubinafsishaji/ urekebishaji kutoka iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC). Hadi kufikia Mwaka 2012 Shirika liliweza kupata mafanikio kwenye urekebishaji wa mashirika katika vitu vifuatavyo; Kusainiwa Kwa Mkataba wa Maelewano (Deed of settlement) Kati ya Serikali na kampuni ya Rites ya India kuhusu Kampuni ya TRL, Kusaini mkataba wa Mauzo wa Kiwanja Na 10, Barabara ya Nyerere na kukabidhi ghala la NMC Ghana Iringa kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Aidha, Shirika limeweza kukusanya kiasi cha Shilingi za kitanzania bilioni 2.8 kutoka katika shughuli za

ubinafsishaji. Pia jumla ya mashirika 170 yaliyobinafsishwa yameweza kusimamiwa na kufanyiwa tathmini.

9.2.1 Hali Halisi Ya Ubinafsishaji

Hadi kufikia Disemba, 2012 jumla ya mashirika 274 yamebinafsishwa. Kati ya mashirika hayo; mashirika 95 yapo katika Sekta ya Kilimo, 94 sekta ya Viwanda, 23 sekta ya Miundombinu, 34 sekta ya Maliasili na Utalii, 15 sekta ya Nishati na Madini na mashirika 13 kutoka sekta zingine. Pia, jumla ya mashirika 29 yalikuwa katika hatua mbalimbali za ubinafsishaji; Kwa Mfano New Africa Hotel na National Bank of Commerce (NBC). Kulikuwa na mashirika 13 ambayo yalikuwa katika hatua mbalimbali za urekebishaji, Mfano; Shirika la Bima la Taifa (NIC), General Tyre East Africa Limited na Shirika la Posta Tanzania (TPC). Mashirika Saba (7) yaliyobinafsishwa yalikuwa na masuala mbalimbali yaliyohitaji ufumbuzi. Masuala hayo ni pamoja na kushindwa kwa wawekezaji kutekeleza kikamilifu mikataba ya mauzo. Serikali ililazimika kufanya uamuzi wa kuyachukua mashirika hayo na kuyaendesha yenyewe. Baadhi ya mashirika yaliyorudishwa serikalini ni pamoja na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), Shirika la Reli Tanzania na Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira. Serikali ilikuwa imekamilisha ufilisi wa mashirika 47 Kati ya mashirika 65 yaliyowekwa chini ya ufilisi. Ufilisi wa mashirika 18 ulikua unaendelea na ulikua katika hatua mbalimbali. Jumla ya Mali 682 ambazo hazikua sehemu-muhimu ya biashara ya mashirika yaliyobinafsishwa zimeuzwa kwa watu mbalimbali. Sehemu kubwa ya Mali hizi ni pamoja na Viwanja, Nyumba, Maghala n.k

Shughuli zifuatazo bado hazijakamilishwa na hivyo shirika linaendelea kuzitekeleza, nazo ni:

- kuuza jengo moja lililobakia ambalo ni George's Grill (Jengo la kantini ya zamani ya NBC) ambalo lipo mtaa wa pamba Dar es salaam.
- Ubinafsishaji na kurekebisha mashirika ya umma yapatayo 42.

- Ufilisi wa mashirika 18 yaliyobakia.
- usimamiaji wa kesi za madai 330 zilizopo katika mahakama mbalimbali za hapa nchini.
- ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wakopaji wa iliyokuwa benki ya NBC yanayofikia Shilingi za kitanzania bilioni 60 (ukijumlisha na riba ya Shilingi za kitanzania bilioni 21) na Shilingi za kitanzania bilioni 48.7 (riba; Shilingi za kitanzania billioni 34) yanayotokana na ubinafsishaji wa mashirika ya umma uliofanywa na PSRC.

SURA YA KUMI

MATOKEO YA KAGUZI MAALUM

10.0 Utangulizi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anayo Mamlaka ya kisheria chini ya Kifungu namba 29(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kufanya ukaguzi maalum kufuatia maombi ya mtu, taasisi, wizara, idara, wakala, mamlaka ya serikali za mitaa na Mashirika ya Umma, kamati za kudumu za bunge na taasisi nyinginezo.

Kufuatia kifungu hicho cha Sheria, katika mwaka huu wa fedha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanya jumla ya kaguzi maalum nne katika mashirika ya Umma. Mashirika ya Umma ambayo kaguzi hizi Maalum zilifanyika ni Shirika la Ugavi na Usambazaji wa Umeme Nchini (TANESCO), Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), Shirika Hodhi la Mali za Reli (RAHCO) na Chuo cha Biashara (CBE).

Matokeo ya kaguzi Maalum yameainishwa kwenye ripoti hii kwa muhtasari, hivyo matokeo ya kina yanapatikana katika ripoti husika ambazo hupatikana katika Mamlaka zilizoomba kufanyika kwa kaguzi hizi Maalum. Yafuatayo ni matokeo ya kaguzi Maalum zilizofanyika na kukamilika katika kipindi cha mwaka huu wa ukaguzi:-

10.1 Shirika la Ugavi wa Umeme Nchini (TANESCO)

Bodi ya Wakurugenzi wa TANESCO ilimuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi Maalum. Ukaguzi huo uligawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni awamu ya kwanza na awamu ya pili.

Awamu ya kwanza ya ukaguzi huu Maalum, ilikuwa ni kwa ajili ya Mkataba Na. PA/001/11/HQ/G/011 unaohusu ugavi wa vifaa vya ofisi, vifaa vya matumizi ya Kompyuta na Mashine za kudurufu ulioanza tarehe 20 Disemba

2011.Mkataba huu unahusu Kampuni ya Santa Clara Supplies Company Limited. Mkataba mwingine wa kukarabati na kutengezeza njia za umeme (Live line) kwa mwaka 2008, 2009, 2010 na 2011 unaohusu Kampuni ya McDonald Live Line Technology Limited.

10.1.1 Matokeo ya Ukaguzi Maalum wa Awamu ya Kwanza Yalikuwa Kama Ifuatavyo:-

Santa Clara Supplies Company Limited

(i) Santa Clara Supplies Company Limited ni kampuni iliyosajiliwa mnamo tarehe 18 Aprili, 2011, na kupewa hati ya usajili Na. 82777, Leseni ya Biashara Na.B. 01291130 iliyotolewa Mei 2011 na namba ya utambulisho ya Mlipa kodi (TIN) 112-813-659 iliyotolewa tarehe 28 Aprili 2011. Namba ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VRN) ya Kampuni ni 40-012119-E. Wakurugenzi na wanahisa wa Kampuni ni mke na watoto wawili wa aliyekuwa Mkurugenzi wa TANESCO.

(ii) Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Santa Clara ni mke wa aliyekuwa Mkurugenzi wa TANESCO na pia alikuwa ni mfanyakazi wa TANESCO ambaye aliacha kazi baada ya mume wake kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO.

(iii) Kampuni hiyo ilipewa zabuni Na. PA/001/11/HQ/G/011 ya ugavi wa vifaa vya ofisi, vifaa vya matumizi ya Komputa na Mashine za kudurufu kwa mwaka 2011/2012. Jumla ya wazabuni 14 walipewa zabuni ya jumla ya Shilingi milioni 884.55 ikijumuisha zabuni ya Santa Clara ya Shilingi milioni 147.5. Iligundulika kuwa Mkataba wa TANESCO na Kampuni ya Santa Clara haukuonyesha kiasi cha fedha ya zabuni aliyopewa. Bali iliambatanishwa fomu ya zabuni yote ya Shilingi milioni 884.55. kwa hali hiyo kampuni ya Santa Clara Ltd ingeweza kupewa zabuni ya vifaa vya ofisi

hadi kufikia thamani ya Shilingi milioni 884.55. Mkataba ulisainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO ukishuhudiwa na Mwanasheria wa Shirika la TANESCO na Mkurugenzi wa Santa Clara aliyeshuhudiwa na shuhuda mmoja.

(iv) Tarehe 24 Januari, 2012 Kampuni ya Santa Clara ilipewa oda namba 2000009446-1 ya kuuza rimu 2,500 za karatasi kwa bei ya Shilingi 7,000 kila moja. Jumla ya gharama ya oda nzima ilikuwa ni Shilingi milioni 20.65 ikijumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Kampuni ya Santa Clara iliweza kuwasilisha TANESCO rimu 500 tu za karatasi zenye thamani ya Shilingi milioni 4.13. Tarehe 22 Februari, 2012 Santa Clara iliwasilisha barua ikiomba ongezeko la bei ya rimu moja za karatasi kutoka Shilingi za kitanzania 7,000 hadi Shilingi 10,000 kwa rimu moja. Ongezeko hilo la bei halikukubaliwa na TANESCO, hivyo Kampuni ya Santa Clara haikuweza tena kuendelea kuwasilisha rimu za karatasi. Hali hiyo ilipelekea zabuni hiyo kutekelezwa na kampuni nyingine. Hali hii ingekuwa imeonekana mapema wakati wa tathmini ya zabuni kwani mali za Kampuni ya Santa Clara zilikuwa ni Shilingi za kitanzania 107.7 milioni. Kiasi hicho kikijumuisha Shilingi za kitanzania milioni 41.3 kwa mali za kudumu na Shilingi za kitanzania milioni 66.4 kwa mali za muda mfupi. Kamati ya tathmini ilitakiwa iwe imekwisha ona uwezo wa Kampuni ya Santa Clara kwamba haina uwezo wa kusimamia zabuni kubwa. Hata hivyo katika kipindi chote cha mwaka 2011 na 2012 kampuni ya Santa Clara ililipwa jumla ya Shilingi za kitanzania milioni 31.825.

(v) Moja ya matakwa ya zabuni Na. PA/001/11/HQ/G/011 ilikuwa ni wazabuni kuwasilisha taarifa za hesabu za hivi karibuni zilizokaguliwa. Kampuni ya Santa Clara iliwasilisha

hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2010 katika kujaribu kutimiza matakwa ya kupewa zabuni. Ilikuja kubainika kuwa hesabu zilizokaguliwa na kuwasilishwa na Kampuni ya Santa Clara zilikuwa ni za kughushi kwa kuwa kampuni hiyo ilisajiliwa tarehe 18 Aprili, 2011. Hesabu hizo zilisainiwa na Kampuni ya ukaguzi wa Fix Capital Certified Public Accountants ambayo usajili wake kwenye Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) ulikuwa umesitishwa. Mamlaka ya Mapato (TRA) ilithibisha kuwa Kampuni ya Santa Clara iliwasilisha makadirio ya kodi kwa mwaka 2011, lakini Kampuni hiyo haikuwasilisha rejesho la kodi yoyote kwa mwaka 2011. Kwa hiyo kiasi cha Shilingi milioni 4.854 zilizolipwa na TANESCO kwa Santa Clara hazikuwasilishwa TRA.

(vi) Mkurugenzi Mkuu wa Tanesco hakuweka wazi mgongano wake wa kimaslahi kwenye manunuzi haya kama inavyotakiwa na kifungu namba 2.2 cha Kanuni za maadili za TANESCO. Kampuni ya Santa Clara pia haikuweka wazi mgongano wake wa kimaslahi uliopo kati yake na TANESCO kwenye nyaraka zake za zabuni. Kampuni ya Santa Clara pia haikuwasilisha idadi ya mikataba mikubwa iliyowahi kupewa katika kipindi cha miaka miwili ya nyuma kama ilivyokuwa inatakiwa kwenye nyaraka zake za zabuni. Kwa maana hiyo Santa Clara haikustahili kupewa zabuni hiyo.

McDonald Live Line Technology Limited

(i) Kampuni ya McDonald Live Line Technology Limited ilisajiliwa tarehe 24 Disemba, 2004 kama ilivyo kwenye hati ya usajili wa Kampuni Na. 51044. Namba ya utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) 103-598-478 iliyotolewa tarehe 27 Mei, 2005. Namba ya usajili ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) (VRN) 10-017916-C. Wana hisa na Wakurugenzi wa Kampuni hiyo ni

watanzania watatu wenye umiliki wa hisa 50:30:20 kwa mfuatano pamoja na Wakurugenzi watatu.

(ii) Mmiliki wa McDonald Live Technology Ltd alikuwa mfanyakazi katika Shirika la TANESCO na aliachishwa kazi tarehe 19 Julai, 1999 kwa sababu za utoro kazini, kutowajibika na upotevu wa jumla ya kiasi cha Shilingi milioni 1.280. Pia aliharibu gari la Shirika lenye namba za usajili TZD 2944. Mmiliki (1st party) huyu aliingia kwenye makubaliano ya ubia na Mkurugenzi mmoja wa TANESCO (2nd party) tarehe 17 Julai, 2008 ambaye baadae aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO.

(iii) Pia walikubaliana kwamba Mkurugenzi wa TANESCO atawajibika kutafuta miradi na kazi kutoka kwa wateja na McDonald Live Technology Limited itawajibika na utekelezaji wa Miradi. Ubia huu haukuwa umesajiliwa na Wakala wa kuandikisha na kutoa leseni za Biashara (BRELA). Mkurugenzi wa TANESCO hakuweka hadharani mgongano wa kimasilahi alionao na Kampuni ya McDonald baada ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO kama inavyotakiwa na Kanuni za Maadili za TANESCO.

(iv) Kwa kipindi kilichoanzia mwaka 2009 hadi 2011, Kampuni ya McDonald Live ilipewa jumla ya mikataba ya zabuni mitano kama ifuatavyo:

(a) Mkataba wa Disemba, 2008 kukarabati na kutengeneza njia ya umeme hai Mtibwa Km 35 na ni mkataba wenye kumbukumbu namba MSG/S006/2008–wa Shilingi za kitanzania milioni 73.810 ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani. Nyaraka za zabuni hii hazikuweza kuwasilishwa kwa wakaguzi kwa ajili ya ukaguzi.

(b) Mkataba wa kukarabati njia ya Nordic 33kV wa tarehe 20 Mei, 2009 – wa kiasi cha Shilingi za kitanzania milioni 110.1 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani. Mkataba huu ulitekelezwa bila kuwepo kwa dhamana ya benki kama nyaraka za zabuni zililivyoelekeza.

(c) Mkataba Na.PA/001/09/HW/W014 wa kukarabati njia ya Kiyungi – Arusha 66kV wa tarehe 11 Machi, 2010 – wa Shilingi za kitanzania bilioni 1.417 pamoja na Kodi ya ongezeko la thamani (VAT); Kazi ilianza tarehe 28 Julai, 2010 na ilitakiwa kuwa imemalizika tarehe 9 Machi, 2011. Kufuatia kutokamilika kwa wakati, kazi hiyo iliongezewa muda wa wiki 19 ili kuikamilisha kazi mara ifikapo 13 Julai, 2011 lengo ambalo halikufikiwa. Muda wa Mkataba uliongezwa tena hadi tarehe 23 Novemba, 2011 ambapo mradi huo pia haukukamilika. Tarehe 19 Juni, 2012, TANESCO ilivunja mkataba huo. Mpaka kufikia kuuvunja mkataba huo McDonald live line Technology ilikuwa imeshalipwa kiasi cha Shilingi za kitanzania milioni 475.6 kama malipo ya awali, ambayo ni asilimia 33 ya mkataba mzima na kinyume na ilivyoainishwa kwenye masharti ya zabuni kuwa, malipo ya awali yatakuwa ni asilimia 15 ya mkataba. TANESCO ilifanya tathmini na kubaini kuwa McDonald live line Technology ilitakiwa kuirejeshea TANESCO kiasi cha Shilingi za kitanzania milioni 504.7 ikiwa ni faini, fidia na kiasi cha dhamana ya benki kilichokadiriwa. Hadi wakati wa kuhitimisha ukaguzi huu Maalum kiasi hicho cha fedha kilikuwa bado hakijarejeshwa TANESCO na Kampuni ya McDonald Live line Technology Company.

(d) Mkataba Na. PA/001/10/HQ/W/025 wa kukarabati njia ya Ifakara 33kV kutoka Kidatu hadi Mahenge na njia ya Mtibwa 33Kv kutoka Mkundi hadi Mvomero wa tarehe 27 Julai, 2010 wa Shilingi za kitanzania 338,247,000.00 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT); na

(e) Mkataba wa matengenezo na ukarabati wa njia za umeme ukiwa haujazimwa (live line) wa Mzakwe 33Kv, Dodoma wa tarehe 6 Januari, 2011 wa Shilingi za kitanzania milioni 49.5 pamoja na Kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Nyaraka za zabuni hii hazikuwasilishwa kwa wakaguzi kwa ajili ya ukaguzi.

Kutokana na hoja hizo za ukaguzi ni wazi kwamba, McDonald Live Line Technology Company Ltd ilipewa mikataba hiyo na Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO kufuatia makubaliano ya ubia kati yake na Mmiliki wa Kampuni hiyo, kama sehemu ya pili ya ubia iliyompa jukumu la kutafuta kazi za kufanya kwa kampuni hiyo.

(V) Uthibitisho kutoka BRELA ulionyesha kwamba Kampuni ya McDonald Live Line Technology Company Ltd haikuwasilisha mrejesho wowote kwa miaka ya 2005, 2006, 2007, 2008, 2009, 2010 na 2011. Pia Kampuni hiyo haikuwasilisha hesabu zozote za mwaka katika vipindi hivyo. Kiasi cha Shilingi za kitanzania bilioni 1.12 kililipwa kwa McDonald kwa mikataba iliyosainiwa mwaka 2008, 2009, 2010 na 2011 na TANESCO. Malipo hayo ni pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kiasi cha Shilingi za kitanzania milioni 168.86 ambacho hakikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

10.1.2 Matokeo ya Ukaguzi Maalum wa Awamu ya Pili

Awamu ya pili ya Ukaguzi Maalum ulikuwa kwa ajili ya kuangalia manunuzi yasiyofuata taratibu za manunuzi ya umma, uchunguzi rushwa, wizi wa umeme, maswala yanayohusu ajira, ununuzi na uuzaji wa mali za shirika, mgao wa umeme Tanzania na malipo yaliyofanyika kwa mawakili. Matokeo ya awamu ya pili ya ukaguzi maalum ni kama ifuatavyo:-

(i) Uchunguzi wa Manunuzi na Maswala ya Rushwa

TANESCO ilionekana kugubikwa na ukiukwaji uliokithiri wa kutozingatia Sheria ya manunuzi ya 2004 na kanuni zake za mwaka 2005 uliosababishwa na viongozi wa juu na kati wa Shirika. Mkurugenzi Mkuu wa Shirika akiwa ndiye mwenye maamuzi ya juu ya manunuzi alishindwa kuzuia ukiukwaji wa taratibu za sheria ya manunuzi na mara nyingi mkurugenzi mkuu aliidhinisha manunuzi ya chanzo kimoja au manunuzi yaliyozuia ushindani.

(a) Wizi wa Umeme

TANESCO bado haina mifumo inayoaminika na kuthibitika kwa ufasaha na ufanisi ili kuihakikishia uhalisia na usahihi kuwa inakusanya mapato yake yote kwa mwaka. Bado Shirika haliwezi kudhibiti mapato yake yote yatokanayo na mauzo ya umeme kupitia vituo vya mawakala wa LUKU Nchini. Pia TANESCO hufanya usuluhisho na uoanishi wa mauzo ya Wakala wa mauzo ya LUKU na kumbukumbu za TANESCO bila kutumia mifumo ya Kompyuta, ambapo huwa na makosa mengi na urahisi wa kugushi.

TANESCO haina kumbukumbu inayoonyesha ni idadi gani ya *''power token generation units (logic modules)''* zilizotolewa kwa wauzaji wa umeme. Shirika la umeme TANESCO halina kumbukumbu ya idadi ya modules 154 *(i.e Conlog: 80 Units and Actaris: 74 Units)* ambazo Shirika limekusanya. Shirika pia halina kumbukumbu za kuaminika na taarifa sahihi za mita za umeme zinazotumika na mashine za kuuzia umeme zilizowekwa nchi nzima

ikidhihirisha kuwepo kwa ukiukwaji wa usimamizi wa mifumo ya fedha, kanuni na mifumo ya udhibiti wa ndani.

(b) Mapitio ya Malipo Yaliyofanyika kwa Mawakili wa Shirika

TANESCO imeingia mikataba na makampuni mawili ya mawakili yakiiwakilisha TANESCO kwenye Kesi kubwa za kimataifa na kesi nyingine ambazo kwa ujumla zinaigharimu TANESCO zaidi ya kiasi cha Shilingi za kitanzania bilioni 10 kila mwaka.

Kampuni hizo za Mawakili zilipewa kazi na TANESCO bila kufuata taratibu za Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005. Pia inaonekana wazi kwamba malipo ya ada za huduma hiyo ya kisheria ni makubwa na hayana uhalisia. Pia Menejimenti ya Shirika haikuweza kubainisha thamani ya fedha iliyopatikana kutokana na huduma hiyo.

10.2 Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA)

Waziri Mkuu wa Tanzania alimuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kufanya ukaguzi Maalum juu ya taratibu zilizotumika wakati wa uuzwaji wa hisa za Shirika la UDA kwa mnunuzi wa hisa hizo na pia kufanya ukaguzi maalum wa Menejimenti ya UDA. Ukaguzi ulifanyika kutokana na maswali yaliyoibuka kwenye kikao cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Julai, 2011 kuhusiana na uuzwaji wa hisa za Serikali zilizokuwa katika Shirika la UDA na uuzwaji wa hisa ambazo zilikuwa bado hazijatengwa kwa mwekezaji.

Matokeo ya Ukaguzi Maalum wa UDA ni Kama Ifuatavyo:-

(a) Uuzwaji wa Hisa za UDA

UDA likiwa ni Shirika ambalo lilitengwa kwa ajili ya ubinafsishaji (Specified) chini ya usimamizi wa Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) ambalo lina jukumu la kuyaunda upya mashirika ya aina hiyo. Kwa mantiki hiyo CHC ndiyo iliyokuwa na mamlaka ya kuidhinisha uuzaji wa

hisa za UDA na siyo Bodi ya Wakurugenzi wa UDA kama ilivyofanyika. Mwezi Julai, 2010, CHC iliishauri Bodi ya Wakurugenzi wa UDA kupata idhini ya Serikali kabla ya kuendelea na uuzaji wa hisa za UDA. Bodi ya Wakurugenzi wa UDA iliendelea na uuzaji wa hiza hizo bila kupata kibali cha Serikali. Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) lilitoa ushauri kwa Bodi ya Wakurugenzi wa UDA kuwa njia ya wazi itumike kulingana na sheria ya Manunuzi ya Umma ili kumpata mwekezaji bora katika Shirika la UDA. Bodi ya Wakurugenzi wa UDA ilipuuza ushauri huo na kuendelea na uuzaji huo wa hisa za UDA kwa anayedaiwa kuwa mmiliki wa UDA bila kufuata taratibu za ushindani wa zabuni kama sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 inavyotaka.

- Hisa za Shirika la UDA zilithaminishwa na kuwa Shilingi 744.79 kwa kila hisa mwezi Octoba, 2009. Mwezi Novemba, 2010 thamani ya kila hisa ikawa 656.15. Hata hivyo, katika uuzaji huo, Bodi ya Wakurugenzi ya UDA ilitoa Punguzo la asilimia 60 kwa kila hisa kwa mwekezaji huyo (kwa tathimini ya bei ya hisa ya mwezi Octoba, 2009), bila kuwepo na sababu za kufanya hivyo. Kwa hiyo kila hisa ilitakiwa kuuzwa kwa Shilingi za kitanzania 298 kutoka Shilingi za kitanzania 744.79 kwa hisa moja ambayo ilithaminishwa mwezi Octoba 2009 na hivyo kupelekea UDA kupata hasara ya Shilingi za kitanzania bilioni 1.559.

  Vilevile ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya UDA illiingia mkataba wa kumuuzia Mwekezaji hisa 7,880,303 ambazo hazikugawiwa kwa bei ya Shilingi za kitanzania 145 kwa jumla ya Shilingi za kitanzania bilioni 1.142 badala ya Shilingi za kitanzania 744.79 kwa hisa kulingana na ripoti ya mshauri ambapo hisa hizo zingekuwa na thamani ya Shilingi za kitanzania bilioni 5.869 hivyo kulisababishia shirika hasara ya Shilingi za kitanzania Shilingi bilioni 4.727. Kwa kutumia bei ya hisa ya Shilingi za kitanzania 298 na 145 badala ya

Shilingi za kitanzania 744.79 kwa hisa moja iliisababishia serikali hasara ya jumla ya Shilingi za kitanzania bilioni 6.285 (sh.1,558,694,380 + shilling 4,726,526,936).

- Mnunuzi (mwekezaji) alilipa kiasi cha Shilingi 145 kwa hisa moja na kulipa jumla ya Shilingi za kitanzania milioni 285 kinyume na thamani ya hisa ya Shilingi za kitanzania 744.79 au 656.15 kwa hisa moja. Bodi ya Wakurugenzi ya UDA ikatoa punguzo la bei ya hisa hadi kufikia Shilingi 145 kwa hisa moja ukilinganisha bei ya punguzo iliyokuwa imeshafanyika mwanzoni ya Shilingi 298 kwa hisa moja ambapo inaonekana iliongeza tena punguzo la asilimia 53.

(b) Ripoti ya Makadirio ya Thamani ya Hisa na Mali za UDA
Ripoti ya makadirio ya thamani ya hisa iliyoandaliwa tarehe 30 Octoba, 2009 na tarehe 15 November, 2010, ilionyesha thamani ya mali za UDA ikiwa ni pamoja na mitambo na vifaa. Makadirio yaliyofanyika mwezi Agosti, 2009. Makadirio hayo hayakuainisha jumla ya mali za Shirika ukiondoa madeni yote (Net Assets). Pia haikuonyesha madeni ya Shirika ambayo ni jumla ya Shilingi za kitanzania milioni 473.241 ambayo yaliripotiwa kuwa yalishahamishiwa kwa Msajili wa Hazina. Haikuweza kufahamika ni sababu zipi zilizopelekea hisa za UDA kuuzwa kwa punguzo la asilimia 60 kutoka kwenye bei ya makadirio ya thamani ya kiasi cha Shilingi za kitanzania 744.79 kwa hisa.

(c) Kuthibitishwa Kiasi Kilicholipwa na Mnunuzi
Mkataba wa kuwasilisha hisa wa tarehe 11 Februari, 2011 unatamka kwamba mnunuzi (mwekezaji) atalipa jumla ya Shilingi za kitanzania bilioni 1.143 kama bei ya ununuzi ya hisa zote ambazo hazijatolewa na UDA ingawa mkataba haukuonyesha akaunti ya benki ambayo malipo yangelifanyika. Mnunuzi (mwekezaji) alilipa kiasi cha Shilingi za kitanzania milioni 285 katika akaunti namba 0J1021393700 ya benki ya CRDB inayomilikiwa na UDA.

Kulikuwa hakuna malipo mengine ya ziada yaliyofanywa na mwekezaji kuhusiana na ununuzi wa hisa za UDA. Malipo haya ni sawa na asilimia 24.9 ya bei ya kuuza iliyokubaliwa. Mwekezaji alidai kumlipa aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya UDA kiasi cha Shilingi milioni 320 kama ada ya kukubali kununua UDA katika mwaka 2009. Mwenyekiti wa Bodi alikubali alipokea kiasi cha Shilingi milioni 320 katika akaunti yake binafsi kutoka kwa Mwekezaji ikiwa kama ada ya ushauri alioutoa kwa Mwekezaji, ambayo ilizua mgongano wa kimaslahi.

(d) Utendaji Usiosahihi na Ukiukwaji wa Taratibu Katika Kuuza Hisa za UDA

Bodi ya Wakurugenzi ya UDA haikupata kibali kutoka kwa wanahisa wake kuhusiana na kuuza hisa zao hizo. Kwa mujibu wa sheria ya Mashirika ya Umma, kifungu Na. 257. Ibara ya 39(2) ya Sheria ya Mashirika ya Umma iko wazi kuwa PSRC/CFC inaweza ikaelekeza njia ya uundwaji upya wa mashirika ya umma ambayo itatekelezwa, uthamini wa mali, ualikaji wa wanunuzi wenye nia na shirika linalobinafsishwa na kubaini bei ya hisa na rasilimali zitakazouzwa.

Mchakato wa zabuni ya uuzaji wa hisa za UDA haukuwa wa kiushindani kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya umma Na.21 ya mwaka 2004 na kama ilivyopendekezwa na Shirika Hodhi la mali za serikali (CHC).

Ripoti ya uangalifu kuhusiana na Mwekezaji ilionyesha kwamba mwekezaji hakukamilisha masharti yaliyowekwa na PSRC kwa ajili ya kuwekeza kwenye shirika la UDA. Bodi ya Wakurugenzi ya UDA haikuzingatia kanuni na sheria tajwa hapo juu na iliendelea na uuzaji wa hisa hizo.

SURA YA KUMI NA MOJA

MATOKEO YATOKANAYO NA RIPOTI ZA UKAGUZI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

11.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo yatokanayo na ripoti za ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Tathmini imefanyika kwa kuangalia ripoti za ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilivyosaidia au matokeo yake katika ajenda za maendeleo ya nchi kwa kipindi kilichoanzia mwaka 2006/2007 hadi 2010/2011. Baadhi ya mapendekezo ambayo yalileta tija kwa taifa yameongelewa kwa kina kwenye ripoti hii. Mapendekezo muhimu yaliyotekelezwa kwenye kaguzi mbalimbali yamekuwa na manufaa kwenye mashirika husika. Kutokana na ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali uwajibikaji kwenye sekta ya umma umeongezeka kwa wale walio na madaraka kwa kujipima juu ya ufanisi wao kwenye majukumu waliyopewa na mamlaka za uteuzi. Kwa ujumla ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekuwa ni kama kioo ambapo mapendekezo yake yakitekelezwa kama yanavyokuwa yamependekezwa yatachangia kuliendeleza taifa.

Sura hii pia imejadili manufaa yaliyopatikana kwenye taifa letu kwa ujumla na siyo shirika moja moja kutokana na ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Yafuatayo hapa chini ni faida na matokeo juu ya mapendekezo ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekuwa akiyafanya kwa taifa kutokana na kaguzi za kanuni na taratibu, kaguzi za kupima ufanisi na kaguzi maalum kama sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 na sheria nyingine zinazompa madaraka.

11.1 Uanzishwaji wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali

Kupitia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Serikali ilishauriwa kuanzisha Divisheni yenye nguvu kamili ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani katika Serikali ambayo itakuwa mwangalizi wa shughuli za kitengo cha ukaguzi wa ndani nchini. Ilipendekezwa kuwa ripoti za wakaguzi wa ndani wa Serikali Kuu na ile ya Serikali za Mitaa ziwasilishwe kwa mkuu wa Divisheni ya Ukaguzi wa Ndani na kuacha desturi iliyozoeleka ya kuziwasilisha kwa wakuu wa idara husika katika ngazi za Serikali Kuu na zile za Mitaa ambao wamekuwa wakiidhoofisha shughuli za kitengo cha ukaguzi wa ndani. Divisheni ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani ilianzishwa ikiwa ni jitihada za Serikali za kutekeleza mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Divisheni ilianza kazi yake mnamo tarehe 6 Aprili, 2011 ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Bwana Mohammed A. Mtonga kuiongoza divisheni hiyo. Nina imani kwamba uwepo wa Mkaguzi Mkuu wa Ndani utasaidia kuimarika kwa kazi za kitengo cha ukaguzi wa ndani katika sekta ya Umma, na itaongeza nguvu ya kuepusha mianya ambayo imekuwa ikitumiwa kufanya ubadhilifu wa mali za umma. Utendaji kazi mzuri wa ofisi hii ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani utapelekea kuimarisha makusanyo ya Serikali na kupunguza matumizi yasiyo na tija ili kuongeza thamani ya fedha kwa matumizi ya mali za umma.

11.2 Kuundwa Upya kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina

Kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na 2008/2009 ilipendekezwa kuwepo na Ofisi ya Msajili wa Hazina inayojitegemea. Zaidi ya hayo ilipendekezwa kuwa maafisa waliopo Ofisi ya Msajili wa Hazina kutokuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi kwenye Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ili kuhakikisha swala la usimamiaji linatekelezwa ipasavyo kuepusha mgongano wa kimaslahi. Pendekezo hili lilitolewa ili

kuongeza nguvu za Msajili wa Hazina kusimamia Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma na pia kuzuia mgongano wa kifungu cha 3(1) – (2) cha Sura ya 418 ya Sheria ya Msajli wa Hazina kuhusu nguvu na kazi za Msajili wa Hazina kinachoeleza kwamba; "Sheria hii itakapoanza kutumika, kutakuwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Atakayeteuliwa na Rais kuwa Msajili wa Hazina na atakuwa mhimili wa ofisi kwa jina la Msajili wa Hazina na kwa jina hilo atakuwa na "perpetual succession" na muhuri rasmi (official seal) mwenye uwezo na mamlaka ya kununua, kuhifadhi, kusimamia na kuuza uwekezaji, kushitaki na kushitakiwa, kutekeleza uwekezaji (deeds and instruments), kuingia mikataba yeye mwenyewe na warithi wake wa ofisi, kutekeleza haki zote, alizopewa na uwekezaji yakiwemo madaraka ya kuhodhi mali zisizohamishika na mali nyinginezo, na kufanya mambo yote ya lazima kwa ajili ya kurahisisha na yatakayofanywa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake au ambayo yanahitajika kufanywa na Msajili wa Hazina kwa mujibu wa sheria hii au sheria nyinginezo".

Kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Ofisi ya Msajili wa Hazina iliundwa upya kwa kufanya mabadiliko ya sheria iliyoianzisha ofisi hiyo Sura ya 370.

11.3 Kuanzishwa kwa Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma (POAC)

Kati ya miaka ya sabini na tisini kulikuwa na kamati ya bunge iliyojulikana kama "POC" iliyokuwa na jukumu la kusimamia hesabu za mashirika ya umma. Pamoja na hayo katika kipindi cha zoezi la ubinafsishaji mnamo mwaka 2007 ilionekana kwamba kamati hiyo isingeweza kuwa na kazi kwa kufikiria kwamba mashirika ya umma yote yangebinafsishwa. Mwaka 2007, niliandaa kongamano la uwajibikaji. Kutokana na kongamano kulionekana kuwepo mahithaji ya kuundwa kwa kamati ya kudumu ya Bunge ambayo itawajibika kusimamia Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma nchini.

Mh. Spika wa Bunge alikubali ushauri na hivyo aliunda Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma. Kamati ilikabidhiwa majukumu hadi ilipovunjwa na Mh. Spika mnamo tarehe 8 Februari, 2013. Mfano kamati iliweza kuishauri serikali kuondoa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), TANESCO, NIC na STAMICO kutoka kwenye mashirika yaliyokuwa yametengwa kubinafsishwa kwa kusisitiza uwajibikaji na utawala bora wa mali za umma kwa wale walio na mamlaka. Kwa sasa mamlaka ya bandari ni miongoni mwa mashirika ya umma yenye fedha nyingi hali inayopelekea shirika kuchangia kwenye mfuko mkuu wa serikali. Kamati ilikuwa ikisisitiza uwajibikaji katika kazi na utendaji wa majukumu kwa pamoja katika nchi kabla ya kuondolewa kwake mwezi Februari, 2012 na majukwaa yake kupangishwa na Kamati ya Hesabu za Serikali kuu (PAC).

11.4 Mapitio ya Mkataba wa TICTS

Mamlaka ya Bandari Tanzania ilikodisha kitengo cha makontena kwa kampuni binafsi iitwayo Tanzania International Container Terminal Services (TICTS) kuanzia mwezi Mei mwaka 2000. Mkataba wa awali ulikuwa ni wa kipindi cha miaka 10, hata hivyo mwishoni mwa mwaka 2005, mkataba huo wa ukodishaji uliongezewa muda bila ya kufuata taratibu na kuwa miaka 15 kwa utaratibu wa Adendam Na.2.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliishauri Serikali kuptia upya mkataba wa TICTS kwa ajili ya kuondoa au kutafuta ufumbuzi wa huduma hafifu zilizosababisha utendaji wa mkataba kuwa chini ya kiwango cha 25% kwa sababu ya mlundikano wa makontena uliotokana na uhaba wa mitambo ya kupakua makontena uliosababishwa na TICTS kushindwa kuwekeza katika mitambo ya kisasa ya kupakia na kupakua makontena bandarini. Kupitia ushauri huu Serikali ilipitia upya mkataba huo wa kitengo cha kupakua na kupakia makontena cha TPA ambao ulikuwa

umekodishwa kwa kampuni binafsi ya TICTS na kufanya kuwa na manufaa zaidi kwa Serikali.

11.5 Kuongezeka kwa Idadi ya Mashirika ya Umma Yanayokaguliwa

Idadi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka kwa kuzingatia kwamba idadi ya mashirika yaliyoripotiwa katika hesabu za mwaka 2011/2012 ni mia moja na sabini na sita (176) ikilinganishwa na mia moja hamsini na nane (158) yaliyoripotiwa kwenye ripoti ya mwaka 2006/2007. Kufanikiwa katika hili kulitokana na mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliyependekeza ofisi ya Msajili wa Hazina ilinganishe rejista ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo serikali inamiliki hisa.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa idadi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuanzia ripoti ya mwaka 2006/2007 ilikuwa 158, wakati kwa mwaka 2007/2008 ilikuwa 164, 2008/2009 ilikuwa mashirika 166, pia mwaka 2009/2010 ilikuwa 170 huku mwaka 2010/2011 na mwaka 2011/2012 idadi ya mashirika ilikuwa sawa yaani 176. Mchanganuo unaoonyesha ongezeko la idadi ya mashirika umeonyeshwa kwenye grafu hapa chini;

Kielelezo Na 6: Ongezeko la Mashirika Yanayokaguliwa



Kwa kuyatambua na kufanya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambayo hayakuwa kwenye orodha ya Msajili wa Hazina imekuwa rahisi kwa ongezeko la mashirika kutoka 158 ya mwaka 2006/2007 hadi 176 katika mwaka 2011/2012. Pia, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameweza kupunguza matumizi yasiyo na tija ya mali ya umma, ongezeko la makusanyo ya mapato ya umma na kupunguza hasara za kizembe, udanganyifu, wizi, ulaghai, rushwa na kutokuwa na uaminifu unaohusiana na mali za umma.

11.6 Kutoyabinafsisha Baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Kupitia ripoti zake za kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekuwa akiishauri Serikali kufikiria aidha kuharakisha ubinafsishwaji wa mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji yaliyotoka PSRC na kuchukuliwa na CHC ili kuepuka uharibifu na uchakavu wa raslimali zinazomilikiwa na mashirika yaliyotengwa au Serikali kutoyabinafsisha na kuyaongezea mitaji ili yaanze kazi upya.

Mapendekezo hayo yalichukuliwa na Serikali ambapo baadhi ya mashirika ya umma yanayotoa huduma muhimu na nyeti kwa umma yaliondolewa katika orodha ya kubinafsishwa miongoni mwao yakiwa TANESCO, Mamlaka ya Bandari Tanzania, TPDC, NIC na STAMICO.

11.7 Uzingatiaji wa Sheria Mbalimbali na Uwasilishaji wa Taarifa za Hesabu kwa Wakati

Mafanikio juu ya uzingatiaji wa sheria mbalimbali umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kwenye Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Katika ripoti yangu ya kwanza ya mwaka 2006/2007 mashirika mengi yalikuwa hayazingatii taratibu/sheria mbalimbali ukilinganisha na sasa. Kwa sasa mashirika mengi ya umma yamekuwa yakizingatia sheria mbalimbali hali iliyochangiwa na uwepo wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008 ambayo haikuwepo wakati wa ripoti yangu ya kwanza ya mwaka ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma (2006/2007). Vile vile, utii wa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za 2005 ambayo imepunguza mianya iliyokuwa ikitumiwa na taasisi mbalimbali wakati wa manunuzi ya bidhaa na huduma, imetiliwa maelekezo na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Zaidi ya hapo, Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yamekuwa yakizingatia Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya kuwasilisha hesabu zao katika ofisi yangu kwa wakati kwa ajili ya ukaguzi, ambayo ni miezi mitatu (3) baada ya ile tarehe ya kufunga mwaka kama sheria inavyotaka ukilinganisha na zamani ambapo uwasilishwaji wa hesabu ulikuwa ukichelewa kwa asilimia kubwa. Mwenendo wa kuwasilisha taarifa za hesabu kwa wakati katika ofisi yangu kwa malengo ya ukaguzi na Wakurugenzi Wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka. Mwenendo unaonyesha kwamba Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma 19 hazikuwasilisha taarifa za hesabu zao kwa wakati katika mwaka 2007/2008, 10 kwa mwaka 2008/2009, na Mashirika

na Taasisi Nyinginezo za Umma 7 kwa mwaka 2009/2010. Hata hivyo, kutoka mwaka wa fedha 2010/2011 na 2011/2012 Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yote yaliwasilisha taarifa zao kwa wakati isipokuwa UDA na Benki ya Azania.

11.8 Utumiaji wa "IFRS na IPSAS Accrual" Kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Awali Mashirika mengi ya Umma na Taasisi Nyinginezo yalikuwa yakitayarisha taarifa za hesabu zao kwa kuzingatia Viwango vya Tanzania vya hesabu (TFAS) viliyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA). Kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serkali mabadiliko makubwa yamefanyika. Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yamehama kutoka mfumo wa TFAS na kutumia mojawapo ya viwango vya Kimataifa vya utayarishaji wa Taarifa za Hesabu (IFRS) au viwango vya Kimataifa vya uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS), kulingana na hali halisi na majukumu ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma husika. Uandaaji na uwasilishaji wa hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa kuzingatia IFRS au IPSAS ni jukumu la kisheria lililoainishwa kwenye Sheria zilizoanzisha Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, ikihimizwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uhimizaji huu, unatokana na uamuzi uliofanywa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na kuungwa mkono na Serikali kuanzia Julai 2004. Mashirika na Serikali kwa ujumla yalitakiwa kutengeneza hesabu zake kwa kufuata mojawapo ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa vya utayarishaji wa Taarifa za Hesabu (IFRS) kama vilivyotolewa na Bodi ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (IASB) au Viwango vya Kimataifa vya uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) kama vilivyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC). Kwa upande mwingine ukaguzi umekuwa unatumia viwango vya ukaguzi vya

kimataifa (ISA) kama vilivyotolewa na IASB na Asasi Kuu za Kimataifa za Ukaguzi (ISSAIs) kama iliyotolewa na Shirikisho la Asasi Kuu za Ukaguzi Duniani (INTOSAI). Zaidi ya hayo, ukaguzi pia, unatumia Miongozo na Viwango vilivotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

Utayarishaji na uwasilishaji wa taarifa za hesabu ambazo zinazingatia IFRS au IPSAS imesisitizwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

SURA YA KUMI NA MBILI

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

12.0 Mtazamo wa Jumla

Sura hii inatoa hitimisho na mapendekezo ya mambo yaliyojadiliwa katika ripoti hii na ambayo yanahitaji kutazamwa na kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika ya Umma. Mambo yote yaliyomo katika ripoti hii ni ya ujumla na ambayo ni muhtasari wa ripoti moja moja zilizopelekwa kwenye menejimenti za mashirika na mambo mengine muhimu yaliyojitokeza ambayo yanayofaa kwa ajili ya umma kuyafahamu.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa nguvu na Kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008 kutoa mapendekezo ambayo yatasaidia kuzuia au kupunguza matumizi ya fedha za umma yasiyo na tija. Mapendekezo yatakayowezesha kuongeza ukusanyaji wa mapato, na kuondoa hasara ambazo zinasababishwa na uzembe, kutojali, wizi, ukosefu wa uaminifu, ubadhilifu na vitendo vya rushwa katika mali za umma ili kuboresha utoaji wa huduma kwa umma.

Katika mwaka huu wa fedha, nilikagua taarifa za fedha za mashirika ya umma 174 na niliweza kukamilisha kaguzi kwa mashirika ya umma 126. Mashirika yalitengeneza taarifa zake za fedha kwa vipindi vinavyoishia tarehe 30 Septemba, 2011, 31 Disemba, 2011 na 30 Juni, 2012.

Kwa kutumia madaraka niliyopewa chini ya sheria ya ukaguzi Na.11 ya mwaka 2008 napenda kutoa mapendekezo kutokana na kaguzi zilizofanyika.

12.1 Maoni ya Ukaguzi na Ripoti Zilizokamilika

Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2013 nimefanikiwa kuhitimisha kaguzi 126 (71.6%) kati ya kaguzi 176

zinazotakiwa kukakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika kaguzi zilizokamilika, mashirika 95 maoni ya ukaguzi yametolewa na kusainiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wakati hesabu zilizokaguliwa za mashirika 31 zinasubiri kupitishwa na kusainiwa na Bodi za Wakurugenzi. Hesabu 62 (65.3%) za Mashirika ya Umma zilizosainiwa zilipata hati inayoridhisha wakati hesabu 23 (24.2%) zilipata hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo. Pia, hesabu za mashirika 2 (2.1 %) zilipata hati yenye mashaka, hesabu za mashirika 7 (7.4%) zilipata hati yenye shaka na masuala ya msisitizo, hesabu 1(1%) ilipata hati mbaya na hakuna shirika lililopata hati isiyoridhisha. Undani na mchanganuo wa maoni haya ya ukaguzi yameainishwa kwenye sura ya pili ya ripoti hii.

12.2 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ripoti Zilizopita

Napenda kutoa shukurani kwa juhudi ilizoonyeshwa na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma nilizozikagua, Bodi za Wakurugenzi, Kamati ya Mashrika ya Umma (POAC) na ofisi yangu katika kufanya ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi zake kwa utaalam, pamoja na mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti yangu ya mwaka ambayo yanahitaji jitihada za ziada kutoka Serikalini. Katika taarifa yangu ya mwaka uliopita mapendekezo mengi yalitolewa ila mengi bado hayajafanyiwa kazi na mengi yako kwenye hatua ya utekelezaji.

Napenda kukiri kupokea majibu ya serikali ya ripoti yangu iliyopita kupitia barua ya Mlipaji Mkuu wa Serikali yenye Kumb.Na. EB/AG/AUDIT/12/VOL.1/53. Majibu niliyoyapokea kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali hayajitoshelezi kujibu mapendekezo yote niliyoyatoa katika taarifa yangu ya mwaka ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ya mwaka 2010/2011. Kwa hali hiyo kuna haja ya Serikali kuingilia kati haswa kwa yale mapendekezo yanayohusiana na Utawala Bora. Nimezungumzia mapendekezo yanayohusu utawala bora zaidi kwa kuwa yasipotekelezwa ndio chanzo cha matatizo kwani

yanasababisha Mashirika ya Umma pamoja na Taasisi zake kutofikia malengo kutokana na muingiliano wa kimaslahi kati ya watendaji na waliopewa jukumu la usimamizi.

Napenda kuifahamisha Serikali kupitia Wizara mama za mashirika hayo, Bunge, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Ofisi ya Msajili, Bodi za Wakurugenzi za Mashirika husika na Watendaji Wakuu kuhakikisha mapendekezo ambayo hayajafanyiwa kazi yanatekelezwa na wafahamu kwamba wanawajibika kuhakikisha kuwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinafikia malengo waliojipangia.

Kitu muhimu ambacho kinaweza kuongeza motisha ya kazi katika ofisi yangu ni kutambua jitihada zinazofanywa na ofisi yangu. Hili litawezekana kwa kuona hatua zinachuchukuliwa katika kutekeleza mapendekezo ya taarifa zangu. Naamini Serikali pamoja na wadau wengine wa Mashirika ya Umma na Taasisi zake wanatambua umuhimu wa mapendekezo niliyotoa na kuchukua hatua haraka. Ikumbukwe kwamba nia na lengo la kutoa mapendekezo katika ripoti za kila mwaka ni kurekebisha kasoro zilizoonekana ili kuleta ufanisi na kufuata njia bora na sahihi za kuendesha Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

12.3 Masuala Muhimu Ambayo Hayakutolewa Taarifa Katika Ripoti ya Mwaka Uliotangulia

Dhamira ya Shirika la Nyumba la Taifa kuongeza nyumba itachangia kwenye Pato la Ndani la Taifa hadi asilimia 4% kwa mwaka 2014. Ongezeko la nyumba litasababisha ukuaji wa uchumi katika maeneo yafuatayo; Utengenezaji wa fursa za ajira zipatazo 200,000 za moja kwa moja na 500,000 ambazo sio za moja kwa moja. Kodi ya moja kwa moja ya ongezeko la Shilingi za kitanzania bilioni 120 kutokana na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), kodi ya majengo, kodi ya ardhi na kodi ya mapato. Ukuaji wa sekta ya fedha mikopo yenye riba ndogo na ukuaji wa sekta ya

bima. Uanzishwaji wa soko lililo tayari kwa ajili ya huduma za jamii na watoa huduma za miundombinu. Ukuaji wa sekta ya nyumba na makazi ya biashara kwa kiwango cha wastani wa 30% hadi 50% kwa mwaka kwa miaka 20 ijayo inawezekana endapo kutakuwa na mipango mizuri ya mikopo kwa kuweka dhamana ya nyumba ile ile iliyokopwa. (Mortgage Financing).

Shirika la Nyumba la Taifa linatakiwa kuzingatia yafuatayo; Kuweka uwiano mzuri ili shirika na biashara ya kupangisha nyumba peke yake bali liweke juhudi zaidi katika kujenga nyumba, Serikali ihimize juu ya wananchi kumiliki nyumba kwa kutumia fursa za sheria ya "Mortgage Financing (Special Provisions) Act and the Unit Titles Act of 2008" ambayo imeanza kutumika hivi karibuni, ili kujenga nyumba za bei nafuu kwa watu wenye kipato cha chini kwa nchi nzima, na kwa kuchukua fursa ya nyumba ambazo ziko kwenye maeneo mazuri ili kuendesha biashara na kupunguza matatizo ya makazi, kwa kushirikiana na wawekezaji (chini ya utaratibu wa PPP) ili kufanya uwekezaji kwenye miradi mikubwa, wakati huo huo kuhakikisha kwamba maslahi ya umma yanalindwa.

Kwa upande mwingine hospitali nyingi hususani zile zinazomilikiwa na Serikali mara nyingi huwa na uhaba wa dawa kutokana na fedha kidogo ambazo Bohari ya Madawa inapewa kutoka Serikalini. Kutokana na hali hii, inasikitisha kuona kuwa wahusika wameshindwa hata kufanya usuluhishi wa taarifa za madawa kati ya MoHSW na MSD na hivyo kuleta wasiwasi juu ya wahusika na utendaji wao wa kazi. Hivyo inapendekezwa kwamba, ufuatiliaji ufanyike mara kwa mara na maelezo ya kina ya fedha zote zilizolipwa kwa MSD kwa ajili ya ununuzi wa mdawa na usululushi wa taarifa ufanyike kwa pamoja ili kuhakikisha ni sahihi.

Napendekeza pia kuwa Menejimenti ya VETA ifanye upya mapitio ya muundo wa Shirika, uliopo kwa sasa ili

kuonyesha majukumu na mpangilio wa wafanyakazi na kuandaliwa kwa muundo wa shirika wenye mfumo mzuri wenye maelezo sahihi ya kazi kwa ajili ya nafasi muhimu. Pia Shirika liweke kanuni zenye uwiano mzuri kwa utumishi, ili kuboresha utendaji kazi wa wafanyakazi. Hii ni pamoja na kuanzishwa kwa mfumo wa uhasibu ambao unaunganisha ofisi zote ili kurahisisha ufanyaji kazi na utoaji wa maamuzi kupitia ngazi zote kwa haraka, ufanisi na ukamilifu.

12.4 Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba

Kuanzishwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma Namba 21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 kulitoa mwongozo wa kisheria na taratibu juu ya manunuzi katika sekta ya Umma. Pamoja na uwepo wa sheria, Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma bado kuna udhaifu katika kuzingatia matakwa ya sheria, kitu kilichonifanya niamini kwamba bado kuna uelewa mdogo wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005. Ukweli huu unathibitishwa na matokeo ya kaguzi nilizofanya kama yanavyoonekana katika sura ya tano ya ripoti hii. Hali kadhalika, ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ulihitimisha kwamba Mashirika ya Umma hayakuweza kufuata kikamilifu matakwa ya Sheria ya manunuzi ya umma ya 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 na kwamba baadhi ya manunuzi hayakufanyika kwa uwazi, ufanisi na manufaa ya kiuchumi ili kuweza kuleta tija na thamani ya fedha katika manunuzi ya Umma. Ukaguzi huu ulibaini kuwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hazikuweza kusimamia ipasavyo mikataba waliyoingia na kandarasi mbali mbali. Usimamizi wa mikataba bado ni tatizo linalohitaji kupewa mtizamo wa haraka katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ili thamani ya fedha ipatikane katika utekelezaji wa manunuzi kwenye Taasisi za Umma.

Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma iendelee kujenga uwezo ili kuhuisha uelewa na utekelezaji wa sheria ya manunuzi ikiwa ni pamoja na uwepo wa

msisitizo wa usimamizi wa mikataba katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

Ili kuhakikisha kunakuwepo na usimamizi sahihi wa mikataba ya manunuzi, menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma wanatakiwa kuhakikisha kwamba kunakuwepo na usimamizi wa karibu wa mikataba wanayoingia na kandarasi mbalimbali ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa na huduma stahiki katika taasisi zao. Pia menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinapaswa kufuatilia kwa karibu sana watoa huduma na Wakandarasi ili kuhakikisha mikataba inatekelezwa kulingana na makubaliano na masharti yaliyomo kwenye mkataba. Aidha, kwa watumishi wote watakaohusika moja kwa moja katika usimamizi usioridhisha wa mikataba hatua stahiki za kisheria zichukuliwe dhidi yao kama inavyoelekeza sheria ya manunuzi ya Umma.

Watendaji wakuu katika mashirika na kitengo cha manunuzi lazima watimize wajibu wao katika kuhakikisha kuwa sheria ya manunuzi inafuatwa kikamilifu. Ni ukweli usiopingika kwamba mpango wa manunuzi katika Mashirika ni muongozo wa dhati katika kutekeleza manunuzi kwenye sekta za Umma. Ninashauri menejimenti za Mashirika ya Umma kuwa makini katika kuandaa mipango ya manunuzi kwenye taasisi zao kwa kutazama matakwa ya kifungu cha 45 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni ya 46, 48 na 49 za sheria hiyo. Pia nashauri Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuhakikisha mpango wa manunuzi unafanyiwa mabadiliko kila mara pale inapobidi ili kuendana na uwezo wa bajeti. Vitengo vya manunuzi vishirikishwe ipasavyo katika hatua zote za manunuzi na vihakikishe ripoti zote za manunuzi zinaandaliwa kama inavyoelekezwa kwenye sehemu ya 35 (o) ya sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na kuziwasilisha kwenye bodi ya zabuni na menejimenti kwa ajili kujadiliwa na kupewa muongozo na kuidhinisha.

Pia ninashauri wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma wahakikishe kwamba bodi za zabuni, vitengo vya manunuzi, kamati za tathmini na watumiaji wa huduma au bidhaa wanafanya kazi bila kuingiliana kama inavyoelekezwa kwenye sehemu ya 38 ya sheria ya manunuzi ya mwaka 2004. Mashirika ya Umma yanapaswa wakati wote kutii viwango vilivyowekwa chini ya jedwali la pili la Kanuni za Sheria ya Manunuzi kwa tangazo la serikali namba 97 na 98 katika kufanya maamuzi ya njia sahihi za kufanya manunuzi. Halikadhalika vitengo vya manunuzi vihakikishe kuwa viwango vilivyoanishwa na sehemu (b) ya jedwali la kwanza la kanununi za sheria ya manunuzi kwa tangazo la serikali namba 97 vinazingatiwa ipasavyo.

12.5 Usimamizi wa Rasilimali

Usimamizi wa rasilimali wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma katika mapitio ya mwaka ulionekana kuwa na madhaifu kadha wa kadha ikiwa ni pamoja na;

Hali tete ya mwelekeo wa kifedha wa TBC, PSPF, BAKITA, MUWASA na TLSB, kuchukuliwa umiliki wa kiwanja Na. 482 cha Bodi ya Sukari, rasilimali zilizopo katika Chuo Kikuu cha Dodoma hazijajumishwa katika vitabu vya hesabu vya Chuo, ukosefu wa umiliki halali wa mali, udhaifu katika usimamizi wa washikadau wa CHC na usimamizi hafifu wa CHC kwa wakopaji wa NBC ya zamani. Udhaifu mwingine uliobainika ni pamoja na deni la muda mrefu lililotokana na bidhaa zilizokuwa zinasafirishwa za Mamlaka ya Bandari Tanzania, kontena za vitabu ambazo hazijatolewa Bandarini kwa muda mrefu na Bodi ya Huduma ya Maktaba Tanzania tangu mwaka 2009 na deni chechefu la City Water bado lipo kwenye vitabu vya mahesabu vya DAWASCO. Madhaifu mengine ni kukithiri kwa taratibu zisizo sahihi katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania na pia kuongezeka kwa matukio ya uwindaji haramu katika mbuga za TANAPA.

Serikali, Bodi za Wakurugenzi, Maafisa watendaji wa mashirika wahakikishe kwamba maamuzi sahihi

yanachukuliwa katika ufuatiliaji wa karibu wa kurudisha rasilimali za Mashirika ambazo zimemilikiwa na kutumiwa isivyo halali.

Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zihakikishe kwamba kunakuwa na umiliki halali wa mali zake. Serikali ichukue hatua muafaka kuhusiana na uwezo wa nafasi ya kifedha za TBC, PSPF, BAKITA, MUWASA na TLSB.

Pia ninapendekeza kwamba Bodi ya Wakurugenzi ya PSPF iweke mpango madhubuti wa kujikwamua katika hasara ambayo bado ni kubwa ikilinganishwa na thamani halisi ya rasilimali ya Shilingi za kitanzania bilioni 1.086 katika kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2012.

Serikali na Mifuko ya Pensheni inapaswa kukubaliana katika umiliki wa rasilimali za Chuo Kikuu cha Dodoma ili kuruhusu uwekwaji kumbukumbu wa mali katika vitabu vya mahesabu ya Chuo. Mikataba yote ya mkopo wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma inapaswa kurekebishwa na kuhakikisha vifungu vyote vya kisheria vyenye utata vinarekebishwa.

Zaidi ya hayo, Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika Hodhi la Mali za Serikali ihakikishe kuwa kuna usimamizi mzuri wa taarifa za akaunti za wateja ili maafisa wasio waaminifu wasipate nafasi ya kula njama ya kubadilisha usahihi wa taarifa hizo na kufanya Shirika kupata hasara.

Pia ninapendekeza kwamba Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zihakikishe kunakuwepo mchanganuo uliowazi wa uondoaji madeni chechefu ukiambatana na ushahidi wa kufutwa kwa madeni hayo.

Zaidi ya hayo, Serikali, Bodi za Wakurugenzi, Maafisa Watendaji wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

wahakikishe kuwa hatua na juhudi za kutosha zinachukuliwa katika kukusanya madeni ya muda mrefu na usimamizi mzuri wa vifaa ghalani unakuwepo. Kwa upande mwingine, Bodi ya Wakurugenzi ya TLSB na TRA wahakikishe muafaka wa makontena mawili ya vitabu vya shule yaliyokwama bandarini unapatikana. TANAPA ihakikishe kwamba doria ya askari kwa ajili ya kulinda wanyama pori hususani Tembo inaboreshwa ili kupunguza idadi ya vitendo vya uwindaji haramu mbugani na kuhakikisha lengo la TANAPA la kuhifadhi Mbuga za Taifa linafanikiwa.

12.6 Usimamizi wa Rasilimali Watu

Kama ilivyoelezwa katika muhtasari kwenye sura ya saba ya ripoti hii, mapungufu mbalimbali yaliyobainika wakati wa ukaguzi yanapaswa yapatiwe ufumbuzi kwa wakati ili kuongeza tija katika utendaji. Mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa Rasilimali watu ni pamoja na kutokuwepo uwazi wakati wa kuajiri kwa baadhi ya mashirika, ucheleweshwaji wa kupeleka michango ya pensheni, mapungufu katika upimaji kazi wa watumishi, majalada ya watumishi kutokuwa na kumbukumbu muhimu, mashirika kuwa na nafasi wazi ambazo ni muhimu, mashirika kutokuwa na mpango wa mafunzo, baadhi ya mashirika kutokuwa na mpango wa kukasimiana madaraka na utendaji usioridhisha.

Bila kuyafanyia kazi mapungufu haya, ari na motisha ya watumishi yanaweza kupungua hivyo kupunguza utendaji kazi yakinifu katika Mashirika ya Umma. Ili kuboresha utendaji, menejimenti za Mashirika ya Umma zihakikishe kunakuwepo uwazi na haki wakati wa kuajiri watumishi, michango ya watumishi iwasilishwe kwa wakati kwenye mifuko ya pensheni, upimaji kazi wa watumishi ufanyike kwa wakati, nafasi muhimu za ajira ambazo ziko wazi kwa muda mrefu inashauriwa zijazwe, mashirika yawe na mpango wa mafunzo utakaokuwa dira ya kupeleka watumishi mafunzo mbalimbali.

12.7 Utawala Bora Katika Sekta ya Umma

Utawala bora katika sekta ya umma ni muhimu ili kuhakikisha mashirika ya umma yanaendeshwa vizuri kwa kuzingatia utawala bora na kama taratibu zinavyoelekeza. Kuwepo na mgawanyo wa madaraka kati ya watendaji na waangalizi na wasimamizi kusaidia kuondoa mgongano wa kimaslahi na kuboresha utendaji kazi katika mashirika ya umma. Mashirika ya Umma ni taasisi huru zinazojitegemea ambazo zinahitaji kutoingiliwa na wizara mama katika uendeshaji ili ziweze kuwajibika kwa maamuzi wanayoyafanya katika shughuli za kiutendaji.

Katika baadhi ya mashirika ya umma, zimejitokeza kasoro kadhaa katika utendaji wa vitengo au idara za ukaguzi wa ndani na kamati za ukaguzi. Menejimenti za mashirika zinakumbushwa tena kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani na utendaji wa kamati za ukaguzi za mashirika ili kuhakikisha udhibiti wa mifumo ya ndani na hivyo kulinda rasilimali za mashirika ya umma.

Kwa upande mwingine, kuchelewa kuteua bodi za wakurugenzi za mashirika ya umma kunaathiri maamuzi muhimu katika mashirika ya umma na kwa hiyo kuwa na matokeo yasiyoridhisha katika utendaji kazi wa mashirika. Kwa ofisi yangu, ukosefu wa bodi za wakurugenzi umekuwa kikwazo kwangu kukamilisha baadhi ya kaguzi za mashirika kwani kabla sijatoa maoni yangu katika ripoti husika, kwani sharti Bodi iwe imeridhia hesabu zake. Kwa hiyo, na kwa kuzingatia mapendekezo yangu katika ripoti zilizotangulia, ninarudia kuiasa Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwa na rejesta inayoonyesha vipindi vya Bodi zilizoko madarakani kumalizika ili kuwa na mpango madhubuti wa uteuzi wa Bodi kabla ya vipindi vyake kuisha.

Mwingiliano wa taasisi zilizoko nje ya mashirika ya umma, mathalani wizara inabidi zitazamwe utazamwe. Masuala yanayohusu shughuli za kila siku za kiutendaji inabidi ziachwe zifanywe na menejimenti, na Bodi zifanye tathmini ya utendaji wa menejimenti katika kufikia malengo

yaliyowekwa katika mpango kazi wa mwaka na mpango mkakati wa shirika.

12.8 Uwekezaji wa Serikali na Mchakato wa Ubinafishaji

Uendeshwaji wa mashirika ya umma kwa mwaka unaohusika umepimwa kwa ubora wa hesabu zake hasa kwenye Vitega uchumi vya ndani ambavyo viliongezeka kwa Shilingi za kitanzania trilioni 1.939, ikiwa ni ongezeko kutoka Shilingi za kitanzania trilioni 10.276 kutoka tarehe 30 Juni, 2011 hadi kufikia Shilingi za kitanzania trilioni 12.215 katika mwaka huu wa ukaguzi. Ongezeko kubwa limetokana na kuongezeka kwa Mashirika ya Umma/ Taasisi za serikali kutoka 204 kwa mwaka 2010/2011 hadi 213 kwa mwaka 2011/2012. Mapato ya Serikali yaliyokusanywa na Msajili wa Hazina kama gawio, malipo ya mikopo na mapato mengineyo yaliongezeka kwa Shilingi za kitanzania bilioni 179.3 ambayo ni sawa na asilimia 622.8 kutoka Shilingi za kitanzania bilioni 28.8 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 mpaka kufikia Shilingi za kitanzania bilioni 208.1 katika mwaka huu wa ukaguzi, ongezeko hilo limesababishwa na utendaji mzuri wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, usisitizaji katika utekelezaji uliofanya ongezeko la mapato na ulipaji wa madeni ya Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa Serikali.

Menejimenti za mashirika haya lazima zisimamiwe kuhakikisha utoaji wa huduma za uhakika na za kuaminika. Panapotokea matatizo ya kifedha, Serikali ihakikishe inatoa msaada unaohitajika na kwa wakati.

Masuala ya Ubinafsishaji

Serikali na wadau wengine ambao wanahusika moja kwa moja kwenye mchakato wa ubinafsishaji, ni lazima wajitahidi kuhakikisha kwamba shughuli zote za ubinafsishaji zinafikia muafaka. Inavyoonekana umiliki wa CHC unaelekea kufika mwisho, kwa hiyo Serikali inapaswa ifanye utaratibu wa jinsi shughuli za ubinafsishaji zitakavyotekelezwa baada ya uhai wa CHC kufikia ukomo. Pia Serikali inatakiwa kupitia upya uamuzi wake kwa

kuongeza muda wa umiliki au kuandaa mrithi wa shughuli zote za ubinafsishaji ili zifanyike kama zilivyokusudiwa.

Shirika limejipanga kutumia mikakati mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake. Baadhi ya mikakati hiyo ni kama ifuatayo:

- Kuongeza juhudi katika kukusanya madeni na pia kuwatumia Mawakala binafsi katika ukusanyaji madeni kwa lengo la kuongeza makusanyo kutokana na madeni hayo kuwa ya muda mrefu.
- Kuuza majengo yaliyobakia kwa kutumia taratibu na kanuni zilizoko katika sheria ya Manunuzi.
- Kusimamia kwa ukaribu shughuli za ufilisi wa makampuni 18 yaliyobakia.
- kuimarisha usimamiaji na tathmini ya matokeo baada ya ubinafsishaji kufanyika ili kujua kiwango cha utekelezaji wa majukumu ya Wawekezaji kulingana na mikataba ya ubinafsishaji.
- Kufuatilia na kukamilisha uandaaji wa hati za ardhi kwa majengo na viwanja vilivyouzwa ili kukabidhi kwa wanunuzi na kuharakisha ulipwaji wa salio la fedha za mauzo ya mali hizo.
- Pamoja na kuweka mipango na mikakati ya kuhakikisha shughuli zilizobaki za ubinafsishaji zinakamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2014 kama Serikali inavyotarajia; Hali halisi inaonyesha kuwa baadhi ya kazi zilizobaki haziwezi kukamilika katika kipindi cha uhai wa Shirika lakini pia jukumu la upembuzi ni endelevu, hivyo Serikali lazima iandae utaratibu wa utekelezaji wa shughuli zitakazo baki baada ya uhai wa CHC kufikia ukomo.
- Mapendekezo yanayotokana na taarifa za upembuzi yafanyiwe kazi na Wizara mama ili Serikali ishauriwe ipasavyo na iweze kuchukua hatua stahiki kwa Wawekezaji ambao wameshindwa kutekeleza masharti ya mikataba ya mauzo kwa wakati.

- Ifanyike tathmini ya uwezo na utendaji wa Shirika kwa maana ya Rasilimali watu, vitendea kazi na mfumo wa utendaji (Capacity and competence assessment);
- Kufanyike mapitio ya sera ya ubinafsishaji (Review of the Privatization Policy); Kufanyike mapitio ya sheria na taratibu za CHC pamoja na Sheria ya Mashirika ya umma (Public Corporations Act) kuhusu suala la ubinafsishaji wa mashirika ya umma;
- Serikali itunge sheria na itoe utaratibu ambao utawataka Wakaguzi (external auditors) wa mashirika yaliyobinafsishwa kutoa taarifa ya utekelezaji wa mipango ya uwekezaji kulingana na mikataba ya mauzo.

12.9 Matokeo ya Ukaguzi Maalum

Katika awamu ya kwanza ya ukaguzi Maalum wa TANESCO; Kampuni za Santa Clara Supplies Company Limited na McDonald Live Line Technology Limited kuwa na uhusiano wa kibiashara na TANESCO, imeonekana kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO alikuwa na mgongano wa kimasilahi na Kampuni zote mbili; Kwa hiyo aliende kinyume na kifungu namba 2.2 cha kanuni za maadili za TANESCO na kifungu namba 6(a) cha Sheria ya Kanuni za Maadili za Viongozi wa Umma ya mwaka 1995.

Awamu ya pili ya ukaguzi Maalum wa TANESCO; ilionekana kwamba; TANESCO ilikithiri kwa ukiukwaji wa Sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005. Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO akiwa kama mwenye maamuzi ya juu ya kufanya manunuzi ya Shirika alishindwa kuzuia ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi katika Shirika, na mara nyingi aliidhinisha manunuzi ya chanzo kimoja na manunuzi yaliyozuia ushindani. Manunuzi ya TANESCO mara nyingi hayakuzingatia makadirio ya bei za zabuni kutoka kwa Wahandisi wake katika kufanya maamuzi sahihi ya bei bora za zabuni.

Kwa hiyo inashauriwa kwamba, Bodi ya Wakurugenzi wa TANESCO inatakiwa; kuchukua hatua za kinidhamu na za kisheria kwa wote waliohusika na manunuzi yanayotia shaka kwa kukiuka taratibu za Sheria ya Manunuzi na uzembe katika kutimiza wajibu kazini. Bodi inapaswa iwaripoti kwa mamlaka inayosimamia udhibiti wa Sheria ya manunuzi (PPRA) na wale wote walioshiriki katika kufanya manunuzi yasiyofata utaratibu ikiwa ni pamoja na watumishi wa TANESCO na wote waliofanya Mauzo hayo kwa Shirika, kama inavyotakiwa na Kifungu namba 16 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 kwa ajili ya kuchukuliwa hatua. Bodi itafute ushauri wa kisheria juu ya kuwachukulia hatua za kinidhamu waliohusika kwenye Manunuzi hayo; Bodi pia ikijengee uwezo kitengo cha Manunuzi na mfumo mzima wa manunuzi na kuimarisha udhibiti wa ndani ya Shirika ili kuhakikisha kuwepo kwa umadhubuti na ufanisi ndani ya Shirika kuanzia katika Kitengo cha Manunuzi, Kamati ya Zabuni, Kamati ya Tathmini na kamati za Ukaguzi wa Vifaa na kamati nyingine zote. Bodi ya TANESCO inatakiwa pia kuunda upya kitengo cha Manunuzi na kamati zake zote na kuhakikisha zinakuwa na wafanyakazi wa kutosha na wenye uwezo na sifa stahiki. Mwisho Bodi inatakiwa iripoti kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DCI) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB) yale yote yaliobainika kwa ajili ya uchunguzi zaidi wa kubaini kuwepo kwa rushwa na ubadhilifu.

Ukaguzi Maalum wa Shirika la Usafiri Dar es Salaam kwenye uuzaji wa hisa kwa mwekezaji; ulibaini mapungufu yafuatayo; Kulikuwa na kukithiri kwa utaratibu usioridhisha katika uuzwaji wa hisa kwa mwekezaji. Bodi ya Wakurugenzi wa UDA haikufuata ushauri kutoka CHC wa kuomba kibali cha Serikali na kutumia utaratibu wa ushindani kabla ya kuendelea na mauzo hayo. Hisa ziliuzwa kwa kiasi cha Shilingi za kitanzania 145 kwa hisa moja. Kiasi cha Shilingi za kitanzania milioni 285 kililipwa na mwekezaji ikiwa ni asilimia 24.9 ya jumla ya bei ya makubaliano ya Shilingi za kitanzania bilioni 1.143. Kiasi

hicho kililipwa tofauti na thamani ya Shilingi za kitanzania 744.79 kwa kila hisa kutokana na ripoti ya makadirio ya thamani iliyofanyika Octoba, 2009. Hapakuwepo na sababu iliyopelekea bei hiyo ya hisa kupata punguzo la asilimia 80.54. Kiasi ambacho bado hakijalipwa na mwekezaji ni Shilingi za kitanzania milioni 857.64. Serikali ifikirie kuwachukulia hatua za kisheria wale wote waliohusika na uuzaji wa hisa za UDA bila kufuata taratibu za Sheria ya Manunuzi na taratibu za ubinafsishaji.

12.10 Matokeo Ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mashirika ya Umma kwa mara ya kwanza ilitolewa mwaka 2006/2007. Kuanzia kutolewa kwake kwa mara ya kwanza, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali imeibua mapendekezo mengi ambayo yalihitaji umakini wa Serikali, Bunge na menejimenti ya mashirika ya umma. Mapendekezo hayo yalitolewa kutafuta ufumbuzi wa hoja zilizoainishwa. Nimekuwa nikiguswa na imani ya Serikali kwa jinsi ambavyo imekuwa ikijihusisha na utekelezaji wa mapendekezo yangu. Hii imepelekea mabadiliko chanya kwenye utendaji wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, ambayo yameongeza thamani na umuhimu kwenye utoaji wa huduma za umma. Mfano wa mambo ambayo yameongeza thamani yanahusisha uanzishwaji wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, kuundwa upya kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina, kuanzishwa kwa kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma (POAC), Mapitio ya mkataba wa TICTS, kuongezeka kwa idadi ya mashirika ya umma yanayokaguliwa, kutoyabinafsisha baadhi ya Mashirika, na utii wa sheria mbalimbali. Kwa mtazamo huu, napendekeza ari ya kushughulikia mapendekezo ambayo yapo kwenye ripoti zangu za mwaka iongezeke kwa maendeleo ya taifa. Tuungane katika kutafuta suluhisho la kudumu kwa matatizo yanayoyakabili mashirika yetu.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho I

Orodha ya Kampuni Binafsi za Ukaguzi

S/N	Name of Audit Firm
1.	AA – Adolph Associates
2.	ABA Alliance
3.	AMAS Associate
4.	ABS Consultants
5.	ATEKAY Accountants and Auditors
6.	Auditax International
7.	BK Associates & David Malishee
8.	BAAS Associates & EVK
9.	Citizen Certified Partners Consortium
10.	Co-operative Audit and Supervision Corp
11.	CT & Associates & Chabegan & Associates
12.	BDO Tanzania
13.	Deloitte & Touche
14.	Ernst & Young
15.	Elite Financial Managers
16.	Fincare & Company
17.	Global Finance and Business Solution
18.	Globe Accountancy Services
19.	Global Auditing and Management Solution
20.	ISM Consultants
21.	INNOVEX Auditors
22.	KPMG
23.	Martec & Company
24.	MATSAB & Company
25.	MEKONSULT Auditors
26.	MGK Certified Public Accountants
27.	MM Micro Business Consultants
28.	MURL-AATEC Associates
29.	PAN Associates
30.	Paul Clem Associates
31.	PIMA ASSOCIATES
32.	PKF Tanzania
33.	PricewaterhouseCoopers
34.	Philips & Company
35.	Quintex Financial Services
36.	R&S Associates
37.	Reliable Consultants,
38.	RS & Partners
39.	SBC Consultancy Services
40.	Shebrila & Co
41.	SMW
42.	TAB Consultants
43.	Tanna Sree Kumar Co.
44.	TAG System Associates
45.	Tax Pro Associates
46.	TAC Associates
47.	TANSCOTT
48.	TMC Associates/TOP Consultants Consortium
49.	Trion & Company
50.	VA Business Assurance Services
51.	WISCON Associates

Hali halisi ya Ukaguzi

A	Taasisi za Fedha, Mifuko ya Pensheni na Mashirika Mengineyo	Hesabu Zimepo kelewa	Ukaguzi Unae-ndelea	Kuhakiki Ubora wa Ripoti	Hesabu Zinasubiri Kupiti-shwa na Bodi ya Wakuru-genzi	Ripoti Zilizokami lika	Maoni
1.	Benki Kuu ya Tanzania (BOT)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
2.	Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa (GEPF).	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
3.	Bodi ya Mfuko wa Bima za Amana	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
4.	Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
5.	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
6.	Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji Tanzania(EPZA)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
7.	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
8.	Mfuko wa Mafao ya Wafanyakazi wa Umma (PSPF)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
9.	Benki ya Raslimali Tanzania (TIB)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
10.	Benki ya Posta Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
11.	Benki ya Twiga	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
12.	Mfuko wa Kuwekeza Tanzania (UTT)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
13.	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
14	Shirika la bima la Taifa (NIC)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
15.	Soko la Hisa Dar es salaam (DSE)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
16.	Mamlaka ya Udhibiti wa Hisa na Mitaji (CMSA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
17.	Bohari ya Madawa (MSD)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
18.	Shirika la Utangazaji Tanzania(TBC)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
19.	Shirika la Masoko ya Kariakoo	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
20.	Mamlakaa ya Hifadhi ya Ngorongoro	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
21.	Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
22.	Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
23.	Kampuni ya Mbolea	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

	Tanzania.						
24.	"Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization" (TEMDO)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
25.	Shirika la Mafuta Tanzania (TPDC)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
26.	Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
27.	Shirika la Magazeti Tanzania.	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
28.	Shirika la Nyumba Tanzania	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
29.	Ubungo Plaza Co. Ltd	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	-
30.	Jengo la IPS la NHC/PPF	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
31.	Shirika la posta Tanzania	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
32.	Benjamin William Mkapa Foundation	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
33.	Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma(CHC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
34.	Shirika la Hifadhi ya Bahari Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
35.	Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
36.	Hifadhi za Taifa za Tanzania (TANAPA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
37.	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA),	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
38.	Kituo cha Uwekezaji Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
39.	Kampuni ya Kusimamia Raslimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
40.	Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
41.	Mamlaka ya Bandari Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
42.	Mamlaka ya Elimu Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
43.	Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
44.	Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
45.	Kampuni ya Maendeleo ya Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
46.	Baraza la Wafugaji Ngorongoro	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
47.	Benki ya Azania	Hapana	-	-	-	-	
B.	**Bodi, Mabaraza, Kamisheni na Mamlaka za udhibiti**	**Hesabu Zimepo kelewa**	**Ukaguzi unae-ndelea**	**Kuhaki-ki Ubora wa Ripoti**	**Hesabu zinasu-biri Kupiti-shwa na Bodi ya Wakuru-**	**Ripoti Zilizokami lika**	**Maoni**

					genzi		
1.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Wasanifu majenzi (AQRB)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
2.	Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi (NLPC)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
3.	Tume ya Ushindani (FCC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
4.	Mamlaka ya Usajili wa Bima Tanzania(TIRA)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
5.	Shirika la Nguvu za Atomiki	Ndiyo	-	-	-	-	
6.	Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
7.	Baraza la Taifa la Biashara Tanzania (TNBC)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
8.	Baraza la Kiswahili Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
9.	Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma (CDA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
10.	Bodi ya Usajili ya Wakandarasi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
11.	Bodi ya Usajili ya Wahandisi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
12.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
13.	Baraza la Sanaa Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
14.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
15.	Bodi ya Manunuzi (PSPTB)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
16.	Baraza la Ujenzi la Taifa (NCC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
17.	Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
18	Baraza la Taifa la uwezeshaji wa kiuchumi (NEEC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
19	Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
20	Baraza la Michezo Tanzania	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
21.	Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
22.	Bodi ya Pareto Tanzania	Ndiyo	Ndiyo	-		-	
23.	Mamlaka ya maendeleo ya Bonde la Rufiji (RUBADA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
24.	Bodi ya sukari Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
25.	Bodi ya Tumbaku Tanzania	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
26.	Bodi ya katani Tanzania	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
27.	Bodi ya Korosho Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

28.	Shirika la Viwango Tanzania (TBS)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
29.	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Na Majini (SUMATRA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
30.	Mamlaka ya anga Tanzania (TCAA)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
31.	Bodi ya Kahawa Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
32.	Makumbusho ya Taifa	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
33.	Mamlaka ya Kudhibiti manunuzi ya Umma (PPRA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
34.	Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo -	
35.	Bodi ya Pamba Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
36.	Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
37.	Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
38.	Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania(TFNC)	Ndiyo	-	-	-		
39.	Bodi ya Chai Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
40.	Bodi ya Utalii Tanzania	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
41.	Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
42.	Shirika la Haki Miliki Tanzania (COSOTA)	Ndiyo	Ndiyo	-	-		
43.	Bodi ya Maziiwa Tanzania	Ndiyo	-	-	-	-	
44.	Bodi ya Usajili wa Maghala Tanzania (TWLB)	Ndiyo	-	-	-	-	
45.	Bodi ya Biashara ya Nje (TANTRADE)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
46.	Mamlaka ya Udhibiti ya Mifuko ya Kijamii Tanzania (SSRA)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
47	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
48.	Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri Majini na Nchi Kavu. (SUMATRA CCC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
49.	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	

C.	Vyuo vya Elimu ya Juu, Tafiti na Mafunzo	Hesabu Zimepo kelewa	Ukaguzi Unaend elea	Kuhakiki Ubora wa Ripoti	Hesabu Zinasu-biri Kupitishwa na Bodi ya Wakuru-genzi	Ripoti Zilizokami lika	Maoni
1.	Chuo Kikuu cha Ardhi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
2.	Chuo Cha Elimu ya Biashara	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
3.	Taasisi ya Taifa ya Sukari	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
4.	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania(TCU)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
5.	Chuo cha Teknolojia Dar es salaam	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
6.	Shirika la Tija la Taifa (NIP)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
7.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
8.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
9.	Chuo cha Uhasibu Arusha	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
10.	Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
11.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
12.	Chuo cha Usimamizi wa Fedha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
13.	Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
14.	Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
15.	Shirika la Elimu Kibaha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
16.	Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
17.	Chuo Kikuu Cha Mkwawa	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
18.	Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Kijijini CARMATEC	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
19.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Masomo ya Biashara Moshi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
20.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi ya Afya Muhimbili (MUCHS)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
21.	Chuo cha Wanyama Pori (MWEKA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
22.	Chuo Kikuu cha Mzumbe	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
23.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa	Ndiyo	-	-	-	-	
24.	Chuo cha Usafirishaji (NIT)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
25.	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
26.	Chuo Kikuu Cha	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	

	Sokoine.						
27.	Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
28.	Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
29.	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
30.	Chuo Kikuu cha Dodoma	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
31.	Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
32.	Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
33.	Taasisi ya Utafiti na Uvuvi Tanzania (TAFIRI)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
34.	Taasisi ya Utafiti ya Wanyama Pori (TAWIRI)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
35.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (TPRI)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
36.	Centre for Foreign Relation	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
37.	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
38.	Shirika la Kutengeneza Magari (NYUMBU)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
39.	Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
40.	Chuo cha Ufundi Arusha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

D.	Mashirika ya Kutoa Huduma	Hesabu Zimepo kelewa	Ukaguzi Unaend elea	Kuhakiki Ubora Ripoti	Hesabu Zinasu-biri Kupitishwa na Bodi ya Wakuru-genzi	Ripoti Zilizoka milika	Maoni
1.	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
2.	Mamlaka ya udhibiti wa Nishati na maji (Ewura)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
3.	Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura CCC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
4.	Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
5.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Bukoba	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
7.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Babati	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
11.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Iringa	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
12.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kigoma	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
13.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
14.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mbeya	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
15.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

	Morogoro						
16.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
17.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Moshi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
18.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
19.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Musoma	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
20.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mbinga	Ndiyo	-	-	-	-	
21.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Rukwa	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
22.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
23.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
24.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
25.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tabora	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
26	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tanga	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
27.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tukuyu	Ndiyo	-	-	-	-	
28.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kyela	Ndiyo	-	-	-	-	
29.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Ngara	Ndiyo	-	-	-	-	
30.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Korogwe	Ndiyo	-	-	-	-	
31.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mpanda	Ndiyo	-	-	-	-	
32.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Njombe	Ndiyo	-	-	-	-	
33.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Namtumbo	Ndiyo	-	-	-	-	
34.	Maktaba Kuu ya	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	

	Taifa						
35.	Usafiri Dar-es-Salaam (UDA)	Hapana	-	-	-	-	Umiliki wa serikali haueleweki
36.	Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)	Ndiyo	-	-	-	-	
37.	Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
38	Kampuni ya Huduma ya Bahari	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
39.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
40.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama shinyanga	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

Aina ya Maoni ya Ukaguzi Yaliyotolewa 2011/2012

Hati Inayoridhisha	
Na.	**Shirika au Taasisi**
1.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha
2.	Bodi ya Mfuko wa Bima za Amana
3.	Mamlaka ya Udhibiti wa Soko la Mtaji (CMSA)
4.	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA)
5.	Mamlaka ya maendeleo ya Bonde la Rufiji.(RUBADA)
6.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania
7.	Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama Shinyanga
9.	Bodi ya Sukari Tanzania
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama
11.	Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI)
12.	Mamlaka ya Elimu Tanzania(TEA)
13.	Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)
14.	Chuo cha Wanyama Pori (MWEKA)
15.	Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA)
16.	Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma (CDA)
17.	Bodi ya Korosho Tanzania
18.	Mfuko wa Kuwekeza Tanzania (UTT)
19.	Benki Kuu ya Tanzania
20.	Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)
21.	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya
22.	Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO)
23.	Bodi ya Usajili wa Wakandarasi(CRB)
24.	Bodi ya kahawa Tanzania
25.	Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa
26.	Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Kiuchumi (NEEC)
27.	Jengo la IPS la NHC/PPF
28.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Majenzi (AQRB Wasanifu)
29.	Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha (AICC)
30.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza
31.	Baraza la Kiswahili Tanzania
32.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma
33.	Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)
34.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro
35.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mbeya
36.	Bodi ya Pamba Tanzania
37.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Babati
38.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam
39.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Masomo ya Biashara Moshi
40.	Kituo cha Uwekezaji Tanzania
41.	Kampuni ya Maendeleo ya Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro
42.	Chuo cha Usimamizi wa Fedha
43.	Benki ya Rasilimali Tanzania
44.	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF)
45.	Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa (GEPF)
46.	Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA)
47.	Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri Majini na Nchi Kavu (SUMATRA CCC)
48.	Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA)
49.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Rukwa
50.	Chuo Kikuu Mzumbe

51.	Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CARMATEC)
52.	Chuo cha Ardhi
53.	Chuo Kikuu Cha Mkwawa
54.	Chuo cha Ufundi Arusha
55.	Mamlaka ya udhibiti wa Nishati na maji (EWURA)
56.	Shirika la Elimu Kibaha
57.	Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)
58.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Iringa
59.	Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini
60.	Baraza la Taifa Usimamizi wa Mazingira (NEMC)
61.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA)
62.	Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB)
Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo	
Na.	**Shirika/Taasisi**
1.	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)
2.	Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization (TEMDO)
3	Mamlaka ya Majisafi na Maji Taka Songea
4	Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)
5.	Bodi ya Chai Tanzania
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga
7.	Baraza la sanaa Tanzania
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kigoma
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar-es-Salaam (DAWASA)
10.	Benki ya Posta Tanzania
11.	Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)
12.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi
13.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Moshi
14.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tanga
15.	Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere
16.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida
17.	Mfuko wa Mafao ya Wafanyakazi wa Umma (PSPF)
18.	Hifadhi za Taifa za Tanzania (TANAPA)
19.	Kampuni ya Mbolea Tanzania.
20.	Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE)
21.	Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW)
22.	Tume ya Ushindani (FCC)
23.	Kampuni ya Usambazaji Maji Dar es Ssalaam
Hati Yenye Shaka	
Na.	**Shirika/Taasisi**
1.	Shirika la Hifadhi ya Bahari Tanzania
2.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
	Hati Yenye Shaka na Suala la Msisitizo
Na.	**Shirika/Taasisi**
1.	Shirika Hodhi la Rasilimali za Mashirika ya Umma
2.	Mamlaka ya Majisafi na Maji Taka Mtwara
3.	Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)
4.	Chuo Kikuu cha Dodoma(UDOM)
5.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Musoma
6.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (TPRI)
7.	Chuo cha Taifa cha Usafirishaji
Hati mbaya	
Na.	**Shirika /Taasisi**
1.	Benki ya Twiga